Nipashe
Ijumaa Novemba 25, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581140
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ
nipasheTZ
nipasheTZ
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

SUPA JACKPOT
TZS.1,053,232,366
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




**Akiri** kuua madai ya kuitwa mchafu mbele ya msichana

UKURASA 3




UKURASA 13



# Ripoti ndege yaibua udhaifu



• **Shujaa** Majaliwa hajatajwa popote, wavuvi wapewa 'shavu'...*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 5
**KINANA AITWISHA ZIGO JUMUIYA YA WAZAZI**
MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, ameipa Jumuiya ya Wazazi wa chama hicho jukumu...

UKURASA WA 7
**SAFARI TRENI YA KISASA ZANUKIA**
SAFARI za treni ya kisasa inayotumia umeme (SGR) kutoka Dar es Saalam...

UKURASA WA 7
**MPANGO ASHANGAZWA BENKI KUTOPUNGUZA RIBA**
MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema anashangazwa na benki nchini...

## BoT yapiga marufuku ukopeshaji bila leseni

UKURASA 3




UKURASA 2

Rais Samia Suluhu akizungumza wakati akifungua Mkutano Mkuu wa 27 wa Chama cha Wanasheria wa Afrika Mashariki jijini Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# Samia asema bado anatafakari ruhusa NGO kuishtaki serikali

**MICHEZO** **YANGA SC: HAKUNA ATAKAYEPONA** UK.32 **KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA



Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana, kuhusu changamoto mbalimbali alizokutana nazo wakati wa ziara yake katika mikoa mitatu ya kusini. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Ripoti ya ndege yaibua udhaifu

**Na Waandishi Wetu**

RIPOTI ya awali ya ajali ya ndege ya Precision Air, imeibua udhaifu katika utayari wa kukabili majanga nchini huku ikishindwa kumtaja Jackson Majaliwa, aliyeonekana shujaa katika ajali hiyo kutokana na kuokoa watu kadhaa, bali ikielezea wavuvi kuwa ndio waliosaidia katika uokoaji.

Juzi, ripoti yenye taarifa hizo ilisambaa kwenye mitandao ya kijamii na ikakanushwa baadaye na Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, kupitia ukurasa wa twiter, jana jioni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alizungumza na waandishi wa habari kutoa ripoti ya awali.

Ripoti hiyo ilitolewa juzi na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, ikiwa ni baada ya siku 14 tangu kutokea kwa ajali hiyo, Novemba 6, mwaka huu, na ndani yake hakuna sehemu iliyomtaja shujaa huyo.

Katika ajali hiyo, Majaliwa alijizolea umaarufu na kuitwa shujaa, baada ya kitendo chake cha kuokoa baadhi ya manusura wa ajali hiyo ndipo serikali ilipomzawadia kwenda kusoma mafunzo ya uokozi katika Jeshi la Zimamoto na Uokozi hatimaye kupewa ajira serikalini.

Ajali hiyo ilitokea wakati ndege hiyo ikitoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kupitia Bukoba na ilianguka Ziwa Victoria na kusababisha vifo vya watu 19 na manusura 24.

Jana, Waziri Mbarawa alisema hali ya hewa katika Uwanja wa Ndege wa Bukoba iliripotiwa kuwa nzuri hadi saa 2:20 asubuhi lakini ilibadilika ghafla na mvua kunyesha ikiambatana na mingurumo ya radi na upepo mkali, mawingu mazito na ukungu.

Alisema ndege iliingia katika anga la Bukoba saa 2:25 asubuhi na kukuta hali ya hewa imebadilika dakika chache na kuanguka takribani dakika 20.

"Baadaye rubani alianza matayarisho ya kutua katika njia ya ndege kuruka na kutua namba 31 kutoka uelekeo wa ziwa. Kutokana na maelezo ya manusura, njia ya kutua ilikuwa inaonekana pamoja na alama zake kabla ya ndege kutua kwenye maji," alisema.

Waziri Mbarawa alisema uwanja huo uko katika hali nzuri ni wenye mwinuko wa futi 3,740 kutoka usawa wa bahari na una njia moja ya kuruka ndege yenye urefu wa kilomita 1.5. Alisema kiwanja kina kituo cha zimamoto ambacho kina gari moja na kikosi cha wafanyakazi 10.

**MLANGO WA NDEGE**

Kuhusu mlango wa ndege ulivyofunguliwa, alisema ulifunguliwa na mhudumu wa ndege kwa msaada wa abiria.

"Kama ripoti ya uchunguzi ilivyosema wananchi waliokuwa wanafanya shughuli za uvuvi walifika dakika tano baada ya ndege kuanguka. Waliendelea na juhudi za kufungua mlango kwa nje, hali iliyompa mhudumu wa ndege na abiria ujasiri wa kuendelea kufungua baada ya kuona nje ya ndege kuna msaada," alisema.

Prof. Mbarawa alipoulizwa kwa nini Majaliwa hajatambuliwa, alisema ripoti haijataja jina la mtu ndiyo maana hata mhudumu na abiria hawajatajwa kwa majina.

**VIKOSI VYA UOKOZI**

Kuhusu kuchelewa kwa vikosi vya uokozi, Mbarawa alisema "napenda kutoa ufafanuzi kuwa katika zoezi lote la uokozi pale ambako kuna ajali au janga lolote hususan ajali za majini upo muongozo wa kimataifa juu ya uendeshaji wa uokozi."

"Tunaongozwa na mkataba wa kimataifa kuhusu masuala ya utafutaji na uokoaji majini, ambao umetoa mwongozo kwamba ajali kwenye maji au ajali inaruhusu mtu au kikundi cha watu walioko karibu na eneo la ajali kuwajibika kwa vyombo vya uokozi na kutoa taarifa kwa vyombo vya uokozi na wataendelea kushiriki hadi vyombo au wataalam wafike.

Alisema mwongozo huo unaendana na utamaduni wetu wa kusaidia kuokoa na ndicho kilichofanywa na wavuvi na kwamba walitimiza wajibu wao kizalendo na inakubalika kimataifa.

**KUCHELEWA KWA BOTI**

Alisema kuna boti ya uokozi na kwamba wakati wa ajali boti ilikuwa mbali kwenye kutekeleza majukumu yake ya doria na ilipofika shughuli za kuokoa zilikuwa zimekamilika.

Alikiri kuwa uwezo wa kukabiliana majanga unatakiwa kuimarishwa ili kuokoa maisha ya watu.

Ripoti hiyo ilisema lengo halikuwa kutua kwenye maji kwani abiria hawakuambiwa wavue viatu au wavae makoti ya kujiokoa na matairi ya ndege yalifunguka kuashiria ndege ilikuwa tayari kutua uwanjani.

Ilieleza kuwa kilichotokea kilikuwa ghafla na rubani hakuwa amejiandaa nacho na kwamba iwapo uokoaji ungefanyika kwa wakati, watu wengi zaidi wangeokolewa. Pia ilisema marubani walishindwa kufungua mlango wa chumba chao na ule wa dharura juu ya ndege kutokana na msukumo mkubwa wa maji.

"Boti ya kitengo cha polisi cha majini ilifika saa 7:00 mchana eneo la tukio kwa sababu haikuwa Bandari ya Bukoba ilikuwa inafanya oparesheni zingine. Baada ya kufika walikuwa na changamoto ya ukosefu wa oksijeni na mafuta ya kutosha. Lakini kabla ya kufika, mvuvi mmoja tayari alianza kutoa maiti zilizokuwa ndani ya ndege," ilisema.

Kwa mujibu manusura wa ajali hiyo, ndege hiyo ilishuka salama lakini kabla haijakanyaga ardhi, ilibadili uelekeo kuelekea upande wa Ziwa Victoria.

Ripoti pia ilibainisha kuwa Uwanja wa Ndege wa Bukoba hauna mnara wa kuongozea ndege na kwamba mawasiliano yote hufanyika kwa kutumia mnara ulioko Mwanza, jambo ambalo Waziri alisema ni kawaida kuongozwa kwa mnara mwingine.

Pia ilisema rubani alijua anatua kwenye njia ya ndege na si kwenye maji na kwamba kuna uwezekano ndege ilisukumwa na upepo kwenda ziwani wakati akijaribu kutua.

## Samia atoa neno kuhusu NGO kuruhusiwa kuishtaki serikali

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema bado anatafakari namna ya kuirudisha Tanzania katika itifaki, inayoruhusu wananchi wake na mashirika yasiyo ya kiserikali kuishtaki nchi katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

Mwaka 2019 Tanzania ilijitoa katika itifaki hiyo, kwa kile kilichoelezwa ni baada ya kujiridhisha inapingana na sheria zake za ndani.

Akizungumza jana jijini hapa wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa 27 wa Jumuiya ya Wanasheria wa Afrika Mashariki (EALS), Samia alisema uamuzi wake huo unatokana na mwenendo wa mahakama hiyo wa kupokea mashauri mengi yanayoikandamiza serikali.

"Niseme nimeyasikia, ombi hilo limeshaletwa kwetu mara kadhaa, lakini naomba niwaambie, kama una rafiki wa kike mzuri, lakini mwenendo wake ukawa sio mzuri, utakaa naye? Si utampa muda akajirekebishe!

"Tumewapa nafasi wajirekebishe katika kesi zilizofunguliwa katika mahakama hiyo. Kesi zaidi ya 270, kesi 260 ni za Tanzania peke yake, na zote ni kinyume na serikali. Sasa tunarudi vipi?

"Nadhani ni muhimu kupeana nafasi ya kujitafakari ili kila mmoja aone atarudi vipi. Sisi tujirekebishe kwetu, na wao wajirekebishe; kila mtu atafakari anarudi vipi. Huku kwetu kuna msemo usemao, ukigongwa na nyoka na ukiona kitu kinafanania ni bora kumwaga zako dizeli ili ubaki salama," alisema.

Licha ya Rais Samia kueleza msimamo huo, alisema serikali imetoa ardhi yenye ukubwa wa ekari 10, kwa ajili ya kujenga makao makuu ya EALS.

Rais Samia pia aliwataka wanasheria wanapotekeleza majukumu yao ya kisheria, kuheshimu utawala wa sheria, wakati wa utekelezaji wa majukumu yao pamoja na kutetea wananchi na kuheshimu haki za binadamu. "Shirikianeni bega kwa bega na vyama vya kitaifa ili kukuza utoaji wa haki na utawala bora wa kisheria kwa sababu penye nia pana njia, onyesheni njia na sisi tutashirikiana pamoja.

"Vyama vyenu visiwe vyama vya kiuanarakati hasa katika kupambana na serikali. Vyama vyenu vijikite kwenye taaluma. Njooni na mikono misafi na moyo safi ili tufanye kazi pamoja kwa ajili ya kuwa na mtengamano wenye nguvu," alisema.

Pia aliwataka wanasheria hao kulinda uhuru na amani wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa lengo la kukuza uchumi. "Nchi haiwezi kufikia mageuzi ya ukweli katika uchumi kwa kukiuka utawala wa kisheria. Lazima tuwe kwakweli katika sheria na utawala bora. Sipendi Taifa linalokiuka utawala wa sheria kuwa sehemu ya nchi za EAC," alisema.

Kuhusu ombi la wanachama wa EALS kufanya kazi nje ya mipaka ya nchi zao, Rais Samia, alisema taaluma hiyo licha ya kuwa na malipo, wanatakiwa kuitambua wanapovuka mipaka, isiwe kwa ajili ya kufanya biashara iwe ni msaada wa kusaidia watu. Rais Samia, aliwataka wanasheria hao kuisaidia Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ambayo inakabiliwa na changamoto nyingi za kiusalama.

"Nchi zote za EAC tunakabiliwa na changamoto za kiusalama lakini siyo kama wenzetu wa DRC, lazima tuwasaidie ili wawe na amani," alisema.

Awali Rais wa EALS, Bernad Oundo, alimwomba Rais Samia, kuirudisha itifaki inayoruhusu wananchi na mashirika yasiyo ya kiserikali kufungua mashauri katika mahakama hiyo.



Wakazi wa Mtaa wa Ilolo Mashariki, Kata ya Sinde, jijini Mbeya, wakibeba miili ya watoto wawili waliouawa kwa kucharangwa na mapanga na anayedaiwa kuwa ni mama yao, Sharon Yohana, ambaye tayari anashikiliwa na Jeshi la Polisi juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# BoT yapiga marufuku taasisi kukopesha fedha bila leseni

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imepiga marufuku taasisi, kampuni na watu binafsi wanaojihusisha na biashara ya kutoa mikopo bila kuwa na leseni.

Kwa mujibu wa Gavana wa BoT, Prof. Florens Luoga, kufanya hivyo ni kinyume cha kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018.

"Tumebaini kuwapo kwa baadhi ya taasisi, kampuni na watu binafsi wanaojihusisha na biashara ya kutoa mikopo bila ya kuwa na leseni. BoT inapenda kuuarifu umma kuwa taasisi, kampuni na mtu binafsi wasio na leseni husika hawaruhusiwi kufanya biashara ya kukopesha," alisema Prof. Luoga katika taarifa iliyotolewa kwa umma.

Alisema adhabu kwa watakaobainika kujihusisha na biashara hiyo bila kibali wataadhibiwa kwa mujibu wa sheria ikiwamo kifungo.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 16(2)(a) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018, hatua zitakazochukuliwa kwa ukiukaji wa sheria hiyo ni pamoja na faini isiyopungua Sh. milioni 20 au kifungo kwa muda usiopungua miaka miwili," alisema.

Aliwataka wananchi kujiepusha kufanya biashara hiyo na watu, taasisi au kampuni zisizo na leseni.

"Sambamba na hilo, BoT inawataka wananchi kuepuka kukopa au kufanya biashara na taasisi, kampuni au mtu binafsi ambao hawana leseni. Orodha ya taasisi, kampuni na watu binafsi wenye leseni za biashara ya kukopesha zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania inapatikana kwenye tovuti yetu ya BoT," alisema Prof. Luoga.

# Wapoteza maisha kwa kuvuta hewa chafu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATU 33 hupoteza maisha kila mwaka kutokana na kuvuta hewa ya ukaa huku waathirika zaidi ni wanawake na watoto. Imeelezwa.

Mwakilishi kutoka Wizara ya Nishati, Joyce Kisano, alibainisha hayo jana wakati akizungumzia mada kutoka kwenye nishati chafu hadi nishati safi, kwenye jukwaa la sekta ya uziduaji madini, gesi na mafuta asilia lililoandaliwa na Taasisi ya Haki Rasilimali jijini hapo.

"Tatizo la matumizi ya nishati isiyo safi imekuwa ikileta madhara kwa afya za binadamu. Uvutaji wa hewa ya ukaa kila mwaka hutokea vifo vya watu 33 na waathirika ni wanawake na watoto na katika mkoa wa Kigoma kila mwaka wananchi 500,000 huwa wanapatwa na tatizo la upumuaji ndiyo maana serikali tunafanya mabadiliko ya kutoka kwenye mfumo wa nishati isiyo safi," alisema Kisano.

Kuhusu mada ya siasa za kijiographia zinazohusu sekta ya uziduaji, Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki, Josephine Lemoyan, alisema mifumo mizuri ya usimamizi wa rasilimali katika sekta ya uziduaji madini, gesi na mafuta itakuwa njia sahihi ya rasilimali hizo kunufaisha Watanzania na kuondokana na umaskini.

"Huwa naumia ninapoona rasilimali za madini, gesi na mafuta hazinufaisha Watanzania huku wakiendelea kuwa maskini, nashauri serikali iweke mifumo mizuri ambayo itakuwa chachu ya kunufaika na rasilimali hizi," alisema.

Baadhi ya wachimbaji wa madini akiwamo, Mary James, kutoka Chama cha Wachimbaji wa Wanawake (WIMO), waliomba serikali itunge sera nzuri itakayosaidia Watanzania kunufaika na rasilimali za nchi yao, pamoja na kusaidia wachimbaji wadogo wapate mikopo.

Naye Veronica Zano kutoka Shirika la Oxfam nchini Zimbabwe, alisema ili rasilimali zipate kunufaisha Afrika ni lazima pia kuwe na sera ya pamoja.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa HakiRasilimali, Adam Anthony, akifungua jukwaa hilo, alisema uwazi na uwajibikaji ukifuatwa katika sekta ya uziduaji utakuwa chachu ya maendeleo ya sekta hiyo na taifa kwa ujumla.

Alisema kila mwaka wamekuwa wakikutana na wadau mbalimbali wa sekta ya uziduaji, kubadilishana uzoefu na namna ya kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika sekta, pamoja na wananchi wanufaike na rasilimali zao.

# Akiri kuua kwa madai kuitwa mchafu mbele ya mwanamke

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemtia hatiani Paul Meshack (25), baada ya kukiri kumuua bila kukusudia William Lupemba, kwa madai ya kuambiwa mchafu mbele ya mwanamke aliyetajwa kwa jina la Dada Bonge.

Kabla ya mshtakiwa kufanya tukio hilo, alidai Lupemba alimkosa kumchoma na kisu Meshack mara sita bila mafanikio, ndiyo sababu iliyomfanya achukue kipande cha ubao akampiga nacho kichwani na kufariki dunia baada ya fuvu la kichwa kupasuka.

Hayo yalidaiwa jana na Wakili wa Serikali, Esther Chale, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Suzan Kihawa, wakati mshtakiwa huyo akisomewa maelekezo yake ya kosa, baada ya kukiri kumuua Lupemba bila kukusudia.

Chale alidai kuwa Oktoba 4, 2017, mshtakiwa alikuwa eneo la Vungunguti Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam.

Alidai marehemu alikuwa amekaa na dada aliyefahamika kwa jina la Dada Bonge, ndipo alifika Lupemba na kumwambia mshtakiwa anaonekana mchafu, maneno yaliyompa mshtakiwa hasira na kuanza kupigana.

Ilidaiwa kuwa katika ugomvi huo, Lupemba alichukua kisu na kujaribu kumchoma nacho mshtakiwa mara sita bila ya mafanikio ndipo mshtakiwa akachukua kipande cha mbao na kumpiga nacho marehemu kichwani na mguuni kisha akaanguka na kufariki dunia.

Alidai kuwa baada ya hapo mwili ulipelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa ajili ya uchunguzi na kubainika kuwa Lupemba alifariki dunia baada ya fuvu la kichwa kupasuka kutokana na jeraha la kichwani.

Mshtakiwa alikamatwa na kufikishwa kituo kidogo cha polisi cha Pugu Mnadani na baadaye alipelekwa Kituo cha Polisi Buguruni kwa mahojiano ndipo akafikishwa mahakamani.

Baada ya Chale kumaliza kusomewa maelezo hayo, aliyakubali yote na kudai kuwa ni kweli huku akionekana akiwa na sura ya huzuni na wasiwasi na pia akilia kwa mbali huku akijifuta machozi kwa kutumia kitambaa.

Hakimu Kihawa alisema kutokana na kukiri kwake kosa, maelekezo ya awali na vielelezo alivyopokea ikiwamo ripoti ya daktari, mahakama inamtia hatiani kwa kosa la kuua bila kukusudia.


NGOMENI ENTERPRISES

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA NA NOTISI YA KULIPA DENI.

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **CRDB PLC** makao makuu Dar es salaam, tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) tu ili uweze kulipa deni lote unalodaiwa Pamoja na gharama za Dalali. Kukaidi au kushindwa kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoweka kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N | JINA LA MTEJA | DHAMANA/MAHALI | TAREHE/MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | IRENE SPARTA MAMKWE | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KIVULEWILAYA YA ILALA | 10.12.2022, KUANZIA SAA 4 ASUBUHINA KUENDELEA. |
| 2. | EDSON BRIGHTON BEBWA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KIZINGAMAJOHE, BLOCK D, PLOT NO 122 WILAYA YA ILALA | 13.12.2022, KUANZIA SAA 4 ASUBUHINA KUENDELEA |
| 3. | KASHEBO JASSONY RWEZAULA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO SAVEIWILAYA YA KINONDONI | 16.12.2022. KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 4. | ANGELA TIMOTHY MSUYA/ ROBERT PASCAL NDIBALEMA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KIMARA | 20.12.2022 KUANZIA SAA 4 ASUBUHINA KUENDELEA |
| 5. | LIGHTNESS KITENGE | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KITUNDAWILAYA YA ILALA DAR ES SALAAM. | 22.12.2022 KUANZIA SAA 4 ASUBUHINA KUENDELEA |
| 6. | ERNEO BONIFACE MWAKANYASA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO NMC BWILINGU WILAYA YA CHALINZE PWANI | 3.1.2023 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 7. | POLIKARIPO GABRIEL MMASI | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KIMARASTOPOVER WILAYA YA UBUNGO | 28.12.2022 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NAKUENDELEA |

217165502

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na 75% atalipia ndani ya siku 14.
3. Mnuniuzi atakayeshundwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu, hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki,kutwaa nyumba na gharama nyinginezo zitzkuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua dhamana hizo muda wowote isipokuwa usiku.

MAWASILIANO:
CRDB BANK PLC HEAD QUARTER, NGOMENI ENTERPRISES, DSM. SIMU 0719974916/0753575752

RIPOTI MAALUM -2

# Mabadiliko ya tabianchi yalivyoathiri upatikanaji huduma ya maji, chakula

## ■Wataalamu wabaini kuna uhaba wa chakula

**Na Gwamaka Alipipi, aliyekuwa** CHEMBA

**JANA katika sehemu ya kwanza ya ripoti hii, kulikuwa na ushuhuda wa ugumu unaowakabili wakazi wa Halmashauri ya Chemba mkoani Dodoma kupata maji na chakula kutokana na ukame uliowakumba. Endelea kupata undani wa kinachojiri huko na hatua zinazochukuliwa...**



Wafugaji wa kata ya Paranga, wilayani Chemba, mkoani Dodoma, wakinywesha maji mifugo huku wananchi wakiwa wamepanga foleni wakisubiri kuchota maji hayo, mapema wiki hii. **PICHA: GWAMAKA ALIPIPI**

SHIDA zilizoko katika Kata ya Paranga pia zinashuhudiwa na Nipashe katika Kijiji cha Gwandi, Kata ya Gwandi, umbali wa Km sita kutoka mjini Chemba.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Gwandi, Mathei Doo anawasilisha kilio cha wenyeji, akisema wakulima wengi msimu uliopita walipata hasara kutokana na kuambulia mavuno kidogo, shida kuu ikiwa ni mabadiliko ya tabianchi.

"Mwaka jana wakulima wengi walivuna chini ya kiwango kutokana na mvua kuchelewa kunyesha. Kuna bwawa la kijiji lilichimbwa na TASAF lakini halijafikia kiwango cha kukidhi mahitaji ya wanakijiji na mifugo. Kwa sasa tuna mpango wa kuliongeza kina ili mvua itakapoanza kunyesha litufae nyakati za kiangazi," anasema.

Ni hoja inayopatiwa ufafanuzi na mkazi wa kijiji hicho, Adam Bakari anayetamka: "Hali ya hewa ni mbaya, mvua haijanyesha inavyotakiwa, nimelima mahindi ekari tatu, alizeti ekari tatu lakini ilipofika Machi mwaka huu, hali ikawa mbaya. Sijapata mavuno ya maana, yaani ni hasara tu."

Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Chacha anakiri wananchi katika eneo lake la uongozi kukabiliwa na ukame unaosababisha ugumu katika upatikanaji maji.

Ofisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Wilaya ya Chemba, Kamili Makia, katika mazungumzo na Nipashe, anasema hali ya upatikanaji wa chakula wilayani kwake ni nzuri, lakini kuna tatizo la bei kuwa juu.

Anabainisha kuwa kwa sasa gunia la mahindi wilayani Chemba linauzwa Sh. 90,000, bei ambayo ni sawa na iliyoko kwenye gunia la mtama na uwele.

"Wakazi wa Chemba wanalima mazao mengi, ila kwa asilimia kubwa wengi wao wanalima mahindi, alizeti, ufuta na mbaazi.

"Msimu wa kilimo wilayani Chemba unaanza Novemba hadi Aprili. Kwa wakati huu wananchi wapo katika maandalizi ya mashamba. Lakini kinachotupa wasiwasi ni taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) walituambia mvua kwa wakati huu zitachelewa na zitaanza wiki ya kwanza na ya pili ya Januari mwakani.

"Kama itakuwa hivyo kweli na sisi (Chemba) tutaathirika, kwa sababu sisi tuna vipindi vifupi vya mvua. Sasa ikianza Januari hadi Aprili tutakuwa katika hatari kubwa. Hivyo, tuombe Mungu hadi ifikapo Desemba mvua iwe imenyesha," anatahadharisha.

Anasema katika kutekeleza jukumu lake la msingi, anatoa elimu ya masuala ya kilimo kwa wananchi ili kuhakikisha kunakuwa na uhakika wa upatikanaji wa chakula na kupata cha ziada kwa ajili ya kujiongezea kipato.

Makia anabainisha kuwa baada ya kufanya tathmini ya awali kwa msimu uliopita, walibaini Wilaya ya Chemba ina upungufu wa chakula tani 25,000.

"Tunatarajia hali itakuwa mbaya kuanzia Desemba mwaka huu hadi Machi mwakani, hiyo ni miezi migumu katika upatikanaji wa chakula.

"Baada ya kufanya tathmini hiyo na kubaini shida hiyo, tuliamua kuzunguka vijijini kuwaeleza wananchi kwamba hali ya upatikanaji wa chakula siyo nzuri, hivyo akiba waliyonayo wasiuze, bali wakiweke ili kiwafikishe msimu ujao.

"Tumewashauri wananchi wauze mifugo na kununua chakula na kuwataka wapunguze mifugo yao kwa sababu mvua ikichelewa, madhara yake ni makubwa, ikiwamo mifugo kufa.

"Lakini hatukuishia hapo, tulifanya mawasiliano na NFRA (Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula) ambao walitaka kutuletea chakula cha kuuza kwa bei nafuu ili kudhibiti bei ya vyakula isipae Novemba, lakini tuliwashauri kwamba 'watu wetu kwa Novemba wana chakula, mnaweza kuleta chakula na kisinunuliwe'.

"Hivyo, tulikubaliana walete Desemba, kwa sababu ifikapo kipindi hicho akiba ya chakula kwa wananchi waliyonayo itakuwa imemalizika," anasema Makia.

Ofisa huyo pia anabainisha Wilaya ya Chemba ina hekta 45,000 zinazotumika kwa kilimo cha mahindi, zikiwa na uwezo wa kuzalisha tani 1.2 kwa hekta moja, yaani magunia sita kwa ekari moja.

Katika kuimarisha usalama wa chakula wilayani Chemba, Makia anasema kwa sasa wataalamu wa kilimo wamepewa pikipiki ili kuwafikia wakulima wengi na kuwapa elimu ya kilimo na kutatua kero zao.

Anasema Chemba ina maofisa kilimo 23 ambao wote wamepewa pikipiki, wakitoa huduma katika vijiji vyote 114 vya wilaya hiyo. "Pia tuna mkakati wa kuendelea kuhamasisha matumizi ya pembejeo bora za kilimo ikiwamo matumizi ya mbolea, mbegu bora na kuandaa mashamba mazuri," alisema.

Makia anakiri matumizi ya mbolea kwa wakazi wa Chemba yako chini kwa kuwa hawajahamasika katika matumizi hayo.

Anasema wakazi wa Chemba wanalima mashamba makubwa, hivyo wengi hawayahudumii vizuri, akilitaja ni jambo walilolipa kipaumbele kwa maofisa kilimo kuwaelimisha wakulima walime eneo dogo ambalo watamudu kulihudumia ipasavyo.

Meneja wa RUWASA Wilayani Chemba, Robert Mganga anakiri kuwapo hali isiyoridhisha katika upatikanaji wa maji wilayani humo.

Mganga anasema hali hiyo imesababishwa na ukame uliolikumba eneo lao, ukichagizwa na mabadiliko ya tabianchi.

"Vyanzo tulivyonavyo tunavyovitumia ni vile vya chini ya ardhi, tegemeo kubwa ni visima virefu. Tuna vijiji 114. Kati yake, 57 vinatoa huduma ya maji, hivyo siyo kwa mtawanyiko unaohitajika kwa mujibu wa sera.

"Vichache kati ya hivyo ndivyo vinakuwa na uhakika wa kutoa maji kwa asilimia 100, lakini vingine vipo tu havitoi maji na vinafanya kazi kwa asilimia tano," anasema.

Meneja huyo ana ufafanuzi zaidi kuhusu hali ya upatikanaji wa maji wilayani Chemba, akibainisha kuwa kuna vijiji 19 wilayani humo vina visima vilivyochimbwa lakini havijaendelezwa, hivyo havitoi huduma na mkakati wao uliopo ni kuvijenga.

"Kuna vijiji 38 havina vyanzo vya maji kabisa. Katika bajeti ya mwaka 2022/23 kuna visima 12 ambavyo vipo katika mpango wa uchimbaji, visima vilivyobaki wilaya ilipata msaada kutoka washirika wa maendeleo kutoka nje ya nchi," anafafanua.

Mganga anasema washirika hao wamewasaidia kufanya utafiti katika visima 18 na kwamba RUWASA wameanza kuchimba visima vitatu kati ya visima hivyo 18 ambavyo vimechimbwa katika maeneo ya Kichuruku, Kubi, Chemka.

"Visima hivyo vimekuwa na mafanikio makubwa kwa maana wametuwekea na miundombinu, hivyo imesaidia wananchi kupata huduma ya maji. Visima vilivyobaki tunaendelea kupambana navyo. Katika bajeti ya mwaka huu, kuna visima vinne tutavichimba ili kuongezea vile vingine 12," anasema.

Meneja huyo anasema kwa sasa wana taarifa ambayo wanairipoti katika sura mbili zinazojumuisha umbali, yaani mtawanyiko wa huduma ambao kwa mujibu wa sera, wananchi wanapaswa kupata maji ndani ya mita 400 kutoka kwenye makazi hayo. Mganga anasema utekelezaji wake hiyo kwa sasa umefikia asilimia 32.9.

Anasema sura ya pili ni kutumia chanzo, akifafanua kuwa wananchi wanapaswa kupata maji kutoka katika chanzo, utekelezaji wake ukiwa umefikia asilimia 50.

## HABARI KITAIFA



Naibu Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Richard Kangarawe (kushoto), akizungumza katika mkusanyiko wa wahitimu na wanafunzi wanaoendelea kabla ya mahafali ya 17 ya chuo hicho chuoni hapo, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kinana aitwisha zigo Jumuiya ya Wazazi maadili, malezi kwa vijana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, ameipa Jumuiya ya Wazazi wa chama hicho jukumu la usimamizi wa maadili na malezi kutokana na taifa kukabiliwa na mmomonyoko mkubwa wa maadili na kuhatarisha usalama wa nchi.

Akifungua mkutano mkuu wa taifa wa uchaguzi wa jumuiya hiyo jana jijini hapo, Kinana alisema kumekuwa na ongezeko la vitendo mbalimbali vinavyokiuka maadili na vingi vinatokana na malezi.

Jumuiya hiyo, alisema imetulia na inafanya kazi kwa umakini lakini ni vyema ikazingatia kwa misingi ya kuundwa kwake katika kusimamia malezi bora, maadili ndani ya chama na jumuiya.

Hata hivyo, alisema uchumi wa jumuiya bado haupo vizuri na kuwataka makatibu wa jumuiya na chama kutekeleza sera ya uwekezaji ili kuondokana na utegemezi wa ruzuku ambayo haitoshi.

"Hatuwezi kutegemea ruzuku kutoka kwa wasamaria na kwa wachangiaji kwa kuwa kufanya hivyo wakati mwingine ni kuhatarisha uhuru wa utendaji wa shughuli za jumuiya na chama,"alisema na kutaja jukumu la tatu ni kupunguza deni ambalo jumuiya imebeba.

"Nakupongeza Katibu Mkuu kwa kazi unayofanya. Wakati nikiwa Katibu Mkuu (wa CCM) sikuweza kufanya kama wewe ya kutizama maslahi ya watumishi wa chama ili kufanya kazi kwa uadilifu na uhodari," alisema.

Pia alipongeza uchaguzi ndani ya jumuiya hiyo za ngazi mbalimbali ulizofanyika kwa kuzingatia katiba ya chama na kanuni za jumuiya.

"Tumetumia muda kuchambua wagombea mbalimbali wenye sifa lakini nafasi ni chache haina maana kama walioachwa walikuwa hawana sifa, bali nafasi ni chache na watakaopita ni wachache zaidi na ndio utaratibu wa chama.

"Mwenyekiti wa CCM (Rais Samia Suluhu Hassan) anaamini mtachagua viongozi bora na si bora viongozi watakaokivusha chama chetu kupitia jumuiya ya wazazi kwenye uchaguzi mkuu wa 2025 na uchaguzi wa serikali za mitaa 2024," alisema.

Aliwataka watakaochaguliwa kujituma ili kufikia matarajio ya jumuiya na chama huku akisema uchaguzi ukiisha wabaki kuwa wamoja ili kujenga chama.

Kinana alisema kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita jumuiya imetekeleza lakini vipo viporo ambavyo wanachama watatambua mafanikio hayo ikiwamo mwongozo wa uendeshaji wa shule za wazazi.

Alisema miradi ya jumuiya imeongezeka kwenye maeneo mbalimbali lakini kutatua migogoro baina ya jumuiya na wawekezaji hadi kufikia hitimisho.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alisema viongozi watakaochaguliwa ni jeshi la kukitafutia ushindi wa chama kwenye chaguzi zijazo.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo anayemaliza muda wake, Dk. Edmund Mndolwa, alisema katika uongozi wake mambo mbalimbali yamefanyika ikiwamo kurudisha heshima ya jumuiya, kuboresha utawala bora na kuongeza mishahara.

Awali Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Gilbert Kalima, alisema kwa miaka mitano ijayo jumuiya imejipanga kutilia mkazo masuala ya maadili.

# Akana kumkata mwenzake jicho, sikio

**Na Kulwa Mzee**

MKAZI wa Gerezani Kariakoo, jijini Dar es Salaam, Abdul Shabani, amekana kumkata sikio na jicho Zawadi Juma aliyekuwa akimzuia kuingia katika uwanja wa michezo wa Jakaya Kikwete saa 4:30 usiku.

Shabani anayedaiwa kuwa mwanafunzi, alikana maelezo ya awali ya mashtaka dhidi yake jana katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala mbele ya Hakimu Mkazi Fadhili Luvinga, aliposomewa maelezo hayo na Wakili wa Serikali, Zamir Masinde.

Wakili Masinde alidai Aprili 10, mwaka huu, saa 4:30 usiku, mshtakiwa Abdul alikuwa maeneo ya Gerezani Kariakoo katika uwanja wa michezo wa Jakaya Kikwete.

Inadaiwa mshtakiwa alikuwa akitaka kuingia katika uwanja huo wa michezo, akazuiwa kufanya hivyo na Juma lakini katika kulazimisha kuingia, alimjeruhi kwa kisu katika sikio la kushoto na jicho la kushoto.

Wakili Masinde alidai Zawadi aliomba msaada akatokea Juma Robert kumsaidia lakini mshtakiwa alimjeruhi mtoa msaada kwa kisu kwenye mkono wa kushoto na mguu.

Inadaiwa mshtakiwa alidhibitiwa katika eneo la tukio na kufikishwa katika Kituo cha Polisi Msimbazi na kuandika maelezo ya onyo huku akikiri kutenda makosa hayo.

Kutokana na maelezo hayo, Hakimu Luvinga alimtaka mshtakiwa kujibu kama ni ya kweli au si kweli.

Mshtakiwa alidai anakubali taarifa zake binafsi lakini anapinga kuwapo katika Uwanja wa Michezo wa Jakaya Kikwete saa 4:30 usiku Aprili 10, mwaka huu. Pia alikana kumkata sikio na jicho Zawadi pamoja na kumjeruhi Robert.


TEMBO NICKEL

**TEMBO NICKEL CORPORATION LIMITED**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUFANYA TATHMINI YA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA KIJAMII KATIKA MRADI WA UJENZI NA USIMIKAJI WA KINU CHA UCHENJUAJI WA MADINI KINACHOMILIKIWA NA KAMPUNI YA TEMBO NICKEL WILAYANI KAHAMA MKOANI SHINYANGA**

Tembo Nickel Corporation Limited (Tembo Nickel) inakusudia kujenga kinu cha kuchenjua aina mbali mbali za madini ya chuma katika wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga kwa ajili ya kuchenjua madini ya nikeli ambayo yatakuwa yakizalishwa kutoka mradi wa uchimbaji madini ya nikeli wa Kabanga (Kabanga Nickel project) uliopo wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera. Mradi utamilikiwa na kusimamiwa na kampuni ya Tembo Nickel ambayo ni kampuni inayomilikiwa kwa ubia ulioundwa chini ya makubaliano kati ya Kabanga Nickel Company Limited na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Chini ya ubia huu, Kabanga Nickel inamiliki asilimia 84 na Serikali ya Tanzania inamiliki asilimia 16 ya hisa.

Kanuni ya 17(2a) cha kanuni za udhibiti na ukaguzi wa athari za kimazingira ya mwaka 2005, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2018, inamtaka muendeleza mradi kutoa taarifa kwa umma kuhusu mradi pendekezwa kwa muda wa wiki mbili mfululizo kwenye chombo cha habari ambacho kinasikika nchi nzima. Kwa mantiki hiyo taarifa hii inatolewa kuutarifu umma kuwa kampuni ya Tembo Nickel imeingia mkataba na kampuni ya kutoa ushauri elekezi ya MTL Consulting Company Limited (MTL) kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii kwa mradi pendekezwa kwa niaba ya Tembo Nickel.

Mradi pendekezwa upo ndani ya leseni ya uchimbaji madini ya Buzwagi, takribani umbali wa Kilomita 4, kusini-mashariki mwa mji wa Kahama.Kwa vile Mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi uko mbioni kufungwa, Halmashauri ya Mji wa Kahama inampango wa kubadilisha matumizi ya eneo la mgodi wa Buzwagi kuwa kitovu cha biashara. Tembo Nickel imeingia makubaliano na Halmashauri ya Mji wa Kahama kutumia sehemu ya eneo lililopangwa kuwa kitovu cha biashara kwa ajili ya ujenzi na usimikaji wa Mtambo wa Uchenjuaji wa Madini. Eneo la mradi linatarajiwa kuwa na mita za mraba laki tano na hamsini (m2 550,000). Eneo la mradi linaweza kuongeza hadi kufikia mita za mraba laki saba na elfu arobaini (m2 740,000) endapo uzalishaji utaongezeka kutokana na kuongezeka kwa uchimbaji kwenye maeneo yaliyotafitiwa zaidi, hii itasababisha kupanuliwa kwa miundo mbinu iliyojengwa awali ikiwemo miundo mbinu ya madini ghafi (makinikia ya madini) ili kuongeza uzaishaji wa madini yaliyosafishwa.

Taarifa hii imetolewa kuomba maoni na mapendekezo ya wadau au pande zozote ambazo kwa namna moja au nyingine wanaweza kuathiriwa na mradi huu. Mtu yeyote mwenye maslahi, maoni, wazo au maarifa (ufahamu) kuhusu athari zozote za kimazingira na kijamii za mradi pendekezwa anaweza kuwasiliana au kuwasilisha maoni yake kwa maandishi kwa anwani zifuatazo

**The Director General,**
**National Environmental Management Council (NEMC),**
**P.O. Box 63154, Regent Estate,**
**Dar es Salaam, Tanzania.**
**Tel: +255 22 2774889**
**Email: nemc@nemctz.org**

**MTL Consulting Company Limited**
**Victoria House, 9th Floor, Plot No.37, Regent Estate, New Bagamoyo Road**
**P.O. Box 77894 Dar Es Salaam.**
**Tel: +255 22 2926117,**
**Mobile: +255767360 225/743127611**
**Ema: info@mtlconsulting-tz.com**

217164002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TANESCO inapaswa kubadilika katika uzalishaji umeme nchini

**SHIRIKA** la Umeme Tanzania (TANESCO), juzi liliutangazia umma wa Watanzania kuwa ukame na matengenezo yanayoendelea kwenye vituo vya kuzalisha umeme, ndizo sababu kubwa za kukosekana kwa nishati hiyo muhimu kwa matumizi ya kawaida ya kila siku na maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Katika taarifa yake, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, aliwaeleza waandishi wa habari kuwa katika vyanzo vyote vya umeme, megawati 300 hadi 350 zimepungua katika uzalishaji kwa siku za hivi karibuni kutokana na vyanzo kukauka kwa sababu ya ukame na matengenezo kwenye baadhi ya mitambo.

Mkurugenzi huyo alibainisha kwamba katika vyanzo vya maji vya Kihansi, Kidatu, Mtera, Nyumba ya Mungu na Hale kiwango cha maji kimepungua kiasi cha kusababisha uzalishaji wa umeme kupungua kwa kiwango kikubwa. Sababu kubwa inayotolewa ni ukame ambao umeathiri maeneo mbalimbali ya nchi, hivyo kusababisha kina cha maji kupungua.

Katika kituo cha Pangani, kwa mfano ambacho awali kilikuwa kinazalisha megawati 68 kwa sasa kinazalisha megawati 10 na kufanya upungufu wa 58. Bwawa la Mtera uzalishaji umepungua kutoka megawati 180 hadi 175 huku Nyumba ya Mungu iliyokuwa inazalisha megawati nane, kwa sasa inazalisha megawati tatu.

Hali hiyo inadhihirisha kuwa kuna hatari kubwa katika upatikanaji wa nishati hiyo ni tatizo kubwa kama hakutakuwa na uwezekano wa kuwapo kwa mvua hivi karibuni ili kujaza mito ambayo inayajaza mabwawa ya kuzalisha umeme.

Pamoja na kuwapo kwa hofu hiyo na mgawo wa umeme kuendelea kutikisa, mipango ya muda mfupi, wa kati na mrefu wa TANESCO katika kukabili hali hiyo inaleta matumaini ya kuwapo kwa unafuu. Katika taarifa yake, Chande alieleza kuwa shirika limejiandaa na mipango ya kukabiliana na tatizo hilo kwa vipindi tofauti.

Miongoni mwa mipango hiyo ni kufanya matengenezo katika mitambo ya gesi ya Ubungo na Kinyerezi hali ambayo itarejesha kiwango cha umeme kwenye gridi ya taifa na wananchi kuondokana na adha hiyo.

Pamoja na mikakati hiyo, TANESCO inapaswa kubuni mikakati ya muda mrefu kuhakikisha umeme unapatikana kwa wingi ili kuhakikisha maendeleo ya sekta zote yanakuwa endelevu tofauti na ilivyo sasa. Hivi sasa, kutokana na kukosekana kwa umeme wa uhakika kwa sababu ya mgawo, baadhi ya shughuli za uzalishaji zimesimama au kusuasua.

Hilo linajidhihirisha wazi baada ya juzi, Mkurugenzi wa Sera na Uchechemuzi wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), Akida Mnyenyelwa, kuzungumza na chombo kimoja cha habari kuwa mgawo unawapa maumivu kwenye shughuli za uzalishaji kwa kuwa gharama zitaongezeka na watalazimika kutumia majenereta kuendesha mitambo yao.


Maelezo ya CTI yanabainisha kuwa shughuli za uzalishaji kwa sababu ya kukosekana kwa umeme wa uhakika zitapungua na wengine kusimama kwa sababu ya gharama kubwa za umeme kutokana na matumizi ya majenereta.

Suala la mgawo wa umeme si geni kwa sababu limekuwapo kwa zaidi ya miaka 30 sasa lakini TANESCO imekuwa ikitoa sababu zile zile za upungufu wa maji katika mabwawa ya kuzalisha nishati hiyo. Jambo la kujiuliza, je, zaidi ya miaka 60 ya uhuru bado tunategemea maji kupata umeme wa uhakika?

Ni wazi kwamba vipo vyanzo vingi vikiwamo makaa ya mawe ambayo yako nchini kwa wingi pamoja na gesi na upepo.

Cha msingi, TANESCO inapaswa kubadilika na kuwa na mipango ya muda mrefu kwa kutumia vyanzo mbadala wa maji katika kupata umeme wa uhakika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Enyi ndugu TANESCO, utaratibu huu wa kutoa taarifa za umeme uwe endelevu

Na Adam Fungamwango

**HADI** sasa nchi nzima tuko kwenye mgawo wa umeme. Hilo tena siyo suala lenye jibu la kubahatisha, kwani uhalisia na wenye nyumba wenyewe wameweka mambo hadharani kwamba mgawo huo upo.

Na tukirudisha mkanda nyuma zaidi, jambo hilo si geni hata kidogo kwenye jamii yetu inakuwapo, na kisha inatoweka na ndiyo mazingira yaliyotawala miaka nenda rudi tangu zama hizo naachana na umri wa udogo, kisha naingia ujana fulani, hadi tarehe hizi ambazo mabinti zetu wanatuwahisha ng'ambo ya pili tunakuwa mababu tutake tusitake, msamiati wa mgawo wa umeme upo pale pale, ambao nikiutafakari naufananisha na ugonjwa wa malaria, kuusambaratisha ni mtihani kweli kweli, unakuja na kuondoka ndani ya familia, kuanzia kule nilikozaliwa mpaka kikosi kipya ninachokiunda mwenyewe.

Nakumbuka wastani wa miongo miwili na ushehe iliyopita, tukatangaziwa kwamba 'mgao wa umeme sasa baibai, kuonana tena majaliwa.' Lakini, ikasonga idadi fulani ya miaka tukaona majaliwa hayo ya kuonana yamerudi tena, mheshimiwa mgao wa umeme kafika.

Hapo ndipo inatuondolea uaminifu katika kile kipengele cha 'kuonana tena ni majaliwa.'

Kikubwa wenyewe tulichokijengea kisaikolojia, tunapitia likizo fulani, kisha tunarudiana na mpambano wa 'no umeme.'

Naam! Juzi tena, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), baada ya minong'ono kutawala kila kona na kila mtu akinena lake 'kwanini' na 'vipi' za kumwaga, wakaona isiwe tabu, sisi ndiyo tunawajibika na shirika hili ni la umma, kwa maana hiyo mali yao tutake tusitake ni lazima tukawaeleze nini kinachoendelea kwenye taasisi yao wananchi ambao pia wanatumia huduma hiyo. Ukaitishwa mkutano wa waandishi wa habari, mafundi wa kuchakata hizo taarifa wakaufikishe umma nini kinaendelea kutokana na upungufu huo wa umeme.

Jibu Kuu, likaangukia mlemle walikonena wenzao wasambaza maji walipokabiliana na shinikizo kama hilo la watoa umeme, mtuhumiwa mkuu yule yule ukame na ukosefu wa mvua.

Ni ufafanuzi uliozama zaidi ukiainisha bwana ukame na ubovu wa mitambo kwa kiasi fulani, wamesababisha kutoweka kwa megawati zaidi ya 400 za umeme, kilio kikiangukia kila sekta, kuanzia wazalishaji viwandani na wenzangu na mimi na huduma mbalimbali.

Hakuna namna ya kuendelea kushikana mashati, kwani mtuhumiwa ameshapatikana, ila cha kuongeza hapo tabia ya uungwana ulioonyeshwa na wazalishaji umeme hao kuwafahamisha wamiliki ambao ni umma nini kinaendelea na mzizi mkuu wa shida ni nini.

Kutoa taarifa ni jambo muhimu linalosambaratisha kelele za umma, minong'ono isiyofaa ikiwamo kwenye mitandao ya kijamii na kushikana uchawi.

Hata kama baadhi ya watu watakuwa wanalalamika kutokana na machungu ya umeme, lakini kitendo cha TANESCO kuwatangazia wananchi siku fulani kutakuwa na mgawo sehemu fulani, hii angalau inawafanya watafute kitu kibadala.

Mfano mdogo, mtu yupo Mikocheni anajua Mbagala kuna mgao, basi kama kuna mechi hata ya Kombe la Dunia atatazama mechi hadi inaisha ndipo atarejea, ambapo kama isingekuwa hivyo amerudi tu kuwahi mechi na kukutana na giza, akaanza kulaumu kwa nini asingekaa huko huko hadi mechi iishe.

Kutoa taarifa mbali na kujiandaa inasaidia hata kisaikolojia tu ile kufahamu leo kuwakuwa na mgao. Ni kama vile mtu kakukanyaga halafu anakwambia 'pole', ni kama maumivu yake hayaumi kwa sababu za kisaikolojia tu, tofauti na yule ambaye anakukanyaga halafu anaanza kukulaumu kuwa 'huoni?' au 'kapande taxi' kama unataka starehe.

Kama hili la kutoa taarifa ya mgao wa umeme nawapa heko, waendelee hivyo hivyo, na ni jambo la kupongezwa. Lakini angalizo ni kwamba yale yote ambayo yamewabainisha kuwa ni mapungufu yanayosababisha umeme ambayo yapo kwenye uwezo wa kibinadamu wayafanyie kazi mara moja ili mgao umalizike.

## Mpango ashangazwa benki kutopunguza riba

**Na Neema Emanuel,** MWANZA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema anashangazwa na benki nchini kushindwa kupunguza riba za mikopo inayotoa wakati suala hilo ni kilio cha muda mrefu na serikali imekuwa ikiagiza mara kwa mara kufanyika kwa suala hilo.

Kutokana na hali hiyo, amezitaka benki hizo kufanya uchambuzi wa gharama za uendeshaji ili kutimiza azma hiyo na kuwawezesha wananchi kuwa na ahueni katika mikopo wanayochukua kwenye taasisi za fedha.

Dk. Mpango alisema hayo jana jijini hapa katika maonyesho ya Wiki ya Huduma ya Taasisi za Fedha kitaifa na kuzitaka benki kuondokana na riba ya asilimia 16 inayotozwa kwa sasa.

"Riba ya mkopo wastani wa asilimia 16 bado ni mzigo kwa Watanzania walio wengi kumudu pamoja na hatua zinazoendelea kuchukuliwa kupunguza hatari za kifedha kila benki. Kupitia umoja wao wakachambue mizizi ya tatizo hilo na kupunguza zaidi riba kwa wakopaji.

"Pigeni darubini gharama zenu za uendeshaji na matumizi mengine ikiwamo bonasi zenu. Serikali imekuwa ikitoa rai hii kwa muda mrefu sana lakini mwitikio wa benki bado ni mdogo sana kuvutia wananchi walio wengi wa kipato cha chini na kati kukopa na kurejesha mikopo," alisema Dk. Mpango.

Alisema benki zinakopeshwa kwa asilimia tatu lakini zenyewe zinakopesha wakulima kwa riba ya asilimia tisa na kwamba kwa nini zisiwatoze asilimia tano. Alizitka benki kutazama upya masharti ya mikopo ikiwamo dhamana ya mali isiyohamishika kwa kuwa ni kikwazo kwa wajasiriamali.

Dk. Mpango alisema sharti hilo ni gumu hususani kwa wanawake na vijana wanaohitaji mikopo kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi.

"Kinamama wameeleza baadhi ya mila zetu zinawabagua kumiliki nyumba kwani ni wachache sana. Sasa unapomdai hati ya nyumba anafanyaje? Angalieni uwezekano wa kutumia historia nzuri ya wakopaji kama dhamana," alisema.

Kuhusu upatikanaji wa huduma za fedha, Dk. Mpango alisema asilimia 8.6 ya wananchi wanaoishi vijijini ndiyo wanaopata huduma za kibenki, hivyo akaziomba benki kupanua wigo wa huduma zao vijijini na kuongeza mitaji yao ili wakopeshe watu zaidi na kukuza akiba na kupunguza utamaduni wa kuhifadhi fedha kwenye vibubu.

Alisema serikali itaendelea kuboresha miundombinu na kwamba Benki Kuu ya Tanzania (BoT), imelegeza masharti ya usajili wa huduma za mawakala wa benki.

Dk. Mpango aliongeza kuwa kwa sasa teknolojia ya kidijitali imekuwa na itasaidia kuwafikia wananchi wengi huku akizitaka benki na taasisi zote za fedha kutobweteka na ukuaji wa amana wa asilimia 13 kwa mwaka 2021.

Kwa mujibu wa Makamu wa Rais, bado mikoa ya Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kusini ina mchango kidogo katika amana za benki kwa chini ya asilimia tisa.

Kuhusu mchango wa sekta ya fedha kwa pato la taifa, Dk. Mpango alisema bado upo chini ya asilimia nne kuanzia mwaka 2018 mpaka 2021.




Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhaji Abdul Maulid (katikati), akikata utepe kuzindua jarida la kisayansi liitwalo OYLA Africa Magazine jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mkurugenzi wa OYLA Afrika, Yevgeniy Semikov (kushoto) na Meneja wa OYLA Afrika Godfrey Lugalambi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Safari za treni ya kisasa zanukia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SAFARI za treni ya kisasa inayotumia umeme (SGR) kutoka Dar es Saalam kwenda Morogoro zinatarajiwa kuanza rasmi Februari, mwakani, imeelezwa.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alibainisha hayo jana jijini hapo alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa reli ya kisasa kipande cha pili Morogoro hadi Makupora mkoani Dodoma kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Alisema kipande cha reli hiyo kutoka Dar es Saalam kimekamilika kwa kiasi kikubwa na kinachofanyika hivi sasa ni majaribio katika mifumo ya umeme.

"Kwa asilimia kubwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro chenye urefu wa kilomita 300, kimeshakamilika na sasa tumeshaanza kupokea mabehewa na vichwa vya treni ili tuanze majaribio hadi Januari, mwakani ili inapofika Februari, treni ianze kazi katika kipande cha kwanza cha mradi huu mkubwa," alisema Kadogosa.

Aidha, alitoa ufafanuzi kuhusu maneno ambayo yamekuwa yakiendelea kwenye mitandao ya kijamii kuhusu mabehewa ambayo serikali imeanza kuyapokea kwa ajili ya treni hiyo ya kisasa.

"Nadhani ni uelewa tuu kwa kuwa ni vitu vigeni bado lazima tuendelee kuelimishana. Watu wanadai kuwa mabehewa tuliyoleta ni tofauti na serikali iliyosema lakini haya ambayo yameanza kuingia ni kwa ajili ya masafa marefu hayo mengine ya safari fupi yaani treni ya mchongoko pia yatakuja yataingia Juni, mwakani. Tayari yameanza kutengenezwa kiwandani, hivyo tutakuwa na aina zote," alisema.

Kadogosa pia aliwashauri wakuu wa mikoa kuhakikisha viwanda vinvyojengwa vinawekwa maeneo ambayo ni jirani na reli hiyo ili iwe rahisi wakati wa ubebaji wa mizigo.

Pia alisema mradi huo wa reli ya kisasa kutoka Dar es Saalam hadi Mwanza unatarajia kukamilika ifikapo mwaka 2026 na Sh. trilioni 16.67 kitatumika.Mwenyekiti wa Bodi ya TRC, Prof. John Kondoro, alisema sababu za mradi huo katika baadhi ya vipande kwenda muda zaidi ya ule ambao upo kwenye mkataba ni mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19.

"Tumekuwa nyuma ya muda kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo kuhamisha shule, makazi na baadhi ya miundombinu ambayo ipo nje ya shirika letu ambazo zilikuwa kwenye eneo la mradi lakini mlipuko wa UVIKO-19 ulisababisha twende nje ya muda ambao tuliutarajia katika mkataba," alisema.

Akizungumza baada ya kukagua ujenzi wa jengo la stesheni kuu ya mkoa wa Dodoma, Waziri Mkuu alisema miradi yote ya kimkakati, ukiwamo wa SGR, haitakwama wala kusimama utekelezaji wake.

"Nimefanya ziara ya kukagua miradi hii ya kimkakati inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini na niwahakikishe kuwa hakuna maradi ambao utakwama au kusimama utekelezaji wake. Tutahakikisha yote zinakamilika kama ambavyo tumeambiwa hapa leo (jana) kuwa vipande vyote vitano vya mradi huu tayari vina makandarasi," alisema.

Majaliwa alisema mradi huo ni fursa kwa wazawa kujifunza ujuzi mbalimbali ili utakapokamilika watumike kusimamia uendeshaji na matengenezo mbalimbali.

## KABWELA





Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni inayotoa mafunzo ya uongozi na menejimenti na huduma bobezi ya DUTENI, Ebony Mbeteni, akizungumza wakati wa semina kwa wakurugenzi wa kampuni zaidi ya 44 jijini Dar es Salaam hivi karibuni, iliyolenga kutoa ujuzi wa kuboresha utendaji kazi kwa watoa maamuzi wa kampuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TIB yawataka Watanzania kuchangamkia fursa mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo TIB imehamasisha umma kuchangamka fursa za mikopo zinazotolewa, ili kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo kwa ajili ya kuchagiza ukuaji wa uchumi nchini.

Wito huo ulitolewa jana na Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa Benki ya Maendeleo TIB, Giusy Mbolile, kwenye maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yanayoendelea jijini Mwanza.

Alisema TIB ina wajibu wa kuwezesha upatikanaji wa mitaji ya muda mrefu na wa kati kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi nchini hivyo amewasihi wawekezaji wenye miradi ya kimkakati kuitumia benki hiyo, ili kufanikisha miradi hiyo.

"TIB ni taasisi ya serikali iliyoanzishwa kwa malengo ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji ya muda mrefu na wa kati kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi, hivyo nawasihi wawekezaji wenye miradi ya kimkakati kuitumia benki ili kufanikisha uwekezaji huo," alisema.

Aliongeza kuwa benki hiyo inatoa mikopo kwenye sekta mbalimbali ikiwamo viwanda, madini, huduma, miundombinu, nishati na maji pamoja na programu za mikopo ya wawekezaji wadogo na wakati (SMES).

Alisema mikopo hiyo inatolewa ili kuchagiza ukuaji wa shughuli za kiuchumi, ili kutekeleza mipango mbalimbali ya serikali inayolenga kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

# Samia mgeni rasmi kilele Siku ya Ukimwi

**Na Said Hamdani,** LINDI

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yatakayofanyika kitaifa Desemba mosi, mkoani hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, alisema maadhimisho hayo yataambatana na jamii kujitokeza kupima afya kwa hiari.

Katika taarifa yake aliyosoma kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zaynab Telack, Ndemanga alisema kuanzia leo wananchi wataruhusiwa kupima afya zao.

Aidha, alisema viongozi wengine wanaotarajiwa kushiriki maadhimisho hayo ni mawaziri wa afya, elimu na utumishi.

Mkuu huyo wa wilaya aliwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki, ikiwa ni pamoja na kupima VVU, shinikizo la damu, saratani ya shingo ya kizazi, kifua kikuu na watakaopenda wataombwa kuchangia damu.

"Maadhimisho haya yanafanyika mkoani hapa kutokana na kwamba ni miongoni mwa mikoa yenye maambukizi ya VVU, mwaka 2017 ulikuwa na maambukizi asilimia 0.3," alisema.

Kwa mujibu wa Ndemanga, watu 28,753 wanaishi na VVU kati yao 26,147 wako kwenye utaratibu wa matumizi ya dawa za kufubaza virusi (ARV), huku 2,506 wameacha huduma.

# Jela maisha kwa kubaka mtoto wa miaka minne

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Ludewa, mkoani Njombe, imemuhukumu mkazi wa Kijiji cha Kiwe, Simon Msanga (24), kifungo cha maisha gerezani kwa kosa la kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka minne.

Akisoma hukumu hiyo jana Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Isaac Ayengo, mshtakiwa huyo amekutwa na hatia ya kosa alilolitenda Mei 30, mwaka huu majira ya saa 10 jioni.

Alisema ushahidi uliotolewa uliithibitishia mahakama kuwa mshtakiwa alifika nyumbani kwao mtoto huyo na kumkuta akiwa nje anacheza kisha akamchukua na kuingia naye kichakani.

Alisema wakati akiingia naye kichakani kaka wa mtoto huyo mwenye umri wa miaka saba alikuwa ndani, lakini alimwona mtuhumiwa wakati anamchukua mdogo wake ndipo akamfuata kimya kimya na kumshuhudia akimvua nguo.

Alisema kaka mtu alikimbia kwenda kumwambia mama yao aliyekuwa kanisani na wakati wanakwenda walipishana na mtuhumiwa.

Alisema kama alimuonyesha mama yake lakini aliwahi kwenda kumkagua mtoto na kukuta ameharibiwa ndipo akamfuata mtuhumiwa ambaye alikuwa katika klabu cha pombe.

Hakimu huyo alisema mama huyo aliwaomba waliokuwapo klabuni wakamkamata na kumpeleka kituo cha polisi na baadaye alifikishwa mahakamani.

Hakimu Ayengo alisema alisikiliza ushahidi wa pande zote mbili na ushahidi wa upande wa mashtaka ukionekana kuwa na nguvu na kuamua kutoa hukumu hiyo kwa mujibu wa kifungu cha sheria namba 131(3) cha kanuni ya adhabu sura ya 16 marejeo ya 2022.

Katika utetezi wake mtuhumuwa aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ana tatizo la kiafya, anaumwa ugonjwa wa kifafa lakini mahakama ikamuamuru kutumikia kifungo hicho kwa mujibu wa sheria.

## HABARI KITAIFA



# Mwanafunzi apotea

**Na Elizabeth Zaya**

JUNIOR Miller (14) (pichani juu) mkazi wa Mbeya Mjini, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari ya Airport mkoani humo amepotea.

Kwa mujibu wa kaka wa mtoto huyo, Patrick Juma, mdogo wake huyo alipotea Novemba 20, mwaka huu, alipoaga kwenda kwenye masomo ya ziada ambayo huyapata katika shule hiyo ya sekondari.

Alisema wakati anaondoka nyumbani kwenda shuleni, alipewa fedha na baba yake Sh.150,000, ili akampatie mwalimu wake kwa ajili ya malipo ya masomo yake hayo ya ziada, lakini baada ya kupotea na familia yake kufuatilia walibaini kwamba hakupeleka fedha hizo kwa mwalimu.

"Mtoto aliondoka nyumbani saa tatu asubuhi na akapewa fedha kwenda kumpatia mwalimu wake kwa ajili ya kulipia masomo yake hayo ya ziada, lakini baada ya kufuatilia ikabainika kwamba hakupeleka japokuwa shuleni alifika na kuondoka kabla ya muda wa masomo kuisha,"alisema Patrick.

"Tumezungumza na rafiki yake ambaye anaishi Mwanjelwa, ametuambia kwamba siku hiyo hiyo aliendа nyumbani kwao mchana akaazima baiskeli, wakampatia akaondoka, na ilipofika saa mbili ya usiku aliirejesha na kuwaambia kwamba anarudi nyumbani, lakini hakufanya hivyo mpaka hivi tunavyozungumza."

Patrick alieleza kuwa mdogo wake hajawahi kupotea kabla ya hapo.

"Tabia ya huyu mtoto ni njema tu na hatujawahi kusikia kwamba ana makundi mabaya na ndiyo maana tunapata shida kujua nini kimemkuta, tunaomba watakaomwona popote watusaidie, maana baada ya kukosekana kwake, tuliripoti kituo cha polisi na tukazunguka kila mahali ikiwamo hospitali bila mafanikio,"alisema Patrick.

Alisema mdogo wake wakati anaondoka nyumbani, alivalia suruali yenye rangi ya kijivu na shati ya drafti yenye rangi nyeupe na kijani pamoja na begi la shule lenye rangi ya bluu na kwamba rangi ya ngozi yake ni nyeusi na ni mwembamba, mrefu.

Aliomba kwa atakeyemwona awasiliane nao kwa namba **0767 626206, 0769906059** au atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

# Gavana apongeza mafanikio ya miaka 10 CRDB Burundi

**BUNJUMBURA,** BURUNDI

BENKI Kuu ya Burundi (BRB) imeipongeza Benki ya CRDB Burundi kwa mafanikio makubwa iliyopata katika kipindi cha miaka 10 ya kuwapo kwake nchini humo.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Naibu Gavana wa Kwanza wa Benki Kuu ya Burundi kwa niaba ya Gavana katika mkutano na ujumbe wa CRDB uliooongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Abdulmajid Nsekela, aliyefuatana na wajumbe wa bodi ya kampuni mama ya Benki ya CRDB pamoja na kampuni tanzu ya Benki ya CRDB Burundi.

Ujumbe huo ulitembelea Benki Kuu ya Burundi kutoa shukrani ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 10 ya utoaji huduma za kibenki ya kampuni tanzu ya Benki ya CRDB Burundi.

Akizungumza katika mkutano, Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Burundi, Desire Musharitse alisema Benki Kuu ya nchi hiyo inafurahia kuwapo kwa Benki ya CRDB nchini Burundi kwa kuwa imekuwa sehemu ya uwezeshaji wa miradi mingi ya kiuchumi kwa nchi lakini pia imechangia uwezeshaji wa wafanyabiashara.

"Tulipata matatizo yaliyosababisha changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha za kigeni mwaka 2015 lakini tulipata msaada mkubwa sana kutoka Benki ya CRDB na hakika hilo limedhihirisha ule usemi wa rafiki wa kweli hujulikana wakati wa shida," alisema Musharitse.

Tangu ilipoingia katika soko la Burundi mwaka 2012, Benki ya CRDB imekuwa ikifanya vyema sokoni na katika kipindi cha miaka 10 imeweza kushika nafasi ya tatu kati ya benki 13 zinazotoa huduma za kibenki Burundi.Katika kipindi hiko, CRDB imefungua matawi manne huku tawi la tano likitarajiwa kufunguliwa mapema mwakani.

"Kutokana na kufanya vizuri kwa Benki ya CRDB Burundi tunatamani kuona ikifungua matawi mengi zaidi nje ya Bujumbura lakini pia kufanikisha upatikanaji wa mikopo kwa njia za kidigitali kama ambavyo wamekuwa wakitoa huduma nyingine za kidigitali," alisema Musharitse.

Nsekela aliishukuru Benki Kuu ya Burundi kwa ushirikiano mkubwa kwa Benki ya CRDB Burundi uliopelekea kampuni tanzu hiyo kupata mafanikio makubwa ndani ya kipindi kifupi cha miaka 10.

Sambamba na hilo, Nsekela aliishukuru serikali ya nchi hiyo chini ya Rais Evariste Ndayishimiye kwa kuipatia eneo Benki ya CRDB Burundi katika makao makuu mapya ya nchi ya Gitega ili kufanikisha ujenzi wa tawi jipya.

"Marais wetu wanatamani kuona ushirikiano wa sekta binafsi za Tanzania na Burundi lakini pia wamezungumza juu ya miradi ya kimkakati kati ya nchi hizi mbili ikiwamo mradi wa SGR (reli ya kisasa) na sisi tuko tayari kuisadia kampuni yetu tanzu kushiriki katika mradi hu kwa upande wa Burundi kama ambavyo tumeshiriki kwa upande wa Tanzania," alisema.

Nsekela alisema Benki ya CRDB inatarajia kuingia Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) hivi karibuni, jambo ambalo litachangia kukuza biashara kati ya Burundi na DRC lakini pia ushirikiano wa biashara kati ya nchi hizo na Tanzania ambazo kwa pamoja ni sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Azma yetu katika masoko tunayohudumia siyo tu kutoa huduma bora, bali pia kutoa mchango katika uchumi na kubadilisha maisha ya watu tunaowahudumia, hivyo tunaahidi kuendelea kufanya kazi kwa ushirikiano na Benki Kuu ya Burundi ili kuleta mageuzi ya kiuchumi Burundi," alisema Nsekela. Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB Burundi, Hosea Kashimba alitoa shukrani za bodi kwa Benki Kuu ya Burundi kwa ushirikiano mkubwa uliochangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya Benki ya CRDB Burundi katika kipindi cha miaka 10 tangu kuingia katika soko la Burundi.

"Tunaona mwelekeo mzuri wa nchi na tunaamini ndani ya kipindi kifupi kijacho, tutaweza kuwa benki kiongozi hapa Burundi, hivyo basi tunaomba ushirikiano huu uendelee kwani hatuwezi kufikia malengo yetu bila ushirikiano wenu," alisema Kashimba ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Maadhimisho ya miaka 10 ya Benki ya CRDB Burundi yameambatana na shughuli mbalimbali zenye lengo la kushukuru jamii ya watu wa Burundi kuiwezesha benki hiyo kufanya vizuri sokoni.



Mwenyekiti wa Bodi ya kampuni mama ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (wa tatu kulia), akikabidhi tuzo maalumu ya shukrani ya maadhimisho ya miaka 10 ya kampuni tanzu ya Benki ya CRDB Burundi kwa Naibu Gavana wa kwanza wa Benki Kuu ya Burundi, Desire Musharitse (katikati) pamoja na Naibu Gavana wa pili, Marie Goreth Ndayishimiye, jijini Bujumbura nchini Burundi jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya CRDB Burundi, Hosea Kashimba (wa pili kulia), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Abdulmajid Nsekela (wa pili kushoto), Mkurugenzi wa Benki hiyo, Burundi, Fredrick Siwale (kushoto) na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Burundi, Menard Bucumi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCRA yapongezwa kuwezesha huduma kifedha

**Na Frank Monyo**

WANANCHI waliotembelea maonyesho ya huduma za kifedha yanayoendelea jijini Mwanza, wameipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kuleta mapinduzi katika huduma za kifedha na kuwezesha huduma hizo kupatikana kwa urahisi bila usumbufu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti walipotembelea banda la TCRA katika maonyesho hayo jana, Frederick Masanja alisema kabla ya huduma za mawasiliano kuanzishwa upatikanaji wa huduma za kifedha ulikuwa na changamoto ikiwemo kupoteza muda, nauli kwenda kuzifuata na kutopatikana kwa taarifa za kifedha kwa haraka tofauti na sasa ambapo kila kitu kiko kiganjani.

Alisema wakulima sasa wanapata huduma za kibenki wakiwa huko mashambani jambo ambalo ni tofauti na zamani walikuwa wakizifuata mijini huduma hizo.

Mwalimu Costa Mabula alisema zamani suala la mishahara kwao ilikuwa changamoto tofauti na sasa kwa kuwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya kisasa imerahisisha.

Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa TCRA, Mabel Masasi, alisema mamlaka inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana huduma za mawasiliano nchini. Alisema katika wiki ya fedha, TCRA ni mdau mkubwa kwa kuwa hivi sasa huduma za kifedha zinafanywa kwa kutumia simu za mkononi na hilo limekuwa na ufanisi kwa asilimia 100.

Masasi alisema wakati mteja akipata changamoto za huduma mawasiliano milango iko wazi ikihusisha na watoa huduma za mawasiliano.

Katika uwezeshaji sekta ya fedha TCRA inatoa leseni kwa makampuni yanayowezeka katika huduma za miundombinu ya mtandao ambapo hadi sasa yapo 20, makampuni ya huduma tumizi ambayo yapo 87na leseni za namba maalum za huduma. Huduma za kifedha zimepewa namba zinazoanzia 150. Wiki ya huduma za kifedha inaadhinishwa jijini Mwanza katika viwanja vya rock city ambapo kaulimbiu ya mwaka huu ni elimu ya fedha kwa maendeleo ya watu.

# Hemed ataka kuanzisha mfuko wasiojiweza

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amekiagiza Chuo Kikuu Mzumbe, kuangalia uwezekano wa kuanzisha mfuko wa ufadhili kwa Watanzania wanaoshindwa kusoma elimu ya juu kutokana na ukosefu wa fedha.

Hemed alitoa agizo hilo juzi wakati wa Mkutano Mkuu wa 22 wa Baraza la Msajili la Chuo Kikuu Mzumbe uliofanyika mjini hapo.

Kiongozi huyo ambaye ni mmoja wa waliosoma chuoni humo miaka ya nyuma, alisema kuanzishwa kwa mfuko huo kutasadifu kauli mbiu ya chuo hicho inayoeleza "Tujifunze kwa maendeleo ya watu".

"Wapo Watanzania wenzetu walio na uwezo kimasomo lakini kutokana na ukosefu wa fedha wanakosa nafasi hii muhimu hivyo mfuko utakuwa mkombozi kwao kuweza kufikia malengo yao," alisema Makamu wa Pili wa Rais.

Akizungumzia Chuo Kikuu Mzumbe, alisema ni kati ya vyuo vikuu nchini ambacho kimefanya vizuri kwa kutoa viongozi wa ngazi ya juu, akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan na wengine waliopo serikalini na sekta binafsi.

"Hata mimi najivunia kuwa zao la Chuo Kikuu Mzumbe kwani nilisoma shahada ya umahiri wa biashara na uchumi ambayo imenisaidia katika kazi yangu ya mwanzo ya Ofisa Mnadhimu wa Wizara ya Biashara nikiwa Pemba," alisema Makamu wa pili wa Rais.

Alisema akiwa Pemba kama ofisa biashara kwa kushirikiana na watumishi wenzake walifanikiwa kupandisha bei ya zao muhimu la uchumi visiwani humo kutoka Sh. 3,000 hadi Sh. 14,000 ya sasa kwa kilo kutokana na matunda ya Chuo Kikuu Mzumbe.

Hata hivyo, Makamu wa pili wa Rais aliwataka wahadhiri wa chuo hicho kuongeza juhudi katika kuongeza machapisho na tafiti mbalimbali ambazo zitaweza kusaidia Taifa katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na teknolojia.

Hemed alishauri uongozi wa chuo hicho kuangalia namna ya kuanzisha mashirikiano na Vyuo vya Zanzibar, ili kutanua wigo wa kuchagua programu za kujifunza na kusogeza fursa ya elimu kwa Wazanzibari.

Aidha, Makamu wa Pili wa Rais aliutaka uongozi wa Chuo hicho kuwa sehemu ya kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi katika kutimiza malengo ya kujenga na kuendeleza Tanzania.

Naye Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Prof. William Mwegoha, alisema mkutano huo hufanyika kila mwaka kwa lengo la kuwakutanisha na kujadili namna ya kuboresha na kukuza chuo hicho pamoja na kuwapongeza wanafunzi na wafanyakazi waliofanya vizuri.

Alisema chuo hicho kinaendeleza kujenga majengo mengine ambayo ni ya utawala, eneo la viwanja vya michezo pamoja na ukumbi wa mahafali.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Bara, Christina Mndeme ambaye ni miongoni mwa wahitimu wa chuo hicho, alitaka wanachuo hicho kujenga uzalendo ikiwamo kujitolea ili kusaidia kutumia elimu waliyoipata kutoa fadhila kwa kukisaidia chuo hicho na jamii.




Meneja uendeshaji wa Kampuni ya Tamgo, Henrik Nielsen, akifafanua jambo kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana wakati wa uzinduzi wa kampuni hiyo, hapa nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yazindua teknolojia ya kisasa ya kutibu maji chumvi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tamgo ambayo inajishughulisha na utengenezaji wa mitambo ya kutibu maji, umeme wa nishati ya jua na majenereta imezinduliwa rasmi nchini.

Uzinduzi huo ulifanyika Dar es Salaam hivi karibuni huku Meneja Uendeshaji wa Tamgo, Henrik Nielsen, akibainisha kuwa lengo lao ni kutoa huduma bora za vifaa vya kisasa hapa vyenye ubora wa hali ya juu.

Nielsen alisema wamejipanga katika soko la ushindani la hapa nchini, lakini vifaa bora ndiyo nguzo yao kubwa ya kushinda soko.

Alisema wanajivunia uzoefu katika sekta ya utengenezaji mitambo ya kisasa na wamefanya hivyo katika nchi nyingi na kuamua kupanua biashara kwa kuwekeza Tanzania. "Tunajua kuna ushindani mkubwa katika soko, lakini nguzo yetu kubwa ni kutoa huduma bora na za kisasa zaidi kama tulivyofanya katika nchi nyingi ambazo tumekuwa na biashara ya aina hii," alisema Nielsen.

Meneja wa kampuni hiyo, Tarek Mostafa, alisema wanajivunia uwekezaji mkubwa wa teknolojia ya tiba za maji, majenereta na umeme wa nishati ya jua katika maeneo yote wanayofanya biashara duniani. Wakati huo huo, Mkuu wa Idara ya Maji ya kampuni hiyo, Damian Massenge, alisema wametengeneza mtambo wa kuchakata maji ya chumvi ujulikanao kwa jina Reverse Asmosis (RO) na kuwa maji matamu.

Massenge alisema teknolojia hiyo inapatikana kote nchini kwa muda mfupi na gharama nafuu akifafanua kwamba itasaidia kuondoa chumvi kwenye maji katika maeneo ambayo yana maji chumvi. Alisema wamejifunza kutoka kwenye nchi za Ujerumani, Italia na Ufaransa na kufafanua kuwa upatikanaji wa maji ya chumvi ni rahisi hasa kipindi hiki cha ukame, hivyo wanapoyachakata na kuondoa chumvi itapunguza makali ya mgao kipindi hiki.

"Mitambo hiyo ya kisasa inazalishwa hapa hapa nchini na kuwarahisisha upatikanaji wake, hivyo kupunguza gharama tofauti na miaka ya nyuma ilikuwa lazima ikatengenezwe nje ya nchi na kuanza kuisafirisha ambapo gharama iliongezeka zaidi," alisema.

# Chuo Kodi chajivunia kuongezeka wahitimu

**Na Elizabeth Zaya**

IDADI ya wanafunzi watakaohitimu katika mahafali ya 15 ya Chuo cha Kodi (ITA) mwaka huu, imeongezeka hadi kufikia 489 kutoka 387 mwaka jana.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam juzi , Mkuu wa chuo hicho, Prof. Isaya Jairo, alisema ongezeko hilo ni sawa na asilimia 25.1.

"Ongezeko hili linatokana na jitihada za chuo kuhakikisha viwango vya mafunzo yanayotolewa vinakidhi matakwa ya mahitaji ya taaluma na kodi," alisema. Prof. Jairo alisema katika mahafali hayo yatakayofanyika kesho, wahitimu wanatarajiwa kutunukiwa vyeti vya stashahada, shahada na shahada ya uzamili katika kozi mbalimbali zinazotolewa na chuo hicho. Alisema kati ya wahitimu hao 489, wahitimu 194 watatunukiwa cheti cha uwakala wa forodha cha Afrika Mashariki, 36 watatunukiwa cheti cha usimamizi wa forodha na kodi, 58 stashahada ya usimamizi wa forodha na kodi, 161, shahada ya usimamizi wa forodha na kodi na 40 stashahada ya uzamili katika kodi.

Alisema Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba ndiye anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mahafali hayo.

Alisema katika mahafali hayo, chuo kinatarajia kutoa zawadi mbalimbali kwa wahitimu na wanafunzi wanaoendelea na masomo, waliofanya vizuri zaidi katika mwaka wa masomo 2021/2022.

"Na katika mahafali haya, kwa kuzingatia ushirikiano uliopo, tumewaalika baadhi ya wakuu wa mamlaka za mapato mbalimbali kutoka nje ya Tanzania na ambao mpaka sasa wamethibitisha kushiriki ni pamoja na mamlaka za mapato Kenya, Ghana, Eswatini na Malawi," alisema Prof. Jairo.



## Samia aagiza kutatuliwa tatizo la maji Monduli

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MATESO ya wanawake na watoto, kutafuta maji usiku wa manane kwenye makorongo na mabonde Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha, kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, yamemuumiza Rais Samia Suluhu Hassan, na kuagiza tatizo hilo litatuliwe ndani ya miezi mitatu kuanzia sasa.

Kutokana na tatizo hilo, Rais Samia amemwagiza Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, kuhakikisha mradi wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 1.7 unaotekelezwa wilayani humo kukamilika ili wananchi wapate huduma hiyo.

Rais Samia alitoa agizo hilo jana, aliposimama kuzungumza na wananchi wa Monduli katika eneo la Makuyuni, wakati akitokea mkoani Manyara, ambako alifanya ziara ya siku mbili ya kikazi.

"Waziri wa Maji (Aweso), nakuagiza huu mradi wa maji wa Mbuyuni/Naiti hadi Losimingori, ambao utawanufaisha wananchi wa Wilaya ya Monduli wanaokabiliwa na tatizo la maji kwa muda mrefu ukamilike na sitaki visingizio.

"Ndugu zangu wananchi wa Monduli, serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuchukua maji kutoka kwenye mradi mkubwa wa maji unaotekelezwa katika Jiji la Arusha na kuuleta Monduli,"alisema na kuongeza:

"Kingine, Mheshimiwa Waziri, ule mradi wa visima vitatu vilivyochimbwa katika Kitongoji cha Zaburi, visima viwili na kimoja Kitongoji cha Meloroni, ambavyo vina uwezo wa kutoa maji lita za ujazo milioni 1.1, upatiwe fedha mara moja ili ukamilike Machi mwakani (2023)."

Mradi huo mkubwa unaogharimu Sh. bilioni 520, umeanzia eneo la Kikuletwa, Wilaya ya Hai (Kilimanjaro) na kwenda hadi Jiji la Arusha, unatekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha, kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB).

Naye Mbunge wa Monduli, Fredrick Lowasa, alimweleza Rais Samia kwamba, wananchi wake wanakabiliwa na tatizo kubwa la maji kutokana na kutokana na kutokuwapo vyanzo vya maji.

Aidha, akimwomba kutumia mamlaka aliyonayo kuagiza mradi wa maji wa Kikuletwa/ Arusha uwanufaishe pia na wananchi wa Monduli.

Baada ya maelekezo hayo ya Rais Samia, Waziri wa Maji, Aweso, alisema katika maeneo yanayoitesa wizara yake kutoa huduma za maji ni pamoja na wilaya ya Monduli, ambako hakuna chanzo cha maji.

# Rais Samia aahidi tatizo la umeme kukoma 2025

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKATI maumivu ya mgawo wa umeme na maji ukiendelea kulitikisa taifa kutokana na ukame uliosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, Rais Samia Suluhu Hassan, amewapa matumaini Watanzania, akisema matatizo hayo yatakoma rasmi ifikapo mwaka 2024.

Akizungumza juzi na wananchi wa Mbauda jijini Arusha, alisema maendeleo ni hatua, hivyo anaamini ifikapo mwaka 2024 kuelekea 2025, matatizo hayo yatakuwa historia, kwa kuwa serikali imejipanga vyema kumaliza matatizo ya umeme na maji.

"Lakini ifikapo mwaka huo, miji mingi itakuwa inawaka umeme na kupata maji kwa asilimia 100 na baadhi kwa asilimia 95. Katika hili kwa sasa serikali imeweka nguvu zaidi kwenye ununuzi wa mitambo ya kisasa ya kuchimba visima, yenye uwezo wa kutambua eneo lenye maji na lisilo na maji, na tayari nimeshagawa maeneo mbalimbali ya nchi yetu. "Lakini pamoja na uwezo wake wa kutambua maeneo yenye maji pia ina uwezo wa kuokoa gharama ambazo tulikuwa tukiingia zamani za kuwalipa makandarasi hata kama walisema kuna maji na wakakosa maji," alisema.

Wiki iliyopita, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande, alikaririwa kueleza mikakati iliyoko katika kukabili mgawo na kueleza hali ngumu iliyoko sasa imesababishwa na ukame pamoja na kuharibika mitambo.

Aidha, alisema mafundi wapo kazini kufanya ukarabati na ifikapo Januari mwakani hali itatengemaa.

Kabla ya Rais Samia kutoa matumaini hayo, Mbunge wa Arusha, Mrisho Gambo, alimwomba Rais Samia, kuliagiza TANESCO, kutoa za taarifa kwa umma za mgawo wa umeme, ambao umekuwa kero kubwa kwa wafanyabiashara wa jijini humo pamoja na maeneo ya kutolea huduma hasa hospitalini.

"Mheshimiwa Rais, wananchi wa Arusha Mjini, wanakabiliwa na tatizo kubwa la kukatika kwa umeme mara kwa mara, bila hata kupewa taarifa. Hili suala linasababisha usumbufu kwa wananchi wanaotumia umeme katika uzalishaji, ikiwamo wafanyabiashara, maeneo ya viwandani na hata hospitali zetu," alisema na kuongeza: "Kwa mamlaka yako tunaomba uwaagize TANESCO kuja na utaratibu wa kutoa taarifa za mgawo wa umeme pamoja na ratiba kila siku ya maeneo yatakayoathirika."



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (kushoto), akiwasikiliza wadau wa maendeleo, walipokutana katika ukaguzi wa jengo la ununuzi wa madini ya Tanzanite, Mji mdogo wa Mirerani juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Serikali yaridhia mfumo wa SCT kutumika vituo vya forodha

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

SERIKALI imeruhusu matumizi ya mfumo wa himaya moja ya forodha (SCT), kwenye vituo vya forodha nchini vilivyoko chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ili kumaliza urasimu wa ucheleweshaji mizigo.

Mfumo huo ni moja ya takwa la kisera la utangamano wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), ambao pamoja na mambo mengine linaainisha utaratibu wa mzunguko huru wa biashara, usimamizi wa mapato na mfumo wa kisheria.

Jana Ofisa Forodha kutoka Kitengo cha Himaya Moja ya Forodha wa TRA, Makao Makuu, Tirassy Kulwa, akizungumza na mawakala wa forodha katika mpaka wa Holili, alisema licha ya mfumo huo kupunguza tatizo la ukwepaji kodi, nchi zote wanachama wa EAC, zinachukuliwa kama himaya moja ya forodha.

Alisema maana yake ni kwamba kuanzia sasa, tamko moja la forodha, linafanywa katika nchi ambayo bidhaa zimepokelewa.

"Himaya moja ya forodha ni hatua ambayo itazifikisha nchi wanachama wa EAC kwenye umoja wa forodha, ambao kutokana na kuondoa ushuru na kanuni au kupunguza vikwazo vya forodha kwenye bidhaa zinazopita katika mipaka ya nchi wanachama, unaruhusu kufanya mzunguko huru wa bidhaa.

"Kimsingi tamko moja la forodha, linaondoa mfumo wa zamani uliohitaji matamko mengi ya forodha. Kwa mfano bidhaa kwenda Rwanda, Burundi au Uganda, zilikuwa zikihitaji mawakala wengi wa forodha.

"Kwa utaratibu huu wa himaya moja ya forodha, mteja anapaswa kukamilisha malipo kwanza, ndipo atoe mzigo wake na kwa utaratibu huu unaihakikishia serikali kupata mapato yake kwa wakati,"alisema na kuongeza:

"Pia utaratibu huu utadhibiti mianya ya ukwepaji kodi, yaani katika utaratibu huu 'documents' (nyaraka) inayotumika ni moja tu, na inamsaidia pia mteja kupunguza gharama," alisema.

Aidha, TRA imewashauri wafanyabiashara kuanza kutumia mfumo huo wa himaya moja ya forodha kutokana na manufaa makubwa yaliyoko.

Kwa bidhaa zinazopitia nchi moja kuelekea katika nchi nyingine, nchi wanachama zimekubaliana kuwa nchi husika bidhaa zinapokwenda, itakusanya mapato yake na kuifahamisha mamlaka ya forodha mizigo ilipoingilia katika EAC, kwa ajili ya kuruhusu bidhaa kuondoshwa.

Chini ya himaya ya moja, nchi wanachama zitatumia mfumo maalum wa ufuatiliaji kielektroniki (electronic cargo tracking system), ili kuhakikisha mizigo inafika salama katika nchi iliyokusudiwa katika jumuiya.

Baadhi ya mawakala wa forodha walioko katika Kituo cha Forodha Holili, wameeleza kuwa utaratibu huo utawawezesha kutoa mizigo kwa haraka na kuondokana na tatizo la urasimu na ucheleweshaji walioukuwa wakiupata.

Mmoja wa mawakala hao, Daniel Benard, alisema hatua hiyo itawawezesha kufanya kazi kwa waledi na kuondoa nalalamiko baina ya maofisa wa forodha na wafanyabiashara, pamoja na malalamiko kati ya mawakala na wafanyabisha, ambayo mengi yalichangiwa na uchekeweshaji wa mizigo.





# Mwenyekiti CCM aanza kwa kishindo

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SIKU tatu, baada ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdurahman, ameanza kutekeleza ahadi yake ya kutibu matatizo yanayokikabili, baada ya kutoa Sh. milioni 14 za kulipa stahiki za makatibu kata na matawi 245.

Rajab, alisema fedha hizo ni malipo ya posho ya miezi sita, watakayolipwa viongozi hao kila mwishoni mwezi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kukijenga chama hicho.

"Nimeamua kutoa fedha hizi, kwa sababu mara nyingine zimekuwa zikichelewa, jambo ambalo limekuwa linapunguza kasi ya uendeshaji wa chama chetu. Mimi nililiona tatizo hili na kuahidi kuanza nalo pamoja na kuimarisha vyanzo mbalimbali vya mapato ndani ya chama kama nitachaguliwa. Sasa baada ya kuchaguliwa nimeamua tumalizane kabisa.

"Katibu wa CCM Mkoa, nikuombe nimepiga hesabu, tuna kata 245 kwa mkoa mzima na kila kata ukiipa shilingi 10,000, maana yake umetoa milioni mbili kwa mwezi. Naomba nikukabidhi pesa ya miezi sita ili kuanzia mwezi huu wa Novemba."

Mwenyekiti huyo, ambaye aliwahi pia kuwa Mwekiti wa CCM, Wilaya ya Pangani, alichaguliwa juzi kwa kupata ushindi wa kishindo wa kura 1,340, akichukua nafasi ya mtangulizi wake, Hendry Shekifu.

Aliwabwaga washindani wake, Derrick Kazoba, aliyepata kura 29 na Mathias Mkingwa, aliyeambulia kura tisa katika mkutano huo wa uchaguzi.

Katika uchaguzi huo, pia mfanyabiashara wa mabasi ya abiria yaendayo mikoani anayemilikiwa Kampuni ya RATCO, Mohamed Salim, alishinda nafasi ya Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kupitia Mkoa wa Tanga.

Salim aliibuka kidedea baada ya kuwashinda wagombea wenzake kwa kupata kura 774 na kufanikiwa kutetea nafasi hiyo aliyokuwa akiishikilia, huku Omar Sempoli na Hassan Bomboko.

# Samia aonya wanasiasa mbio 2025

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WANASIASA wanaowachochea wananchi, wakihamasisha kuvamia ardhi iliyotengwa kwa ajili ya shughuli za umma 'wamemchefua' Rais Samia Suluhu Hassan, akionya wanaofanya siasa nyepesi ili kujitafutia mtaji wa kura, kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kuacha mara moja.

Rais Samia alieleza kukerwa na tabia hiyo juzi, alipokuwa akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Manyara katika mkutano wa hadhara uliofanyika uwanja wa Kwaraa Babati Mjini. Alikuwa mkoani Manyara kwa ziara ya kikazi ya siku mbili.

"Kuna tabia kwa wanasiasa, mnakaa kimya maeneo yanapovamiwa lakini baadaye mnasimama na kuwatetea ili kupata kura wakati wa uchaguzi. Tabia hiyo si nzuri muache. Unajua wamevamia na wameharibu mipango ya matumizi bora ya ardhi, halafu unasimama kuwatetea ili upate kura, kwangu hiyo hapana!" Alisisitiza.

Kutokana na tabia hiyo, Rais Samia alisema migogoro hiyo inapoteza muda mwingi na kuchelewesha maendeleo, akiwataka wenye malengo ya kisiasa kuelekea 2025, wasimame na serikali katika kupanga matumizi bora ya ardhi.

"Eneo ambalo wananchi wangelitumia kwa maendeleo, halitumiki kwa sababu lipo kwenye mgogoro hadi umalizike. Niombe sana wanasiasa tusaidiane kwenye jambo hili na tusichochee migogoro, kwa sababu wakati wanavamia wanakuwapo wanawaona ila hawawazuii, wanawaacha migogoro inaendelea ili walinde kura zao.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, akizungumza katika mkutano huo, alimweleza Rais Samia juu ya mgogoro wa ardhi unaochochewa na wanasiasa, ambao unahusu mashamba mawili ya Amir Estates na Manyara Estates. Alisema Shamba la Amir Estates, lilifutwa kwa mamlaka ya Rais.

"Mheshimiwa Rais, mwekezaji wa shamba hilo alitakiwa kulipwa fidia shilingi milioni 700 ila mpaka sasa hajalipwa. Kimsingi, mwekezaji alikuwa amekubali kuondoka ila alitaka apewe ekari 145, halafu pia bado anatakiwa kupewa fidia.

"Tukasema serikali haiwezi kuingia hasara ya kulipa shilingi milioni 700 kwa ajili ya eneo lililovamiwa na mtu, badala yake yeye ndio anatakiwa alipe fidia. Hata hivyo, mpaka sasa hakuna fungu serikalini, ambalo limetengwa ili kuwalipia watu wanaovamia," alisema Dk. Mabula.

Kuhusu Shamba la Dudumera, ambalo Mbunge wa Babati Vijijini, Daniel Sillo, alimweleza Rais Samia kwamba haliendelezwi, Waziri Mabula, alisema wizara yake ina shauri ni vizuri.

Halmashauri husika ifanye uchunguzi kujiridhisha kama mwekezaji haliendelezi, ndipo wafuate utaratibu wa kisheria wa kuomba Rais Samia afute hati, lakini siyo kuacha wananchi walivamie.

Awali, Mbunge wa Babati Vijijini, Daniel Sillo, alimweleza Rais Samia kwamba katika wilaya hiyo, kuna migogoro ya ardhi katika Kata za Kiru, Magala na jirani na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire. Alisema upo mgogoro wa Shamba la Amir Estates na Shamba la Manyara Estates, akiomba atatue migogoro hiyo.



Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Kilimanjaro, Masawa Masatu (kushoto), akikabidhi misaada mbalimbali ya kibinadamu ikiwamo vyakula na sabuni kwa mmoja wa wazee wasiokuwa na makazi wanaolelewa katika makao ya wazee katika kata ya Njoro, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya shukrani kwa walipakodi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Mbunge aomba wananchi nyongeza bei ya maji

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MBUNGE wa Babati Mjini, Pauline Gekul, amelazimika kuwaomba wakazi wa mji huo, akiwa mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan, kukubali mapendekezo ya kupandishwa kwa bei ya matumizi ya maji ili kukabiliana na gharama kubwa za uendeshaji wa miradi ya maji.

Gekul aliwasihi wakazi hao kutofikiria kugomea kuchangia gharama hizo ili kupata huduma ya maji kwa wakati wote kwa kuwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mji wa Babati (BABATI WSSA) inahitaji kufanya maboresho makubwa kwenye miundombinu yake ya maji ili kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo.

Alilazimika kufanya hivyo juzi, kabla ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuzungumza na wananchi wa Babati katika mkutano wa hadhara uliofanyika uwanja wa Kwaraa.

"Aidha, niwadokeze tu kwamba serikali inafikiria kuleta huduma ya kulipia maji kabla ya kutumia (prepaid meter) ila haina uwezo wa kupeleka huduma hiyo kila mahali. Ninachokiomba kwenu wananchi wangu mridhie hilo na kuendelea kulipia huduma ya maji," alisema.

Baada ya kauli hiyo, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alipanda jukwaani na kutoa ufafanuzi kuhusu mapendekezo yaliyofanyika akieleza kuwa utoaji wa huduma za maji si biashara, bali ni huduma.

"Hatufanyi biashara ila ni lazima maboresho ya miundombinu nayo yafanyike, na ndio maana serikali imeamua kutoa shilingi bilioni 12 ili wananchi wa Babati wapate maji kutoka kwenye Mradi wa Maji wa Dareda/Singu.

"Niweke wazi kwamba, siyo maeneo yote yatapata maji kwa mara moja, kwa kuwa hivi sasa kuna shida ya vyanzo vya maji, hivyo tutachimba visima vya maji nchi nzima ili watu wapate huduma kwa asilimia 100," alisema.

Mwanzoni mwa mwezi huu, Mkurugenzi Mtendaji wa Babati- WSSA, Iddy Msuya, alitisha mkutano wa wadau wa maji kujadili mapendekezo ya kupanda kwa bei ya matumizi ya maji kutokana na ongezeko la gharama za uendeshaji wa huduma za maji.

Baada ya kuwasilishwa pendekezo hilo, Kaimu Mkurugenzi wa EWURA, Walter Geofrey, alisema wao wanahitaji wananchi wapate maji kwa ubora unaotakiwa na kwamba bei hiyo inayopendekezwa itasaidia huduma kuwa endelevu.

Ofisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Maji na Nishati (EWURA CCC), Neema Nnko, yeye alishauri kuongezwa idadi ya watumiaji wa maji na kupunguzwa kwa kiwango cha maji yanayopotea katika miradi ya mamlaka hiyo.



Ukurasa 14

**Njia panda dai la fidia ya miaka 26 wachimbaji wadogo 362 North Mara**



Ukurasa 18

Ugeni wa Taliban: Hali mbaya watu wengi wauza figo



**Tembo Nickel iliyoonyesha nuru ya mapinduzi katika elimu Ngara**

Ukurasa 19



# Matokeo ya Sensa; yamekufunza na kukuandaa kwa mambo mangapi?

**Na Pankras Luoga**

"Wazazi wenye familia yenye jumla ya watu watatu ikiongezeka na kuwa na jumla ya watu sita basi wazazi hao lazima waongeze juhudi katika kufanya kazi ili kuimudu familia ambayo kwa sasa imekuwa kubwa zaidi," ni ujumbe unaohusu zaidi jamii.

Serikali ilizindua Sensa ya Watu na Makazi mnamo Agosti 23 mwaka huu na kuendelea kwa siku saba, ikihusisha ukusanyaji taarifa za watu wa jinsia zote, wenye ulemavu na wasio na ulemavu na mali kama majengo.

Hadi sasa nchini kuna matokeo ya awali yamesharipotiwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan, mnamo Oktoba 31, wastani wa mwezi mmoja. Kuna watu 61,741,120, kutoka ile ya mwaka 2012 ambayo ilikuwa ni watu 44,928,923.

Hivi sasa kwenye ujumbe wa simu inasambazwa taarifa zinazotambulishwa kwa neno 'Sensa 2022, ikifafanua " idadi ya watu nchini imeongezeka kutoka watu 44,928,923 mwaka 2012 hadi 61,741,120. Inatarajiwa kuongezeka mara mbili 2044."



Mtumishi wa Sensa akiwajibika. **PICHA: MTANDAO**

Nini tafsiri yake? Ni kwamba kuna idadi kubwa sana ya wakazi ikilinganishwa na uwezo wa nchi katika kutoa huduma muhimu za elimu, afya, maji na nyinginezo, Rais akiitafsiri ni mzigo mkubwa kwa taifa.

Muhimu kwa umma, ni kwamba takwimu hizo za sensa zinatoa ujumbe kuwa idadi ya watu nchini inatarajiwa kuongezeka zaidi, ikihusisha pia idadi kubwa ya watoto ambao ni wahitaji wa huduma muhimu.

Pia, kwa wazazi ni ishara sasa kwamba, ni lazima wafanye kazi zaidi, kwani mahitaji ya familia kama vile chakula na mengine yanazidi kuongezeka.

Vilevile, kuna ishara ya takwimu sahihi, mamlaka za kiserikali kufahamu vyema wanachotakiwa kuhudumia, kama vile elimu, maji, umeme na afya.

**NINI KIFANYIKE?**

Huo ukiwa ni ujumbe mkubwa kwa kila Mtanzania afanye kazi kwa bidii, aongeze juhudi katika anachokifanya, kuanzia mwanafunzi ajitahidi darasani, jamii ikisubiri mafanikio yake; mfanyakazi aliyepo shambani alime zaidi kukidhi mahitaji ya watu wake, mlo umeongezeka, vivyo hivyo watoa huduma mbalimbali.

Pia, inatajwa kuwapo faida ya idadi kubwa ya watu, kwamba kunaongeza bidii ya kazi nchini, kukiwepo nguvukazi ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji mali na kutoa huduma kitaifa.

Jingine, ni hali inayoipa taifa fursa ya kutumia vilivyo ukubwa wa soko la watu kufaidisha huduma ya rasilimali kwa wahitaji wa ndani au maarufu 'soko la ndani'.

Kwa ujumla bado kuna ujumbe mzito unaotokana na majibu ya awali ya sensa nchini, ukiitaka jamii kwa kila namna na nafasi yake, kujiandaa kuhimili matokeo yake na mwelekeo jamii inakoenda na huduma zitazoakisi ongezeko hilo la watu nchini.

Ni msukumo sahihi, kwa kila mwananchi ahamasike kwa kushiriki na kufanya kazi kwa bidii, kuwezesha idadi hiyo ya watu kupata bidhaa na huduma kadiri ya mahitaji yao.

***Mwandishi wa Makala hii ni Mhadhiri Msaidizi katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Tiba Muhimbili (MUHAS) na anapatikana kwa simu: + 255 757645746.***

FEDHA

# Njia panda dai la fidia ya miaka 26 wachimbaji wadogo 362 North Mara

## • Mbunge Waitara: Huu mtihani jamani!

**Na Anthony Gervas,** aliyekuwa Tarime

WALIOKUWA wachimbaji wadogo wa dhahabu eneo la Nyabigena wilayani Tarime mkoani Mara, sasa wanadai fidia kutoka kwa kampuni ya Mgodi wa Barrick Gold Mine Ltd (North Mara).

Ni madai waliyodumu nayo takribani miaka 26 hadi sasa tangu mwaka 1996 bila ya mafanikio, lakini wanaendelea kupaza sauti zao kwa serikali kupitia Wizara ya Madini.

Wachimbaji hao jumla 362, sasa wanadai kulipwa fidia ya uharibifu wa mali zao, zikiwemo nyumba za makazi kufukiwa mashimo waliyokuwa wakichimba, kuharibiwa vifusi vyao vya mawe ya dhahabu na upotevu wa vitendea kazi kama vile makarai.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wachimbaji hao, ambaye pia ni Diwani wa Viti Maalumu katika Kata ya Nyamwaga wilayani Tarime, Mariam Mkono, anasema yeye ni miongoni mwa waathirika wa kudai fidia hizo.

Mkono anaeleza kuwa mgogoro huo umedumu miaka mingi tangu uanze bila ya mafanikio na wamekuwa wakiwasilisha barua na vielelezo katika Ofisi ya Waziri wa Madini, bila ya kufikia ufumbuzi.

Anasema mwaka 1995 wakiwa wachimbaji wadogo wa dhahabu katika eneo hilo la Nyabigena, serikali za vijiji vitano ziliazimia kuwaondoa wachimbaji hao kwa makubaliano ya kulipwa fidia za mali zao na mwekezaji mkubwa aliyepewa leseni na serikali kwa ajili ya uchimbaji mkubwa.

Vijiji hivyo ni pamoja na Genkuru, Kewanja, Nyamwaga, Kerende na Nyangoto, ambavyo wachimbaji hao waliondolewa kwa nguvu ya serikali, kabla ya kulipwa fidia hizo.

### MENEJA MKUU BARRICK

Katika majibu yake, Meneja Mkuu wa kampuni ya Uchimbaji Dhahabu, Barrick Gold Mine Ltd, Apolinary Lyambiko, anafafanua kuwa anachokifahamu yeye ni kuwepo mikataba ya vijiji vitano, kwamba kila dhahabu itakayozalishwa vitapata asilimia moja.

Pia, mwaka 2018 katika vijiji vyote vitano kila kimoja kililipwa na mgodi huo dola 400,000 huku akisema kutokana na mgogoro huo, uchimbaji katika eneo hilo umesimama hauendeleii toka mwaka 2012.

### MAAGIZO YA SERIKALI

NAIBU Waziri wa Madini Dkt,Steven Kiruswa aliyetua wilayani Tarime hivi karibuni amewaagiza wachimbaji hao wanaodai kulipwa fidia ya uharibifu huo kuwasilisha kila mmoja vielelezo vya madai kwa ofisa madini mkoa wa Mara.

Kiruswa ametoa agizo hilo katika kikao cha pamoja na wachimbaji hao, kilichokuwa na lengo la kumaliza mgogoro huo na kubaini ukweli kuwa ni watu wangapi halali wanaotakiwa kulipwa na mlipaji kama kweli ni Kampuni ya Barrick( North Mara) au nani ?

Naibu Waziri Kiruswa anasema sababu ya kuwataka kila mdai apeleke vielelezo vyake ni kutokana na kwamba wanakosa ushahidi wa kutosha na hivyo kumpa yeye utata na wasiwasi wa kuamaliza mgogoro huo mapema iwezekanavyo.

Anafafanua kwamba kwanza wachimbaji wenyewe wanasalitiana na kugawanyika makundi matatu tofauti ya kudai fidia zao na hivyo wanakuwa hawana uthibitisho wa kutosha.

Mali hizo ni pamoja na kuvunjwa nyumba zao za makazi,kufukiwa mashimo yao,vifusi vyao vya mawe ya dhahabu, mchanga na kuvunjiwa nyumba za makazi yao.

"Nawaagiza kila mtu anayedai apeleke vielelezo vyake vya ushahidi ikiwemo mikataba ya madai ya kulipwa fidia ya uharibifu wa mali zake, kwa Ofisa Madini Mkoa wa Mara, ifikapo Novemba 30 atakayeshindwa kufanya, hivyo atapoteza haki zake zote,' anasema.

Vilevile anataka kila mmoja, abainishe alikuwa na mashimo mangapi, urefu wa kina kwenda chini, kiasi cha fidia anayodai ili kujua nani anayehusika kuwalipa sababu hawana vielelezo kamili na mikataba ya moja kwa moja kuwa "nani anawalipa, je ndiye mwekezaji aliyepo au la?"

"Kila mmoja anayedai kulipwa fidia apeleke vielelezo vyake vyote na mikataba,kwa Ofisa Madini wa Mkoa wa Mara, sababu pia nimeshtushwa na udanganyifu wa baadhi ya watu wamepachikwa majina hewa ndani ya hayo 362, zikiwemo nyumba za kutegesha ili walipwe fidia anasema.

### MBUNGE WAITARA

Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, analifafanua akitumia kauli 'anapenda ukweli,hataki kuaibishwa mbele ya viongozi' akifafanua, wanaodai fidia wamekosa ushahidi wa moja kwa moja wa kumpatia Naibu Waziri huyo, aweze kuumaliza mgogoro kwa kutoa maamuzi sahihi.

"Nimesikitika sana kutosema ukweli ndugu zangu,nilitegemea mmekuja hapa mkiwa mmejipanga kumbe tena hamna kila kitu nimetoka bungeni nikijua nakuja kuwasaidia mpate haki zenu, sasa nitawasaidiaje?" anahoji Waitara.

Anasema atakapoondoka Naibu Waziri wa Madini Tarime, yeye hana chochote cha kuwasaidia tena, ila kama kuna watu wameshafariki dunia wakiwa wanadai watalipwa watoto wao.

Mgodi North Mara ulioko wilayani Tarime, ukiwa kati ya migodi mikubwa nchini, ulikuwa na uwezo wa kuzalisha tani 8,000 za udongo wenye dhahabu kwa siku. Migodi mingine mikubwa nchini ya kuchimba dhahabu inajumuisha Tulawaka ya Biharamulo, Buzwagi (Kahama), Bulyanhulu na Geita, unaomilikiwa na mwekezaji tofauti.



Meneja Mkuu wa Kampuni ya Dhahabu Barrick Gold Mine, katika kikao na wachimbaji wadogo wanaodai fidia, eneo la Nyabigena. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**

> **"Nimesikitika sana kutosema ukweli ndugu zangu, nilitegemea mmekuja hapa mkiwa mmejipanga kumbe tena hamna kila kitu nimetoka bungeni nikijua nakuja kuwasaidia mpate haki zenu, sasa nitawasaidiaje?**



Naibu Waziri wa Madini, Steven Kiruswa, akielekeza jambo kwa wachimbaji wanaodai fidia zao.

BIASHARA

# EWURA wanapoamka na operesheni mpya vituo mafuta visambae vijijini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NI ukweli dhahiri nishati ya mafuta ya taa, petroli na dizeli bado ni kichocheo kikubwa kwa shughuli za kila siku hasa katika kuendesha mitambo mbalimbali yakiwamo magari.

Kutokana na kukua uchumi na wananchi kuhamasika kumiliki vyombo vya usafiri kwa maeneo ya vijijini kwa sasa, kumeonyesha umuhimu mkubwa wa kuwa na vituo vidogo vya mafuta sehemu nyingi vifikie umma uliko.

Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imekuwa ikifanya kila jitihada kuhakikisha nishati hiyo inapatikana kwa wingi ili kupunguza ulanguzi na pia wananchi kutokupata shida katika shughuli zao za kila siku.



Kituo cha mafuta kilichoko nje ya mji. **PICHA: MTANDAO**

### HODI VIJIJINI

Pamoja na mafuta kuuzwa katika vituo ambavyo vimejengwa kupitia vibali vya Ewura, hali ya upatikanaji wa nishati hiyo vijijini imekuwa ngumu kutokana na hali halisi ya miundombinu.

Zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania wanaishi vijijini na kutokana na umuhimu wa huduma hiyo, baadhi ya wafanyabiashara wadogo wanalazimika kununua mafuta kwenye vituo mijini na kuuza kwa rejareja kwenye madumu na chupa za maji kwa ujazo tofauti vijijini.

Mmoja wa wafanyabiashara hao maarufu kwa jina la Pati Mchaga wilayani Bahi, anasema wauzaji wamekuwa wakiuza kwa ujazo tofauti kwenye maduka ya bidhaa zingine, pia kwenye vibanda barabarani ili kurahisisha upatikanaji wake kwa maeneo ya vijijini.

Anasema, kutokana na hali hiyo ya kimiundombinu, wafanyabiashara wa mafuta wamekuwa wakisita kujenga vituo vya mafuta maeneo ya vijijini na matokeo yake kujikita zaidi katika sehemu za miji mikubwa, barabara kuu na miji midogo ambayo inakua kibiashara.

Petro Mahikwi, anashiriki hoja hiyo, akisema hali ya upatikanaji mafuta ni changamoto kwa kuwa hutegemea wafanyabiashara wenye maduka kijijini hapo kusafirisha bidhaa hiyo kutoka Dodoma Mjini.

"Hapa unaweza kuishiwa mafuta ya taa ukasubiri hadi jioni ndiyo upate maana wanaouza wanafuata Dodoma mjini na hadi kufika huku ni jioni kabisa, giza limeshaingia kwa kuwa magari yanayofanya safari za huku yanaondoka Dodoma Mjini saa nane mchana, kwa kweli ni changamoto," anaeleza.

Pia, anasema mafuta hayo yanatunzwa kwenye madumu kwenye makazi au sehemu za kawaida za biashara na pindi ukitokea moto, ni hatari kusababisha madhara kwa maisha ya watu na mali zao.




Msemaji wa EWURA, Titus Kaguo. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

### EWURA YAANIKA

Mkuu wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, anasema kuwapo mazingira hayo hatarishi, kunatokana na utunzaji na uhifadhi wa mafuta usiozingatia vigezo na masharti, ikibuni mbinu mbalimbali kuhakikisha nishati hiyo inapatikana vijijini tena kwa usalama.

Anasema, EWURA imeweka mazingira rafiki kuhakikisha huduma ya mafuta inapatikana nchi nzima ili kuimarisha huduma ya usafiri kwa vyombo vya moto vijijini.

Kaguo anafafanua: "Sisi Ewura kwa sasa tunahimiza sana ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini ili kuepuka wananchi kutumia mafuta kwenye vidumu, na tumetengeneza kanuni mahususi kwa hiyo tumerahisisha vigezo na masharti.

"Ndio maana ukiona vituo vya mjini huku gharama yake kujenga inaweza kuwa shilingi milioni 300 mpaka 500, sasa kwa mtanzania wa kawaida kule kijijini ambako kuna bodaboda na shughuli zingine vigezo tumevirahisisha zaidi.

"Mtu akiwa na shilingi milioni 40 mpaka 50, unaweza ukajenga kituo cha mafuta katika ngazi ya kijiji na wananchi wakapata mafuta bora na kwa gharama ambayo tunaipangia (bei elekezi),"anasema.

Anafafanua kuwa, kuwapo utaratibu wa vituo tembezi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma, kutokana na mahitaji yake

> "Mtu akiwa na shilingi milioni 40 mpaka 50, unaweza ukajenga kituo cha mafuta katika ngazi ya kijiji na wananchi wakapata mafuta bora na kwa gharama ambayo tunaipangia (bei elekezi).

kuongezeka kwa kushamiri kwa usafiri wa pikipiki maarufu kama bodaboda, ambazo ndio usafiri wa haraka kwa maeneo mengi.

"Nishati ya mafuta inatakiwa kuuzwa kwa utaratibu unaokubalika na kwa kuwa kujenga visima vikubwa ni gharama, njia hiyo ni bora na itakuwa ni rahisi kuwafikia wateja walio wengi," anasema Kaguo.

Anaeleza katika maeneo mengi nchini wafanyabiashara wadogo wamekuwa wakisafirisha na kuuza mafuta kwa njia ambazo si sahihi na zinazohatarisha usalama wa vyombo vya watumiaji na maisha yao wenyewe.

Kaguo, anafafanua kuwa watu wanatakiwa kufahamu kuwa kusafirisha na kuuza mafuta kwa njia zisizo rasmi, kwa kutumia madumu ni kosa kisheria na pia ni hatari kubwa inayoweza kusababisha majanga kama milipuko ya moto.

"Kutokana na ongezeko la vyombo vya usafiri kama pikipiki, tumeamua kupunguza gharama za kuanzisha vituo vya uuzaji mafuta ili viweze kujengwa katika maeneo mbalimbali hasa vijijini, ili kuepuka uuzaji mafuta katika vidumu," anasema.

Pia, Kaguo anahadharisha kuwa shughuli zote zinazohusu mafuta ya petroli, ni lazima zifanyike kwa umakini na uangalifu mkubwa ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea.

Anashauri kuwa ni muhimu kuzingatia na kufuata Sheria, kanuni, viwango vya ubora na masharti ya leseni wakati wote huku akiwataka kuzingatia utunzaji, usafirishaji, utumiaji na uuzaji wa bidhaa za petroli.

UCHUMI

# Uvivu na kilio cha ajira kulivyouingiza mji Mpanda kashesheni vikundi vya wakabaji

• Majina yao; Damu Chafu, Manyigu, Kaburi Moja, Kunguru Mweusi, Mchelemchele, Mazombi, Wafu • Mkoa waigeuza ajenda, RPC awawashia moto

**Na Neema Hussein, Mpanda**

***JANA, ilikuwa sehemu ya kwanza ya makala hii, ikiwa na simulizi namna uongozi na wakazi walivyoshirikiana kufyeka vichaka, makazi ya wakabaji, ambao waligeuka tishio kubwa. Endelea na simulizi ya kilichojiri.***



Shule ya Msingi Mwangaza, Mpanda iliyoko jirani na makaburi, ambako ndiko kumekuwa ngome ya kupanga uhalifu usiku.. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN**

MJI wa Mpanda ulioko mkoani Katavi, mara zote wakazi wake wengi wanajishughulisha na uchumi wa biashara na kilimo, kukiwapo mzunguko wa pesa, huku sehemu kubwa ya waajiriwa ni wa serikalini na taasisi zisizokuwa za kiserikali.

Ndani ya mazingira hayo, ndipo napo kuna hofu ya kuwapo makundi ya kihalifu yaliyoibuka hata kuwarudisha nyuma wananchi wanaopambana kujipatia kipato halali, maana wanawapora vitu mbalimbali kama vile pesa, simu na wengine wanavunja nyumba zao kuwaibia.

Makundi hayo yamejipa majina maaarufu kama Damu Chafu, Manyigu, Kaburi Moja, Kunguru Mweusi, Mchelemchele, Mazombi na Wafu na staili yao imekuwa kuvizia maeneo ya mikusanyiko ya watu, kama vile kumbi za starehe, harusini, misibani na barabarani pale wanapokutana na mtu pekee, hasa nyakati za usiku.

Ni hali inayowafanya wakazi wa Mpanda kufanya shughuli bila ya kuwa na amani wakilazimika kuwahi nyumbani kutoka kwenye biashara zao, wakihofu kukabwa na kuporwa.

Ni uporaji wa kutumia silaha za jadi kama vile mapanga, visu, nondo, bisibisi na vingine vyenye ncha kali, hata ajenda hiyo ikaifikia ngazi ya kujadiliwa katika kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama cha Mkoa wa Katavi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, SACP, Ali Makame anasema sehemu kubwa ya vijana hao ni kuanzia umri wa miaka 14 hadi 32 na tayari wameshachukua hatua kubwa kuwasaka na kuwakamata, baadhi wameshafikishwa mahakamani na operesheni inaendelea kuwakabili.

Jeshi hilo lilifanya msako katika mitaa mbalimbali na hivi karibuni limetoa taarifa ya kukamatwa kwa vijana wengine 11 kutoka katika mitaa ya Nsemulwa, Majengo na Kazima katika wilaya ya Mpanda

"Sasa hivi mbona raha mtu unatembea mpaka saa 5 saa sita usiku, wala hupati tatizo lolote kwa kweli tulipongeze jeshi la Polisi limejitahidi sana kuwakusanya hawa vijana mtaani sa hizi mtaa umetulia," anasema Juma Shabani, mkazi wa Manipsaa Mpanda.

> **"Vijana wanapomaliza shule hawajui wafanye nini, hata wazazi wao pia hawawafuatilii kabisa. Njia rahisi ya kujipatia kipato wanaona bora waingie huko, kumbe ndio wanaenda kupotea kabisa.**

Mkazi Jackson Phillipo, anaielezea Nipashe kwa kauli: "Ni vijana wadogo wadogo! Chanzo cha makundi haya kwangu mimi naona ni ushawishi unaotokea kwenye makundi rika, wengi wanaingia huko pasipokuwa na elimu yoyote ya kujua wanafanya vile kwa faida ipi au hasara ipi katika jamii.

"Vijana wanapomaliza shule hawajui wafanye nini, hata wazazi wao pia hawawafuatilii kabisa. Njia rahisi ya kujipatia kipato wanaona bora waingie huko, kumbe ndio wanaenda kupotea kabisa.

"Kitu kingine mimi nadhani vijana wengi wanataka mafanikio ya haraka yaani anahisi akifanya hivo atapata labda mali, pesa nyingi kumbe hapana. Mimi nashauri tu labda wazazi wangewasomesha watoto na elimu ya dini ili wapate hofu ya Mungu."

Hiyo inaendana na maoni ya Juma Shabani, kwamba:"Mimi naona tatizo kubwa ni wazazi kutokuwajibika. Tuangalie kabla ya kuwawajibisha hawa vijana, lazima tuangalie kwanza je wazazi wanatimiza wajibu wao, Kabla Jeshi la Polisi au serikali halijawahukumu?.

Ivo Chambala, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Makanyagio, eneo mojawapo maarufu kwa uhalifu, anaisimulia Nipashe kuwa ongezeko la makundi ya kihalifu linachangiwa na serikali kunyimwa ushirikiano kutoka kwa wazazi wasiojua shughuli za watoto wao, hata wanakolala.

"Kama wiki mbili zilizopita kuna kundi la mitaa jirani kutoka kata ya Misunkumilo, Shanwe na Kigamboni walivuka huku majira ya saa mbili (usiku) kuja kuvamia na kuleta fujo ya kutaka kupora watu, lakini kwa kushirikiana na viongozi wenzangu, tulilisambaratisha hilo kundi na kutoa taarifa kwa Polisi Kata wetu.

"Tulikuja kungundua ni sehemu ya vijana wengi ambao wapo majengo na kituo chao kinakuwa ni Shule ya Sekondari Mwangaza, ndio ilikuwa kituo wanachokutana mara kwa mara. Ukiwaona ni kama wameenda kwa mazoezi ya mpira kumbe wanakuwa ukingoni mwa makaburi na kupanga mipango yao ya kihalifu.

"Sasa katika vikao vyetu tulikua tunajua kabisa hilo eneo la makaburi ya Mwangaza ni eneo hatarishi hasa tukiliacha likiwa chafu sababu vitendo vyote vya kihalifu lilikuwa hilohilo chaka linawahifadhi wavuta bangi, hata mali za wizi zilikuwa zikifichwa katika hayo makaburi, anasema Chambala."



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, SACP, Ali Makame; ndiye kavisambaratisha vikundi.

**BANGO LA RC**

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko amekuwa akikemea vikundi hivyo tena kwa majina, akiwasisitiza vijana kubadilika, kwa kutafuta kipato cha halali.

Ni mara kadhaa Nipashe imemshuhudia akitenga muda wake kukutana na vijana na kuzungumza nao, ikiwemo kusikiliza kero zao, hata kuwasaidia pale inapobidi.

Hivi karibuni alipozuru katika shughuli za vijana wabeba mizigo waliounda umoja wao kumiliki miradi kadhaa unaoitwa Trans Cargo, amewasisitiza vijana kuondokana na utegemezi na kuondoa umasikini uliokithiri.

"Mara nyingi mwili wa binadamu haukubali yaani ana afya njema, amekula ameshiba, halafu amekaa hana kitu cha kufanya, ukiona mtu yuko hivo huyo mtu ni hatari sana! Kwa sababu ni lazima kwa mujibu wa asili yetu 'nature' ya miili yetu, atatafuta jambo la kufanya kwa ajili ya kutumia ile nguvu yake," anasema Mkuu wa Mkoa.

Mzee Charles Anthony, mwenyeji mkongwe wa mjini Mpanda, anaunga mkono kauli ya Mkuu wa Mkoa Mwanamvua, akisema: "Changamoto za vijana sasa hivi ni nyingi sana wengi wanawaza kuajiriwa tu, sasa ile inawapa shida. Zamani ilikuwa ukitoka darasa la saba la nane unapata kazi, usipopata kazi unashika jembe unalima au shughuli zingine.

"Sasa hivi hilo halipo! Kwanza 'kinacho- wakosti' (kinachowagharimu) ni mitaji, mitaji hawana. Pia, huwa nawaza wakikamatwa kwanini wanaachiwa? Watu mmeshajua ni wahalifu, mnawaachia tena wakirudi wanafanya uhalifu!"

Mkazi Evarist Katoto, anafafanua kupitia simulizi akisema: "Kulikuwa kuna watu hapa Mpanda Hoteli (mtaa wa kiserikali) sio watu, hao ni balaa! Si bora sasa hivi, ilikuwa hutembei kwa raha. Unaweza ukatembea, ukashangaa tu ngwala, kofi, umenyang'anywa simu, umesachiwa, umechukuliwa hela, unabaki unapiga kelele na hamna wa kukusaidia."

**ULINGO WA MIKASA**

Juvenary Deus, ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Msasani, Mpanda anaisimulia Nipashe, kuna wakati wizi umefanyika mchana, ila sasa usalama umetawala kutokana na vikundi vingi vya kihalifu kukamatwa na mtaa wake umetulia.

Anasema, watu waliokuwa wakikabwa katika eneo hilo, zaidi ni abiria kutokana na mtaa huo kuwa karibu na stesheni, pia hata wapita njia hasa wafanyabiashara waliokuwa wakitoka kwenye biashara zao.

"Pia, hata siku za kawaida ambazo treni haipo basi wanakaa wanamvizia mtu yeyote watakayemuona labda amebeba kibegi chochote wanamuona mwonekano wake mzuri, basi wanamfuatilia nyuma mpaka sehemu fulani, halafu wanajifanya kuwa wao ni askari wapelelezi.

"Yaani mbinu wanayotumia hadi mtu, aamini wanaenda kwa wale migambo migambo wanakubali kuchukua fedha kutoka kwao wanavua zile nguo wanawapa halafu wanapiga nazo picha za paspoti wanaenda kutengeneza vitambulisho vya kuonyesha kuwa wao ni askari au mgambo.

"Sasa wakimkamata mtu wanamuonyesha hicho kitambulisho na yeye anakubali anawafuata akifika huko anawakuta na wengine kwenye kichaka ndio wanamkaba sasa hizo ndio zilikuwa mbinu zao.

"Mimi mpaka nililala ndani, ikaonekana labda nashirikiana nao maana ilionekana, baadhi ya vitu vinaingia huu mtaa vya wizi na wanafanya biashara humu humu, mazoezi ya ukabaji yanafanyika kwenye mtaa huu, lakini baada ya kufuatilia kiundani zaidi wahusika walibainika na walikamatwa na mpaka hivi sasa wako ndani," anasema.

Anasema, kwenye kikundi cha Damu Chafu, watu wazima wakawa wanawapa watoto silaha kama nondo kwenye majira ya saa mbili na saa tatu, akiweka mfano hai, penye shule ya Sekondari Kashaulili, walikogundua watu wazima usiku wakishiriki njama na watoto wanaowaweka katika sehemu za maficho kushiriki uhalifu.

"Wakipita watu wale watoto wanaanzisha fujo, wale watu wazima wanafanya kama wanajipitisha ili waamue ule ugomvi, kumbe wao ndio wamewaagiza wale watoto, hapo wanaingilia na kumkaba mtu, wanamuumiza na kumpora.

Anasema, Polisi imechangia sana kufanikisha kukabili uhalifu huo na watuhumiwa wamekamatwa, hali iliyorejesha usalama wa mji kwa ujumla.

Taasisi mbalimbali nazo zikaingilia kati kusaidiana, ikiwamo Jeshi la Magereza kushiriki kufyeka mapori na vichaka kama vya makaburi ya Mwangaza na mapori ya Stesheni, ambako kulitumiwa kama vituo vya kupanga na kufanya uhalifu, pia kuhifadhi silaha na mali zilizoibwa.

TAFAKURI YA MLALAHOI




## Utamaduni wetu Watanzania umelalia wapi?



**NA JOSEPH KULANGWA**
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

NILIPOANZA kugundua napenda muziki nikiwa shuleni, nilijunga na bendi ya shule-Brass Band. Nikawa nafurahi sana kupiga ngoma, huku wanafunzi wenzetu wamejipanga mstarini kukaguliwa kabla ya kungia madarasani.

Nilishangaa kuwa naweza kumudu kupiga ngoma ndogo zikisindikizwa na nyingine tatu na kubwa moja na filimbi. Bahati mbaya, shule yetu haikuwa na uwezo wa kununua matarumbeta au saxophone. Hivyo tukaishia kwenye vifaa vichache tu.

Baada ya kumaliza elimu ya msingi, wakati huo nikisubiri matokeo, nikawa na shauku sana ya kuhudhuria maonyesho ya bendi ya dansi iliyokuwa ikitumbuiza katika mji niliokuwa naishi na wazazi wangu-Jazz Band.

Mapenzi hayo yalinifanya nisiwe nakosa maonyesho hayo hususan yaliyofanyika mchana, katika ukumbi uliokuwa unamilikiwa na Jeshi la Polisi katika mji niliokuwa naishi. Hakika ilikuwa raha kushuhudia wanamuziki wakipiga ala na kuimba.

Katika mazoea hayo, iko siku nikiwa ukumbini nilijikuta nami naambiwa nijaribu kupiga tumba. Nilifanya hivyo hata bila mafunzo, lakini nikaweza nikadenda na mirindimo. Tangu hapo muziki ukaniingia akilini, lakini sikusahau shule.

Ndivyo ilivyotokea nikawa napendelea kwenda kushuhudia maonyesho ya muziki ya wanamuziki mahiri na nguli nchini, kama Mbaraka Mwinshehe, Marijani Rajabu na Patrick Balisidya na wengine wengi.

Wanamuziki hao wote walikuwa wakiimba na kupiga ala na umaarufu wao ukajijenga katika hilo wakitikisa nchi na Bara la Afrika

Enzi za muziki wa dansi kutawala nchi zimepita na sasa tumegubikwa na muziki unaojulikana kama muziki wa Bongofleva, muziki wa vijana usioakisi utamaduni wetu wa kitanzania. Lakini, tunaufurahia na kuupa kipaumbele kana kwamba nchi hii haina Wizara inayosimamia utamaduni.

Muziki wa dansi uliokuwa na vionjo vya utamaduni wa kitanzania umepotea, hivi sasa tunauona muziki huo kuwa ndio wa kwetu tukichekelea tukidhani unadumisha mila zetu, kumbe ni tofauti kabisa.

Hivi sasa ukifungulia redio muziki unaosikika ni wa lugha ya Kiswanglishi (Ulaya), Kiswanaija (Nigeria) na Kiswazulu (Afrika Kusini), kwenye kumbi ni wapi hutasikia muziki wenye vionjo vya Kizungu, Kinaijeria, Kiafrika Kusini yaani Amapiano?

Katika mirindimo ya kigeni, utasikia maneno ya kigeni na ya Kiswahili machache yaliyosheheni lugha ya matusi, lugha ya faragha ya mke na mumewe, na sisi wasikilizaji tukishangilia na kucheza kama hatunazo.

Ilishangaza siku moja, nchi ikatembelewa na kiongozi wa kitaifa kutoka Burundi, Rais wa nchi hiyo akiwa na mwenyeji wake, mbele ya kadamnasi ya Watanzania, akaitwa msanii wa muziki huo tunaouita wa kizazi kipya usiogemea utamaduni wa nchi hii, akatakiwa kutumbuiza, ghafla akaimba wimbo unaitwa Uno.

Mwimbaji huyo asiyetumia ala hata moja akaanza kuimba viuno vya wasichana wasanii wenzake akimwimbia Rais wa nchi ya kigeni akiwa na Rais mwenyeji nasi tukishangilia na kutuza kama hamnazo!

Nakumbuka mwaka 1978 Tanzania ilipovamiwa na majeshi ya Iddi Amin wa Uganda, hapo ndipo Watanzania walipoonyesha mshikamano wa ajabu, kila mtu akiwa tayari kupambana, ndipo bendi za JKT Kimulimuli na Mwenge Jazz zilipopiga nyimbo za kuhamasisha mpaka kuleta ushindi.

Hivi waimbaji wetu wa leo, au waghani hawa wasiojua kupiga ala, yakitokea ya kutokea, watakuwa na tungo za kuisaidia nchi?

Tumekaa tukakubali kuimbiwa nyimbo za matusi na sisi kuzicheza kwa mitindo ya Amapiano kweli, huku tukitazama jinsi utamaduni wetu unavyoangamia kila kukicha kweli? Hivi uko wapi huo utamadui kama si kichekesho?

Hebu wenye dhamana ya kusimamia utamaduni wetu, tusikalie kufurahia nyimbo badala yake tuingie kwenye maudhui na uwasilishaji katika kulinda kilicho chetu, isijetokea siku zijazo vizazi vijavyo vikachapa makaburi yetu kwa ubozi huu tunaouendekeza. Alamsiki!

UGENI WA TALIBAN AFGHANISTAN

# Hali mbaya watu wengi wauza figo wahimili makali maisha nyumbani



Watoto wakihudumiwa chakula kukimu njaa nchini Afghanistan. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

RAIA wa Afghanistan sasa wanawapa watoto wao wenye njaa dawa za kuwatuliza, wengine wameuza binti zao na viungo vyao ili kujikimu kimaisha.

Katika majira ya pili ya baridi tangu Taliban kuchukua mamlaka na fedha za kigeni kupigwa tanji, mamilioni ya watu wanakabiliwa na tishio la njaa.

"Watoto wetu wanaendelea kulia, na hawalali. Hatuna chakula," Abdul Wahab anasema, akiwa na ufafanuzi: "Kwa hiyo tunaenda kwenye duka la dawa, tunanunua vidonge na kuwapa watoto wetu ili wapate usingizi."

Anaishi nje kidogo ya Herat, jiji la tatu kwa ukubwa nchini humo, katika makazi ya maelfu ya nyumba ndogo za udongo ambazo zimekua kwa miongo kadhaa, zimejaa watu waliokimbia makazi yao na kukumbwa na vita na majanga ya asili.

Abdul ni miongoni mwa kundi la karibu, wanaume 12 waliokusanyika karibu, kisha wanaulizwa ni wangapi walikuwa wanawapa watoto wao dawa za kuwatuliza? Ajabu ya majibu: "Wengi wetu, sisi sote," walijibu.

**USHUHUDA WA AJABU**

Ghulam Hazrat, akaingiza mkono kwenye mfuko wa kanzu na akachomoa kipande cha vidonge. Zilikuwa dawa za kawaida kutibu matatizo ya wasiwasil; vidonge vitano sasa vinagharimu sawa na kipande cha mkate.

Ghulam ana watoto sita, mdogo akiwa na mwaka mmoja, wote anawapatia dawa na wengine wakatuonyesha vipande vya escilatopram na vidonge vya sertraline ambavyo walisema walikuwa wakiwapa watoto wao.

> **"Wiki kadhaa baadaye nilipigiwa simu ikinitaka nije hospitali. Walifanya vipimo, kisha wakanidunga sindano iliyonifanya kupoteza fahamu. Niliogopa lakini sikuwa na la kufanya.**

Madaktari wanasema kwamba dawa hizo wanapopewa watoto wadogo na hawapati lishe ya kutosha, zinasababisha uharibifu wa ini, pamoja na matatizo mengine kama vile uchovu wa kudumu, usingizi na matatizo ya tabia.

Wanaume katika eneo hili nje ya Herat wanatatizika kupata kazi. Katika moja la duka dawa, ikagundulika kwamba mtu anaweza kununua vidonge vitano vya dawa zinazotumiwa kwa bei ya kipande cha mkate.

Familia nyingi zilikuwa zikigawana vipande vichache vya mkate kila siku na mwanamke mmoja akasema, walikula mkate mkavu asubuhi na usiku waliuchovya kwenye maji ili kuufanya uwe na unyevu.

Umoja wa Mataifa sasa unasema "janga" la kibinadamu sasa linatokea nchini Afghanistan."Wengi wa wanaume katika eneo la Herat hufanya kazi kama vibarua wa kila siku. Wamekuwa wakiishi maisha magumu kwa miaka mingi.

Lakini wakati Taliban walipochukua madaraka Agosti iliyopita, bila serikali mpya kutambuliwa kimataifa, fedha za kigeni zilizoingia Afghanistan zilizuiliwa na kusababisha kuporomoka kwa uchumi ambao uliwaacha wanaume bila kazi.

Siku wanapopata kazi, wanalipwa zaidi ya dola moja. Kila mahali watu wakilazimika kuchukua hatua kali ili kuokoa familia zao kutokana na njaa.

**MUUZA FIGO**

Ammar (sio jina lake halisi) anasema alifanyiwa upasuaji wa kutoa figo miezi mitatu iliyopita na akaonyesha kovu la inchi tisa - alama za kushonwa zinaonekana kwenye tumbo lake. Ana umri miaka 20, katika kile ambacho kingekuwa kilele cha maisha yake.

"Hakukuwa na njia ya kutoka. Nilikuwa nimesikia unaweza kuuza figo katika hospitali ya mtaani. Nilikwenda huko na kuwaambia nataka, " anasimulia mtu huyo.

"Wiki kadhaa baadaye nilipigiwa simu ikinitaka nije hospitali. Walifanya vipimo, kisha wakanidunga sindano iliyonifanya kupoteza fahamu. Niliogopa lakini sikuwa na la kufanya," anasimulia muuza figo huyo, miezi mitatu iliyopita.

Anasema akalipwa dola 3,100 na sehemu kubwa ya hela hiyo alitumia kulipa pesa alizokopa kununua chakula cha familia yake.

"Tukila usiku mmoja, hatutakula mwingine. Baada ya kuuza figo yangu najiona kuwa nusu mtu. Najihisi kukosa matumaini. Maisha yakiendelea hivi ninahisi naweza kufa," anasema.

Kuuza viungo kwa pesa sio jambo geni nchini Afghanistan. Watu walikuwa wakifanya hivyo hata kabla ya Taliban kuchukua mamlaka. Lakini sasa, hata baada ya kuchukua hatua hiyo ya kusikitisha, watu wanaona bado hawawezi kujikimu kimaisha.

Katika nyumba nyingine mama naye akauza figo yake miezi saba iliyopita. Pia alilazimika kulipa deni, pesa alizokopa kununua wanyama wa kufuga nyumbani (kondoo).

Wanyama hao walikufa katika mafuriko miaka michache iliyopita na kumfanya apoteze njia zake za kujikimu. Dola 2,700 alizopata baada ya kuuza figo hazitoshi.

"Sasa tunalazimishwa kumuuza binti yetu wa miaka miwili, watu tuliowakopa wanatunyanyasa kila siku wakisema tupatie binti yako ikiwa huwezi kutulipa," anasema.

"Nilihisi kudhalilika kutokana na maisha tunayoishi. Wakati mwingine naona heri kufa kuliko kuishi hivi," mume wake alisema.

Tukasikia visa tofauti vya watu kuuza binti zao. "Nilimuuza binti yangu wa miaka mitano kwa 100,000 za Afghanistan," Nizamuddin alisema.

Hiyo ni chini ya nusu hela unazopata ukiuza figo huenda, kulingana na kile tulichopata ardhini. Akauma mdomo, macho yakamtoka. Heshima ambayo watu hapa waliishi nayo imevunjwa kutokana na njaa.

"Tunaelewa ni kinyume na sheria za Kiislamu, na kwamba tunaweka maisha ya watoto wetu hatarini, lakini hakuna njia nyingine," Abdul Ghafar, mmoja wa wakuu wa jamii hiyo, anasimulia.

Nazia bado anaishi na wazazi wake lakini familia yake ilimuuza alipokuwa na umri wa miaka 14.

Katika nyumba nyingine tulikutana na Nazia mwenye umri wa miaka minne, msichana mdogo mchangamfu akicheza na kaka yake Shamshullah mwenye umri wa miezi 18.

"Hatuna pesa za kununulia chakula, kwa hivyo nilitangaza msikitini kwamba nataka kumuuza binti yangu," baba yake Hazratullah alisema.

Nazia ameuzwa kwa familia nyingine kusini ya Kandahar ili akaolewe. Atakapotimiza umri wa miaka 14, atakabidhiwa kwa familia yake mpya.

Kufikia sasa Hazratullah amepokea malipo mara mbili.

"Sehemu kubwa ya pesa hizo nilizitumia kununua chakula, na nyingine nikatumia kumnunulia dawa mwanangu mdogo. Mwangalieni hana afya," Hazratullah alisema huku akivuta shati la Shamsullah ili kutuonyesha tumbo lake lililokuwa limevimba.

Kuongezeka kwa kasi kwa viwango vya utapiamlo ni ushahidi wa athari ya njaa kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano nchini Afghanistan.

Shirika la Madaktari Wasio na Mipaka (MSF) linaelezea kuongezeka kwa asilimia 47 ikilinganishwa na mwaka jana idadi ya watoto wanaolazwa katika vituo vyao vya kutibu utapiamlo kote nchini.

Kituo cha lishe cha MSF huko Herat ndicho kituo pekee cha utapiamlo chenye vifaa vya kutosha kinachohudumia sio tu kwa Herat, lakini pia katika majimbo jirani ya Ghor na Badghis, viwango vya utapiamlo vimepanda kwa asilimia 55 mwaka jana.

• ***Kwa mujibu wa BBC.***

FEDHA

# Tembo Nickel iliyoonyesha nuru ya mapinduzi katika elimu Ngara

**Na Mwandishi Wetu,** NGARA

• Programu ya kurudisha kwa jamii yatatua kero ya ukosefu miundombinu



Jengo la madarasa mawili na ofisi ya mwalimu mkuu katika Shule ya Msingi Muganza, lililojengwa kwa ushirikiano wa wananchi, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara na Kampuni ya Tembo Nickel, likiwa limekamilika. **NA MPIGAPICHA WETU**

SUALA la wanafunzi kuacha au kukatisha masomo kwa sababu mbalimbali limekuwa sugu hali ambayo imekuwa kikwazo kwa maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

Katika wilaya ya Ngara mkoani Kagera, takwimu rasmi za elimu zinazoishia Machi 31, 2022, zinaonyesha wanafunzi 912 sawa na asilimia sita ya wanafunzi wote wa wilaya hiyo, waliacha shule kwa sababu mbalimbali.

Sababu zinazotajwa kuchangia hali hiyo ni pamoja na wanafunzi kujishughulisha na biashara ndogondogo, kazi za ndani, ndoa za utotoni na kulea familia, umbali kutoka nyumbani kwenda shuleni, mwamko duni wa elimu kwa wazazi na mazingira yasiyo rafiki kwa wanafunzi.

Kwa kuliona hilo, Julai 8, 2022 Kampuni ya Tembo Nickel, ilitia saini mkataba wa makubaliano (MoU), ya utekelezaji wa miradi ya kijamii ya jumla ya Sh. milioni 207.8 katika wilaya ya Ngara na moja ya maeneo yaliyowekewa mkazo ni sekta ya elimu. Lengo la kufanya hivyo ni kutafuta jawabu la upungufu wa miundombinu, hasa kwenye vijiji vinavyozunguka mgodi huo wa uchimbaji wa madini ya Nickel.

Wakati wa utiaji saini, Meneja Mkazi wa Tembo Nickel, Benedict Busunzu, alisema kampuni inatia saini mkataba huo wa kurudisha kwa Jamii (CSR) wakati ambao bado hata uchimbaji haujaanza.

"Tunaonyesha ushirikiano, upendo na ujirani mwema mapema tu. Wahenga wanasema nyota njema huonekana mapema sana," alisema.

Ikiwa imepita miezi minne tangu kuanza kwa utekelezaji wa mkataba huo, hadi sasa baadhi ya miradi imekamilika huku mingine ikiwa katika hatua za mwisho.

Gervase Chiza, Kiongozi wa Kitengo cha Maendeleo ya Jamii, Idara ya Uhusiano kutoka Tembo Nickel, anasema katika utekelezaji wa miradi hiyo, wanashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara na wananchi wa vijiji husika.

Anaongezea kuwa miradi wanayotekeleza iko katika shule tano za msingi na moja ya sekondari, zikiwa katika kata za Bugarama, Bukiriro, Muganza, Rulenge, Mbuba na Keza. Pia anasema miradi hiyo inajumuisha ukarabati wa vyumba vya madarasa, kumalizia vyumba vilivyokuwa katika hatua ya maboma, ofisi za walimu na kununua madawati.

Kadhalika, kwenye miradi hii kuna vyumba 10 vya madarasa, ofisi tatu za walimu, madawati 80 kwenye shule za msingi na viti pamoja na meza zake 80 kwa shule moja ya sekondari.

"Kwenye utekelezaji wa miradi hii ya elimu, kuna baadhi utekelezaji wake upo kwenye asilimia zaidi ya 80 na mingine imekamilika," anasema Chiza.

Kuhusu ushiriki wa wananchi, Chiza anasema jukumu la wananchi ni kuchangia nguvu kazi, vifaa vya ujenzi vya asili kama mawe na utunzaji wa miundo mbinu inayojengwa. Anasema miradi yote wanayotekeleza inaibuliwa na wananchi kupitia mikutano mikuu katika vijiji husika na kupitia ngazi za kata hadi wilaya.

Wakati Chiza akisema hayo, baadhi ya walimu, wanafunzi na wazazi wa baadhi ya shule zilizofaidika na miradi hiyo, wanaeleza jinsi upungufu wa miundombinu hiyo ulivyowaathiri na namna sasa wanavyoona mwanga siku za usoni.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Muganza, Shaaban Juma, anasema shule yake ina wanafunzi 555 huku ikiwa na vyumba vya madarasa vitano vinavyotumika na wanafunzi wa darasa la awali hadi la saba. Anasema wanafunzi wa darasa la awali pekee wako 108, hivyo wamelazimika kuomba jengo la mahakama lililopo eneo la shule litumike kuwafundisha watoto hao.

Ili kukidhi mahitaji ya waliobaki, anasema ilibidi kuomba kibali ili wale wa darasa la kwanza na la tatu, wawe wanaingia kwa zamu ambapo darasa la tatu wanaingia asubuhi hadi saa sita na wale wa darasa la kwanza wanaingia saa sita hadi saa nane.

> **Wakati mwingine ilikuwa inabidi kutumia mgambo kushika wananchi na kuwalazimisha kulipa kwa sababu ukweli ni kwamba wengi wao hali zao ni duni.**

"Ukiangalia sera inavyotaka na jinsi hali ilivyo ni vitu viwili tofauti. Ili kukidhi mahitaji ya sera tungehitaji vyumba vinne na walimu wanne, kwa sasa mwalimu ni mmoja na wanasomea kwenye chumba cha mahakama tulichoomba na chenyewe ni kidogo na hali yake ni kama unavyoiona, kwa darasa la kwanza hadi la saba upungufu ni huohuo pia," anasema.

Anasema Agosti, mwaka huu, Tembo Nickel ilianza kumalizia madarasa ambayo yalikuwa yamesimama kwa muda mrefu na nyumba moja ya walimu, ujenzi ambao umekamilika.

"Kwa kiasi kikubwa haya majengo yatatusaidia kupunguza msongamano darasani, lakini hata ofisi za walimu hatuna kabisa, kwa sasa hapa nilipo ilikuwa stoo na walipo walimu ni maktaba, na utaona mvua ikinyesha panavuja lakini kwa bahati nzuri ofisi ya mwalimu mkuu imepatikana bado ya walimu," anaongeza.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Muganza, Jackson Gwabjala, anasema kabla ya kupata msaada wa Tembo Nickel, walikuwa wanafanya ujenzi wa madarasa kwa kuchangishana jambo lililokuwa linafanya utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua.

"Wakati mwingine ilikuwa inabidi kutumia mgambo kushika wananchi na kuwalazimisha kulipa kwa sababu ukweli ni kwamba wengi wao hali zao ni duni," anasema.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyabihanga, Nichodemus Nicholaus, anasema shule yake ina wanafunzi 670 kuanzia darasa la awali hadi la saba.

"Darasa la awali tuna wanafunzi 130 na wote wanatumia chumba kimoja cha darasa, wengine wapo wastani wa 80 kwa darasa. Hatukuwa na ofisi ya walimu, tulikuwa tunatumia jengo la maktaba, majengo haya mapya yatatusaidia kupunguza mrundikano wa wanafunzi na tunaamini hata taalamu itapanda kwa sababu walimu wataweza kuhudumia wanafunzi vizuri.

"Wanafunzi pia wataweza kuandika vizuri na kufanya mitihani bila kuigiliziana kwa sababu kwa sasa wanakaa hadi watano kwenye dawati moja," anasema Mwalimu Nicholaus.

Anasema majengo yaliyomaliziwa na Tembo Nickel, utekelezaji wake ulianza kwa mipango mbalimbali ya Halmashauri, wananchi na mwingine wa Education Programme For Results (EP4R).

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ruhuba, Yustas Benedicto, anasema shule yake yenye wanafunzi 517 ina madarasa nane yanayochukua wanafunzi wa kuanzia darasa la awali hadi la saba.

"Pamoja na yote bado upungufu wa madarasa upo, bado wanafunzi wanakosa vipindi vingi kwa sababu ni vigumu kufanya mgawanyo, ili kuwe na utoshelevu sisi tunatakiwa tuwe na vyumba vya madarasa 12. Tembo Nickel wametusaidia sana, tunaamini taaluma kwenye shule yetu itapanda kwa sababu sasa angalia mwalimu akiwa darasani anaweza kuwasiliana na wanafunzi," anasema.

Philipo Bahema (60), mkazi

INAENDELEA UK.20

# Tembo Nickel iliyoonyesha nuru

INATOKA UK.19

wa Kijiji cha Ruhuba, anasema licha ya kwamba madarasa yanayokarabatiwa na Tembo Nickel kwa sasa yalikuwa yanatumika, anasema hali yake haikuwa nzuri na wananchi walishindwa kuyafanyia matengenezo.

"Hali ya wananchi si nzuri, kuwaambia wachange ili kurekebisha haya madarasa ilikuwa haiwezekani, tunashukuru huu msaada naamini watoto wetu watasoma kwenye mazingira mazuri," alisema.

Naye Philibata Lauriani (32) mwenye watoto wawili katika Shule ya Msingi, Ruhuba, anasema shule hiyo tangu ijengwe mwaka 2007 ilikuwa haijafanyiwa marekebisho yoyote.

"Madarasa yalikuwa yanatumika lakini yalikuwa chakavu na kuna vitu vingi vilikuwa havijakamilika, kwa sasa Tembo Nickel wameyafanya yamekuwa ya kisasa, yana vigae (tailizi), dari lipo, plasta nzuri kwa kweli watoto watasoma kwenye mazingira mazuri,"alisema.

Baraka Kristopha, mwanafunzi wa darasa la tano shuleni hapo, anasema moja ya kero ya madarasa yanayokarabatiwa na Tembo ilikuwa ni vumbi, hali iliyokuwa inawawia vigumu wakati wa kufagia.

Naye Florida Kliani, mwanafunzi wa darasa la sita, anasema madarasa wanayotumia sasa na yale ya awali, sakafu ilikuwa imeharibika huku yakiwa hayana milango wala madirisha, hivyo anaamini akihamia kwenye madarasa mapya atakuwa na utulivu.



Wajumbe wa Serikali ya Kijiji cha Ruhuba kilichopo Kata ya Mbuba wilayani Ngara, wakiwa kwenye kikao cha kujadili vipaumbele vya kijiji hicho ili viweze kuingizwa kwenye Mpango wa Kurudisha kwa Jamii (CSR) wa Tembo Nickel, kwa mwaka 2023. **NA MPIGAPICHA WETU**

Sofia Emanuel, mwanafunzi wa darasa la sita, anasema vyumba vipya vya madarasa vinavutia na tofauti na wanavyotumia sasa, hivyo anaamini vitakuwa na mazingira mazuri ya kujifunzia.

Takwimu za wilaya hiyo zinaonyesha mahitaji ya vyumba vya madarasa kwenye wilaya nzima kwa shule za sekondari ni 462, vilivyopo ni 395 hivyo kufanya upungufu kuwa 63 wakati kwa shule za msingi mahitaji ni vyumba 2,075 na vilivyopo ni 994 na upungufu ni 1,081.

Kwa upande wa nyumba za walimu, kwa upande wa shule za sekondari mahitaji ni 453, zilizopo 99 na upungufu 354 wakati kwa shule za msingi mahitaji ni 1150 na zilizopo ni 263 upungufu ukiwa 887.

Kwa kutambua umuhimu wa miundombinu hiyo muhimu ambayo inaweza kuchangia kuboresha mazingira ya elimu na kupunguza utoro kwa wanafunzi, Kampuni ya Tembo Nickel, inaendelea na mchakato wa kushirikisha wadau muhimu kuanzia ngazi za vijiji hadi wilayani ili kujua vipaumbele ambavyo vitafanyiwa kazi kuanzia mwakani.

Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alitambua umuhimu wa miradi ya CSR inayofanywa na Tembo Nickel kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

Chalamila akizungumza na maofisa wa Tembo Nickel waliofika ofisini kwake kumweleza hatua za mradi huo ulipofikia, alisema ni jambo jema kwa kampuni hiyo kutekeleza miradi ya CSR, huku akiihimiza ifanye mambo makubwa zaidi katika eneo hilo.

"Nitatamani siku moja mniambie njoo uzindue kitu fulani hiki tumefanya," anasema Chalamila akitambua mchango wa Tembo Nickel kwenye miradi ya maendeleo mkoani kwake.

Mkataba wa Tembo Nickel na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara juu ya utekelezaji wa miradi hii ambao kwa sasa unaelekea ukingoni, ulitiwa saini mbele ya Baraza la Madiwani, ambapo mwenyekiti wa baraza hilo, William Bambala, aliishukuru Tembo Nickel kwa kutia saini mkataba huo, yeye na madiwani wenzake watahakikisha wanafuatilia utekelezaji wa mkataba huo.

Mbunge wa Ngara, Ndaisaba George Ruhoro, alisema ili kujenga miundombinu ya madarasa na zahanati walikuwa wakichangisha wananchi, lakini fedha zilizotolewa na Tembo Nickel zitapunguza mzigo kwa wananchi.

"Mgodi huu ni wa miaka 33, lakini kabla hata hiyo miaka hatujaanza kuihesabu sasa hivi wako kwenye maandalizi ya mgodi matunda tumeanza kuyaona, hii ni hatua kubwa,"alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ngara, Solomon Kimilike, alisema mkataba uliosainiwa utasaidia umarishaji wa huduma za afya na kuboresha elimu kwenye kata zitakazoguswa.


"Niseme tu kupitia mradi huu Ngara itafaidika sana, kwa sababu mradi ukianza halmashauri itakuwa ikipata asilimia 0.3, fedha hiyo itakuwa sehemu ya mapato ya ndani ya halmashauri, itasaidia miradi mbalimbali kwenye maeneo yote ya wilaya na si vijiji vinavyozunguka mradi tu ,kama ilivyo sasa hivi,"alisema.

## CHEMSHABONGO NA -00 23 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. kiungo cha kutembelea
5. nasaba 8. kitu cha duara kinachofanya gari itembee
10.tayarisha 11.gari kubwa ya abiria 13.ghasia 14.vunja kanuni za nchi 15.Rome ni mji mkuu 16.safisha mwili 18.minyoo ya kuvulia samaki 20.dakika 60 22.shimo la kuzikia wafu 23.njiwa 24.Bamako ni mji mkuu 25.heshima


Chini:
1. askari wa akiba
2. toa sauti ya kuonyesha kukataa
3. lugha ya Pakistani
4. utoaji uhai kiumbe 5. masafa
6. kukataa kutii sheria za nchi
7. jicho 9. tia hatarini
12.itikadi ya kuendesha uchumi na utamaduni wa nchi
17.taifa lililoasisiwa na Kwameh Nkrumah 18.sayari tunayoishi
19.dhihirishia kitu kilivyo
20.mdudu mdogo jamii ya chungu
21.mwanzo




## Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

KAAKAA
MAANANI
OSAMA
PAKA
KASHA
ARUSI
KISIWANI
MAISHA
AIBIKA
SHAA
MAISHA
MZAHA
MADIWANI
KINGA

OKA
TAI
AKA
MDAU
DANI
DHAKA
ARIA








# Polisi yashikilia watatu kwa kukutwa na meno ya tembo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya, linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kukutwa na nyara za serikali kama vile meno ya tembo baada ya kufanya msako na doria maeneo mbalimbali mkoani humo.

Kamishna Msaidizi wa Polisi Mkoa wa Mbeya, ACP Benjamin Kuzaga, akizungumza na waandishi wa habari jana, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni David Mwahaya (40) fundi cherehani, mkazi wa Tabata jijini Dar es Salaam aliyekutwa na vipande tisa vya meno ya tembo vyenye uzito wa kilogramu 17.4 vyenye thamani ya Sh. milioni 104.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa eneo la Lubele, Kata ya Ikimba, wilayani Kyela akitafuta mteja wa vipande hivyo alivyokuwa amevihifadhi kwenye mfuko wa sandarusi.

Mwingine ni Ninde Bundala (78) mkazi wa Iheha wilayani Mbarali, mkoani humo alikamatwa akiwa na pembe tatu za swala jamii ya tandala, kipande cha ngozi ya tandala na mafuta yanayodhaniwa kuwa ni ya mnyamapori yaliyohifadhiwa kwenye chupa mbili za plastiki.

"Aidha, mtuhumiwa alikutwa na silaha mbalimbali za jadi ambazo ni mikuki 16, podo lenye mishale sita, upinde mmoja historia inaonyesha ni mwindaji haramu na alikuwa akitafutwa kwa tuhuma ya kujeruhi akiwa na mwenzake aitwaye Mathidi Mboje,"alisema Kamanda Kuzaga.

Kamanda Kuzaga alisema pia jeshi hilo limewakamata vijana 10 kwa tuhuma za kukutwa na dawa za kulevya aina ya bangi debe mbili na kete 293 na gramu 30. Waliokamatwa ni Isaya Julius (28), Gisbert Mchilo (30), Jamson Furaha( 25) Emmanuel Joesph (22), Bryton Mkondya (24) Salum Masanja (29), Zawadi Mwampashi (26) na Emmanuel Frank (21) wakazi wa Wilaya ya Chunya.

Alisema baada ya kukamilika kwa upelelezi watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

Hata hivyo, alitoa wito kwa wananchi kuacha tabia ya kuhujumu miradi ya serikali ambayo inajengwa kwa manufaa yao na kuwataka kuachana na biashara haramu kwani Jeshi la Polisi halitamvumilia mtu yeyote atakayejihusisha na vitendo vya uhalifu na uvunjifu wa amani.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, ACP Benjamin Kuzaga, akionyesha kwa waandishi wa habari mkoani humo jana pembe za ndovu walizozikamata kwenye operesheni iliyofanyika hivi karibuni. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TGNP yaeleza athari za ukatili unaoendelea kwenye jamii

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WANAWAKE 30 kila siku hufanyiwa aina mbalimbali ya ukatili wa kijinsia ikiwamo wa kingono, ulawiti, ubakaji na vipigo hali ambayo imedaiwa kuwa ni idadi kubwa na hatari kwa usalama wa kundi hilo. Imeelezwa.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Ofisa Habari wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Monica John, ripoti ya Kituo cha Haki za Binadamu nchini (LHRC) ya 2019 jumla ya wanawake 11,838 walifanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Alisema ripoti hiyo inaonesha kila mwezi wanawake 928 hufanyiwa ukatili unaochangia kudidimiza shughuli zao kiuchumi.

"Ripoti ya LHRC mwaka 2019 inaonesha matukio ya ukatili wa kijinsia yaliripotiwa kwa Jeshi la Polisi yalikuwa zaidi ya 10,000 idadi ambayo inaonesha ukubwa wa tatizo hilo kwa jamii ambalo linachangiwa na mambo mbalimbali kama vile familia kutoripoti matukio hayo yanapotendeka,"alisema Monica.

Alifafanua kuwa vitendo vya ukabaji kwa mwaka 2019 viliripotiwa visa 7,837 kwa Jeshi la Polisi na mwaka 2021 viliripotiwa 6,305 idadi ambayo imepungua kwa asilimia 13.

Aidha, alisema idadi hiyo inaonyesha vimepungua kutokana na wananchi kupata elimu juu ya athari za vitendo hivyo kwa jamii na umuhimu wa kuviripoti kwenye vyombo vya dola ili kukomesha. Aliongeza utafiti uliofanywa na LHRC ulionyesha kuwa asilimia 52 ya wananchi waliofikiwa walikiri kushamiri wa vitendo vya ukatili wa kingono, ubakaji, ulawiti kwenye jamii.

Kwa mujibu wa Monica, vitendo vya ukatili wa kijinsia vinachangia kwa kiasi kikubwa hasara kwa serikali na familia kwa sababu hutumia fedha na muda mwingi kushughulikia masuala hayo kama vile kutibu waathirika, kusimamia kesi na muda ambao ungetumika kwenye shughuli nyingine za uzalishaji mali.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha jamii inakuwa salama na kutetea haki za wanawake na watoto nchini, maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia yamekuwa msaada mkubwa katika kukabiliana na vitendo hivyo.

Alisema maadhimisho ya siku 16 hutoa fursa kwa wadau wa haki za wanawake na watoto kukaa pamoja na kujadiliana namna ya kupinga vitendo vya ukatili kwa kijinsia dhidi ya makundi hayo.

Alisema TGNP ambao ni wadau wa masuala ya kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia na kutoa elimu kwa jamii kuachana navyo imeendelea kuwafikia wananchi hususani wanaoishi vijiji kuwajengea uwezo wa kuripoti pindi yanapotendeka. Miongoni mwa masuala tunayoyashughulikia ni kuhimiza haki na usawa kwa jamii ili kujenga taifa la watu wanaoheshimu na kulinda haki za wengine, kama kauli mbiu ya mwaka huu inayosema "Kila uhai una thamani tokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto," alieleza Monica na kuongeza:

"Katika siku 16 za kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia ukiwa ni mwaka wa 31 sasa itatoa nafasi ya kujadiliana vikwazo vinawakabili wanawake na watoto nchini na namna ya kulisaidia kundi hilo ambalo wamekuwa waathirika wa vitendo hivyo," alisema Monica.

Mkuu wa Dawati la Jinsia Mkoa wa Mbeya, Inspekta Loveness Mtemi, alisema polisi wataendelea kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa kuwahamasisha kuripoti pindi wanapofanyiwa.

Pia aliwahamasisha wanaume kutoogopa kuripoti vitendo vya ukatili ndani ya familia zao wakidai kuwa ni fedheha kuripoti. Alisema woga ndio husababisha wanaume wengi kuchukua maamuzi magumu ambayo yanagharimu maisha yao na watu wanaowazunguka.

# TRA Mbeya yajivunia uhusiano uliopaisha makusanyo ya kodi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Mbeya, imesema uhusiano mzuri na walipa kodi umeiwezesha kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 73.2 kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022.

Meneja Msaidizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mkoa wa Mbeya, Nuhu Suleiman, aliyasema hayo wakati wa maadhimisho ya wiki ya shukrani kwa mlipa kodi mkoani humo iliyoanza Novemba 18, mwaka huu.

Alifafanua kuwa mwaka wa fedha 2021/2022 walikusanya Sh. bilioni 73.2 ikilinganishwa na makusanyo ya 2020/2021 walikusanya Sh. bilioni 68, ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni tano sawa na asilimia saba.

Alisema Oktoba 2022 pekee walikusanya Sh. bilioni 5.8 wakati Oktoba ya 2021 walikusanya Sh. bilioni 4.7 sawa na ongezeko la asilimia 25 mafanikio hayo yametokana na hamasa waliyoipata walipa kodi kutambua umuhimu wa uzalendo kwa taifa.

Aliongeza mafanikio hayo yamejengwa na uhusiano mzuri pamoja na maridhiano ambayo yamesaidia ongezeko la makusanyo ya kodi bila matumizi ya nguvu na njia zenye migogoro.

"TRA tunapoadhimisha wiki ya shukrani kwa mlipa kodi tunahakikisha tunarudisha fadhili kwa wateja wetu kwa kuyafikia maeneo yenye uhitaji na faraja kutoka kwetu mwaka huu tumetembea Gereza la Ruanda na kutoa misaada ya vitu mbalimbali kwa ajili ya wafungwa,"alisema na kuongeza:

Pia tulitembelea Hospitali ya Rufani ya Mbeya wodi ya mama na mtoto tumetoa neti pisi 100 ili kuwalinda na ugonjwa wa malaria."

Ofisa Muuguzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Maridhia Mvungi aliishukuru TRA kwa msaada wa vyandarua kwa ajili ya kina mama na watoto wanaopata matibabu kwenye hospitali hiyo, akidai itasaidia kuwakinga na maradhi kama vile malaria.

Ofisa Mnadhimu wa Magereza ya Ruanda, Deotada Timothy, alisema ni nadra kwa taasisi za serikali kuwakumbuka na kuwapatia misaada ya hali na mali wafungwa na mahabusu.

Alisema uamuzi wa TRA kuwapatia misaada ya vitu mbalimbali wafungwa na mahabusu katika gereza la Ruanda imewapunguzia mzigo Jeshi la Magereza katika kuwahudumia. Aidha, aliwaomba kuendelea na utaratibu huo wa kuwatembelea mara kwa mara kwani bado wanahitaji msaada wa vitu mbalimbali kama vile nguo, magodoro chakula.



# Waapa kumlinda mganga wa jadi

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

UKISHANGAA ya Musa utayaona ya Firauni! Hivi ndivyo ilivyo kwa baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Seluka, Mpwapwa mkoani Dodoma ambao kwa kauli moja wameapa kumlinda mganga wa tiba asili baada ya kuamini amewaondolea mikosi ikiwamo wanawake na wanaume kuingiliana kimapenzi kwa njia ya miujiza.

Wakizungumza juzi katika mkutano uliosimamiwa na Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Kenneth Magayo, mmoja wa wananchi hao, Pendo Lameck, alisema baadhi ya matukio ya kishirikina yanayotokea ni pamoja na wanawake kuingiliwa kimapenzi na watu wasiofahamika pamoja na kung'atwa na mbwa kimiujiza.

"Tunaomba mganga huyu, Rasi, asisumbuliwe maana amesaidia kuokoa maisha yetu. Wanawake tumekuwa tunachafuliwa usiku bila kumwona mwanamume tunayefanya naye mapenzi, wanaume nao hivyo hivyo," alisema Magoyo.

Mwananchi mwingine, George Manyika, alisema kabla ya mganga huyo hajafika kijijini hapo, kulikuwapo na shida ya maji, lakini baada ya (Rasi) kwenda katika chanzo cha maji na kufanya tambiko, mpaka sasa maji yanapatikana kwa wingi.

"Sasa tutashindwaje kumwamini mganga huyo wakati amesaidia kuokoa maisha yetu kuwa watu waliapa maji kutopatikana hapa kijijini lakini sasa wanaona aibu baada ya maji kuanza kupatikana kwa wingi," alisema Manyika.

Naye Richard Magawa, alisema tatizo la ushirikina kijijini hapo limekuwa kubwa kutokana na matukio ya baadhi ya wenye nyumba kuhofia kuishi ndani ya nyumba zao kwa hofu ya kupigwa makofi na watu kimiujiza.

"Yapo mambo mengi, unaweza kulima shamba ekari 50 kisha ukavuna magunia matatano lakini yule anayelima ekari mbili anavuna magunia 100. Je, siyo mambo ya kishirikina hayo," alihoji Magawa.

Naye Leornard Luganje alisema,

"Tunaomba wananchi tuache tufanye haya mambo ya jadi ili kujiokoa hapa kijijini, maana wengi tumefungwa kimiujiza. Pamoja na serikali kutoamini haya mambo, tunaomba tuachwe tusisumbuliwe," alisema mwananchi mwingine, Leonard Luganje.

Ernest Mganga ambaye ni mzee wa kijiji hicho, alisema wananchi wa Seluka wameonewa kwa miaka mingi kishirikina na kunyonywa sana mali zao lakini kwa sasa wanataka kijiji kisafishwe ili wananchi waishi kwa amani.

Miongoni mwa matukio hayo ambayo wananchi wa kijiji cha Seluka wamekutana nayo kimiujiza ni pamoja na watu kupigwa au kufanyishwakazi kimiujiza.

Mzazi wa mtoto Rida (9), Frank Ernest, alisema binti yake alipigwa ndani ya nyumba kimiujiza baada ya kimbunga kuingia na kumsababishia maumivu makali na baadaye wote kuhama nyumba hiyo kabla ya mganga kwenda 'kurekebisha'.

Mwenyekti wa kijiji, Kenneth Magayo, alisema kikao hicho ni halali na wananchi wamekubaliana kwa kauli moja mganga huyo wa tiba asili aendelee kuwepo na kufanya kazi zake na kutoingilia na mtu.

"Kuna watu wanakosesha amani kijiji. Hali hii hatutokubali iendelee kuwapo. Kijiji hiki inasemekana ni cha kichawi kutokana na kufungwa kimaendeleo na hapa hatahongwa mtu na anayetoa rushwa ili mganga tiba aondoke mkamateni huyo," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya mganga huyo, mwanasheria wa kampuni ya Njulumi Advocate & Company, Geofrey Kajigili, aliwataka wananchi hao wawe na nia moja kama mganga abaki au aondoke.

"Nipo kama mwanasheria wake kwa chochote ambacho kitamtokea ama nyie kitawatokea, nitawasimamia haki zenu ili ipatikane," alisema Wakili Kajigili.



Wafanyakazi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wakizoa taka zilizojaa kwenye dampo lililoko stendi na soko la Sabasaba jana, huku wengine wakiwa hawana vifaa vya kujikinga mikononi kitendo ambacho ni hatari kwa afya zao. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Katibu mkuu aeleza dhamira ya serikali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAIMU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Gilbert Moga, amesema serikali kupitia mpango wa maendeleo awamu ya tatu wa miaka mitano 2021/22 hadi 25/26 imekusudia kujenga uchumi shindani wenye kutoa huduma bora kwa jamii na kuwaletea maendeleo Watanzania.

Moga alibainisha hayo jana jijini hapo wakati akifungua semina ya fedha, utawala bora na uwajibikaji kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA).

Alisema serikali imekusudia kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha miundombinu ikiwamo ya usafiri, upatikanaji wa nishati, kuendelea kuimarisha mazingira ya ufanyajibiashara na uwekezaji ili kuwezesha ushindani wa sekta binafsi. "Mwaka 2022/23, Sh. trilioni 2.99 zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika halmashauri. Natoa wito kuhakikisha fedha hizi zinasimamiwa ipasavyo na kuhakikisha thamani ya fedha inaonekana na miradi inakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa," alisisitiza Moga.

Pia alisema serikali imeimarisha ukaguzi hali ambayo itapunguza upotevu wa mapato na kuongeza usimamizi madhubuti katika kusimamia fedha za miradi hasa zinazopelekwa katika mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema Ofisi ya Rais, TAMISEMI iko tayari kutoa ushirikiano kwa TAA katika masuala ya kifedha na maeneo mengine ambayo yatasaidia kuhakikisha wataalamu wetu wanajengewa uwezo kulingana na mabadiliko ya teknolojia.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Serikali za Mitaa Upande wa Fedha, Ummy Wayayu, aliwataka wataalamu hao kuhakikisha wanatumia mafunzo waliyopata kuongeza tija na kuleta matokea chanya katika serikali za mitaa.

Naye Rais wa Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA), CPA Peter Mwambija, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara. Aliiomba serikali kuendelea kuweka udhibiti kwa kuziba mianya ya upotevu wa fedha katika mamlaka za serikali za mitaa.

## Madereva wapewa somo kuhusu ajali barabarani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, amesema miongoni mwa sababu zinazochangia ajali kwa madereva wa serikali ni uchovu na kuwashauri kuwa wa kweli kwa wanaowaendesha ili wapumzike.

Takwimu za kikosi cha usalama barabarani nchini zinaonesha kati ya mwezi Januari hadi Agosti, mwaka huu, zilitokea ajali za barabarani 1,177 ambapo kati yake 135 sawa na asilimia 11.5 ni za magari ya serikali.

Akifungua kongamano la siku tatu la Chama cha Madereva wa Serikali Tanzania, jijini hapo juzi, Naibu Waziri huyo alisema madereva hao wanapaswa kuongeza umakini kwenye utekelezaji wa majukumu yao ili kuondokana na ajali ambazo zinachangia uharibifu wa magari na vifo.

"Madereva wa serikali ni kada inayoheshimika ni vyema kuwa makini ili kuondokana na ajali za barabarani. Kumekuwa na sababu kadhaa ambazo zinachangia ajali kwa madereva ikiwa ni pamoja na uchovu, muwe wa kweli na kuwashauri watu wanaowaendesha kupumzika pindi mnapojiona mmechoka," alisema.

Pamoja na hayo, aliwaonya matumizi ya vilevi vya aina yoyote wanapotekeleza wajibu wao.

"Zingatie sheria za usalama barabarani na kuondokana na vitendo vya uovu na matumizi mabaya ya magari ya serikali na taasisi mbalimbali," alisema.

Mwakibete aliwataka waajiri kutoa fursa ya ajira kwa madereva wanawake ili kuongeza idadi yao kwa sababu kwa sasa madereva wa serikali waliopo ni 5,973 madereva wanawake ni 41 pekee.

Akisoma risala ya chama hicho, mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya mkutano, Saidi Kapande, aliomba serikali kutoa mwongozo utakaosaidia kupunguza safari za usiku ili kupunguza tatizo la ajali.

Kadhalika, alisema kuangalia namna ya kuwalipa pensheni madereva waliostaafu kabla ya kupitisha muundo mpya wa utumishi kwa madereva kwa kuwa mbali ya pensheni pia wamekosa bima za afya.

"Waliostaafu kabla ya kupitisha muundo mpya mwaka 2007 na humu wamo madereva ambao wamewahi kuwaendesha marais na viongozi wakubwa wa nchi hii," alisema.

Pia aliomba serikali ipitie upya Sheria ya Ununuzi ambayo imekuwa ikichangia gharama kubwa ya matengenezo ya magari ya serikali.

## Sheria ya wenye ulemavu yazidi kuwabana wabaguzi, wanaowaficha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MUSWADA wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2022, umependekeza kutiwa hatiani atakayebainika kumficha au kumbagua mwenye ulemavu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, alitoa ufafanuzi huo jana wakati akiwasilisha muswada huo unaolenga kuimarisha haki za watu wenye ulemavu pamoja na fursa zao kwa mujibu wa katiba.

Alisema kwa sheria hiyo atakayemficha mwenye ulemavu ikiwamo mtoto na kumkosesha haki ya msingi kama elimu akikutwa na hatia atalipa faini isiyopungua Sh. 50,000 na isiyozidi 500,000.

Aidha, alisema atakayembagua mtu mwenye ulemavu kutokana na ulemavu wake atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Sh.milioni moja na isiyozidi Sh.milioni 5.

Kwa mujibu wa Suleiman, muswada huo umelenga kuhakikisha haki za watu wenye ulemavu zinalindwa na kutekelezwa kwa vitendo kwa mujibu wa sheria za nchi, mikataba ya kimataifa na kikanda.

Alisema muswada huo umeweka kipaumbele zaidi kwenye masuala ya ajira na kwamba wapo watu wa kundi hilo wanatakiwa kuajiriwa kwenye taasisi za serikali na sekta binafsi kwa mujibu wa uwezo na sifa zao.

Waziri huyo alisema muswada huo atakayekataa kumwajiri mwenye ulemavu kutokana na ulemavu wake atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopunguwa Sh.milioni 3 na isiyozidi Sh.milioni 5. Alisema walibaini kuna taasisi za watu binafsi hawataki kuwaajiri wenye ulemavu bila sababu za msingi licha ya kwamba wana uwezo mkubwa wa kufanyakazi.

"Muswada wa sheria ya watu wenye ulemavu haki na fursa sasa unakuja fungua fursa na haki kwa kundi la watu wenye ulemavu kuona kwamba wanaajiriwa kulingana na sifa na uwezo," alisema.

Jana Baraza la Wawakilishi lilipitisha muswada huo wa sheria ya kufuta sheria ya watu wenye ulemavu haki na fursa namba 6 wa mwaka 2006 na kuweka masharti yanayohusiana na watu wenye ulemavu kwa mwaka 2023.

# NGO zamkosha Dk. Mwinyi kuboresha huduma za jamii

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali inafarijika kuona taasisi zisizo za kiserikali zinasaidia kuimarisha huduma za kijamii ikiwamo afya na elimu.

Alisema hayo jana Ikulu Zanzibar alipozungumza na uongozi wa Taasisi ya 'Mwanamke Intiative Foundation' iliyokwenda kujitambulisha.

Alisema serikali inafarijika inapoona taasisi zisizo za kiserikali zinaunga mkono juhudi zake kwenye masuala mbalimbali ikiwamo uimarishaji wa sekta za elimu, afya, hasa kwa kuzingatia kwamba serikali haiwezi kufanya kila kitu.

Alisema serikali iko tayari kushirikiana na wadau wa elimu kufanikisha dhamira ya kuimarisha sekta hiyo.

Rais Mwinyi alisema kipaumbele kimewekwa katika maeneo matano ambayo ni uimarishaji wa miundombinu kwa kuanzisha ujenzi wa shule mpya, kukarabati shule za na kujenga maabara na maktaba za kisasa.

Kingine ni uimarishaji wa rasilimali watu kwenye kada ya ualimu kwa kuhakikisha kuna walimu wenye kiwango cha elimu cha kutosha hasa kwenye masomo ya sayansi.

Aidha, alisema serikali inatarajia kuongeza nguvu kwenye upatikanaji wa nyenzo mbalimbali ikiwamo madawati na vitabu.

Alitaja kingine ni kuimarisha kwenye tekonolojia ya mawasiliano na habari kwa kuwafundisha wanafunzi katika ngazi mbalimbali ili kwenda sambamba na kasi ya dunia.

Dk. Mwinyi alisema uendelezaji wa sekta ya elimu unategemea bajeti ya serikali kwa asilimia 100 na kwamba wakati mwingine fedha zilizoko hazitoshelezi mahitaji, hali inayowalazimu kutafuta vyanzo vingine.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Elimu iko tayari kukutana na kushirikiana na Taasisi za 'Planet One' ili kuangalia uwezekano wa kusaidia ukuaji wa sekta hiyo pamoja na Taasisi ya 'G.S Group' inayoshughulikia masuala ya ICT.

Aidha, aliishukuru Taasisi ya Mwanamke Initiative Foundation kwa programu iliyoianzisha katika Mkoa wa Kusini Unguja inayolenga kuongeza ufaulu kwa wanafunzi kwenye mitihani yao ya taifa, akisema imeanza kuleta matokeo chanya. Aidha, alitilia mkazo umuhimu wa kuelekeza nguvu katika uimarishaji wa vyuo vya amali, kwa kigezo kuwa kumekuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaoanza katika ngazi za msingi, idadi inayopungua kadri kiwango cha elimu kinavyoongezeka na kuwaacha vijana wengi wakishindwa kutumia fursa mbalimbali katika soko la ajira.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwanamke Initiative Foundation, Wanu Hafidh Ameir, alisema taasisi hiyo inaunga mkono juhudi za serikali katika kuimarisha sekta za afya, elimu na kilimo.

Wakati huo huo, Dk. Mwinyi amezungumza Balozi wa Shirikisho la Somalia nchini Tanzania, aliyekwenda kujitambulisha.Aidha, aliwaomba wawekezaji na wafanyabiashara kuwenda visiwani humo na kuwekeza kwenye sekta mbalimbali ikiwamo uzalishaji wa nyumba za makazi.

Pia Balozi wa Shirikisho la Somalia nchi Tanzania, Zahra Ali Hassan, alishukuru ushirikiano ulioko baina ya nchi hizo na kubainisha azma ya Somalia kwa kuwekeza kwenye miradi mbalimbali na kuimarisha biashara.



Baadhi ya wafanyakazi wa Barrick North Mara, wakiwa na kombe la ushindi wa kwanza kwa mlipa kodi ambalo mgodi ulitunukiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), katika kilele cha wiki ya mlipa kodi iliyomalizika hivi karibuni, lilipowasili mgodini hapo, wilayani Tarime, mkoani Mara jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zanzibar yabainisha chanzo hitilafu umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini imesema inatarajia kufanya matengenezo makubwa kwenye waya wa kusambaza umeme uliolazwa chini ya bahari (Submarine Cable), ili kutibu tatizo la hitilafu ya nishati hiyo inayojitokeza mara kwa mara.

Aidha, wamesema kutokana na kutofanyika matengenezo kumekuwa na hitilafu za mara kwa mara zilizopelekea kupungua nguvu nishati hiyo.

Naibu Waziri Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Shaaban Ali Othman, aliyasema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu, Haji Omari Kheir, aliyetaka kujua ni lini waya huyo utafanyiwa matengenezo kutokana na hitilafu iliyoko.

Mwakilishi huyo alisema Kisiwa cha Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja kimeunganishwa na umeme kutoka Mkokotoni kwa kulaza waya chini ya bahari zaidi ya miaka 10 iliyopita.

Naibu Waziri huyo alisema Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), linataarifa na kwamba wameanza kulishughulikia ili wananchi wasipate usumbufu.


Aidha, alisema ZECO imejipanga katika kipindi cha miaka miwili kuimarisha huduma za nishati ya umeme ikiwamo kuunganisha vijiji vyote na visiwa vidogo vinavyoishi watu.

Alisema katika kisiwa cha Tumbatu wanakusudia kujenga laini nyingine za umeme ili kutosheleza mahitaji wa wananchi.

"Mheshimiwa Spika nataka niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wananchi wa kisiwa cha Tumbatu kwamba tumejipanga kuhakikisha wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo vidogo wanapata huduma ya nishati ya umeme kwa uhakika," alisema.

Aidha, alipiga marufuku wanaojenga makazi ya kudumu jirani na waya wa laini kubwa ili kuepuka athari za mazingira.

Alisema ZECO imefanya uchunguzi na kubaini kuna wananchi wamejenga kwenye maeneo yaliyopigwa marufuku jambo ambalo ni hatari.



# Mbwa 285 wapatiwa chanjo ya kichaa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya mbwa 285 na paka 10 katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamepatiwa chanjo ya kichaa bure ikiwa moja ya harakati za kutokomeza ugonjwa huo katika vijiji na kata zilizoko pembezoni.

Chanjo hiyo imetolewa na shirika lisilo la kiserikali la Ustawi na Haki za Wanyama Tanzania (TAPO) kwa kushirikiana na halmashauri hiyo katika kata za Nyamilango, Kisuke, Bulungwa, Chona na Chambo na kwamba kazi hiyo itakuwa endelevu kila mwaka.

Hata hivyo, idadi ya wanyama hao waliochanjwa ni ndogo kwa sababu wananchi wengi wanashinda katika shughuli za kilimo hali inayosababisha kushindwa kutekeleza huduma hiyo kwa wakati.

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, Yohana Kashililah, akizungumza wakati wa utoaji wa chanjo hiyo jana, alisema huduma hiyo hutolewa na shirika lao bila malipo.

Alisema kwa mwaka huu, wameamua kujikita katika kutoa huduma hiyo kwa maeneo ya pembezoni tofauti na awali walipokuwa wakitoa mijini pekee. Sababu kubwa, alisema ni kutokana na maeneo hayo kuwa na tatizo kubwa la matukio ya watu kung'atwa na mbwa huku wengi wao wakiwa bado hawajapata chanjo.

"Tumeamua kuleta chanjo hii na kutoa elimu ya kichaa cha mbwa Ushetu kwa sababu kuna wafugaji wengi ambao wanaishi na mbwa na paka na hawapatiwi chanjo. Wananchi wanapong'atwa hawafahamu wapi wanatakiwa kwenda kupata kinga ya kichaa hicho tofauti na wale wa mjini," alisema Kashililah.

Bulungwa Masanja, mfugaji kutoka Ushetu alipongeza shirika hilo kwa kutoa chanjo bure. Alisema awali walilazimika kuchangia Sh. 3,000 na halmashauri kwa kila mfugo hali iliyosababisha baadhi ya wafugaji wasiokuwa na uwezo kushindwa kuchanja mifugo yao.

Alisema katika halmashauri hiyo, kuna mbwa wengi zaidi ya idadi ya mifugo waliochanjwa kutokana na wengi wao kuwa shambani wakiendelea na kupanda mazao ya chakula na biashara huku wengine wakidhani kuwa huduma hiyo ni ya kulipia.

Naye Ofisa Mifugo wa Kata ya Nyamilango, utaratibu huo umewasaidia kuwaondolea gharama wananchi ya kulipa chanjo hiyo na kati ya kata 20 zilizoko wamezifikia kata tano kwa awamu ya kwanza.



Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Juma Chikoka 'Mchopanga' (kulia), akikabidhiwa zawadi na Ofisa Mwandamizi wa Bima wa Benki ya Maendeleo ya TIB, James Manyama, alipotembelea banda la benki hiyo, kwenye maonyesho ya wiki ya huduma za kifedha kitaifa yanayoendelea jijini Mwanza jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC ataka huduma ya chakula kwa wanafunzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amewaagiza maofisa maendeleo ya jamii pamoja na waratibu elimu Manispaa ya Shinyanga, kuhakikisha wanafunzi wote wa shule za msingi na sekondari waanza kupatiwa chakula shuleni ili kuongeza kiwango cha ufaulu shuleni.

Mboneko alitoa agizo hilo juzi katika kikao cha kamati ya lishe Manispaa ya Shinyanga, kilichokuwa na lengo la kupitia mkataba wa lishe ngazi ya halmashauri ikiwa ni sehemu ya kuboresha kiwango cha elimu kwa wanafunzi wilayani hapo.

Alisema katika kuimarisha masuala ya lishe kwa watoto, wanafunzi walioko shuleni wanapaswa kuweka huduma ya chakula ili kuimarisha afya zao zinazoenda sambamba na afya ya akili.

"Nasisitiza maofisa maendeleo, waratibu wa elimu, shirikianeni kuhakikisha suala la lishe linazingatiwa shuleni, ili watoto waanze kula chakula kuanzia Januari mwakani kwa shule za msingi na sekondari. Wekeni utaratibu mzuri," alisema Mboneko.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Shinyanga, John Tesha, alisema watalitekeleza agizo hilo na kutoa elimu kwa wazazi ikiwa ni pamoja na kupanga utaratibu mzuri namna ya kuanza kutoa chakula kwa wanafunzi shuleni, hasa katika Kata za Chibe, Ndala na Oldshinyanga.

# Waanza kunufaika huduma majisafi na usafi wa mazingira

**Na Vitus Audax,** MAGU

ZAIDI ya wananchi 20,000 kutoka vijiji vya Nsola, Kisamba, Bubinza na Yichobela katika kata za Lubugu na Ichobela, Magu mkoani Mwanza, wameanza kunufaika na miradi ya maji inayotekelezwa na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani hapo.

Wakizungumza na gazeti hii juzi, baadhi ya wananchi hao walisema awali walivyoteseka kupata maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali huku zaidi ya watu wa vijiji hivyo wakielezwa kutafunwa na mamba wakati wakichota maji ziwani.

"Ili kupata maji tulikuwa tunalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilometa sita kwa mguu kwenda ziwani na kuna vipindi tofauti wenzetu walivamiwa, kushambuliwa mpaka kuuawa na mamba walipoenda kuchota maji alfajiri ziwani," alisema Elizabeth Sahani, mkazi wa Bubinza.

Sahani alisema kwa sasa wamepumzika na adha ya upatikanaji wa maji baada ya huduma hiyo kuwafikia mpaka mlangoni kupitia miradi iliyotekelezwa na RUWASA katika vijiji vyao.

Naye Wase Zabron mkazi wa kijiji cha Kisamba, alisema hali ya upatikanaji wa maji katika kijiji hicho ilikuwa ngumu awali kutokana na wanakijiji kuchota maji katika madimbwi yanayotumika kunyweshea mifugo huku maji hayo yakiwa si safi na salama.

"Muda mwingine tulilazimika kuamka usiku kwenda kuchota maji ili ikifika asubuhi tupate nafasi ya kufanya shughuli zetu nyingine za kilimo pamoja na shughuli nyingine za kiuchumi. Hatua hii ilitugombanisha na waume zetu ambao hawakuamini mienendo yetu," alisema Magreth John. Lucas Zabron, Diwani wa Lubugu, aliiambia Nipashe kuwa katika kata yake pamoja na kata jirani, wamefikishiwa maji kutoka miradi ya usambazaji maji iliyotengenezwa na RUWASA kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wananchi hao.

Pia alisema maji hayo wanayapata kwa bili hasa wale waliounganisha kwenye nyumba zao pamoja na wengine ambao wanapata kupitia vituo vya usambazaji wanapolipia kwa wastani wa Sh. 30 kwa ndoo moja.

Kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo wilayani humo Meneja wa RUWASA Wilaya ya Magu, Mhandisi Daudi Amlima, alisema miradi hiyo miwili katika wilaya hiyo imegharimu Sh. bilioni 1.5.

Alisema miradi hiyo tayari inawahudumia wananchi na wameondokana na adha waliyokuwa nayo muda mrefu na sasa wananunua maji kwa ndoo moja kubwa kwa Sh.30 hadi Sh. 50 huku wengine wakifikishiwa nyumbani kwa malipo ya bili ikiwa kwa uniti moja ni Sh.1,500.

HABARI KIMATAIFA

# Raia Ukraine wateseka na baridi

**KYIV,** Ukraine

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky ameishutumu Russia kwa vitendo vya kihalifu dhidi ya binadamu baada ya kufanya mashambulizi mapya ya makombora na kusababisha kukatika kwa umeme nchini kote.

Kiongozi huyo, aliliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kupitia video kwamba mfumo wa ugaidi wa Russia umelazimisha mamilioni ya watu kukaa bila vifaa vya kupashia joto na bila maji katika kipindi cha baridi kilichofikia nyuzi sifuri.

Mashambulizi hayo pia yamesababisha vifo vya watu saba.

Aidha, mitambo mitatu ya Nyuklia ambayo bado iko chini ya udhibiti wa Ukraine ilikosa huduma ya umeme kutoka kwa gridi ya taifa.

**Wakati majira ya baridi yakianza, Russia imeongeza mashambulizi kwenye miundombinu ya nishati.**

Pia mtambo mkubwa zaidi barani Ulaya wa Zaporizhzhia, ulilazimika tena kutegemea jenereta za dizeli kuwezesha mifumo yake ya kupozea vifaa muhimu vya usalama.

Shirika la Kimataifa la Nishati ya Atomiki (IAEA) limeeleza wasiwasi wake kuhusu mtambo wa Zaporizhzhia unaodhibitiwa na Russia, ambao umepata madhara kutokana na kushambuliwa kwa makombora mara kwa mara.

Nchi jirani ya Moldova pia ilikumbwa na kukatika kwa umeme juzi kutokana na nchi hiyo kutegemea nishati hiyo kutoka Ukraine na Russia.

Wakati majira ya baridi yakianza, Russia imeongeza mashambulizi kwenye miundombinu ya nishati.

**RUSSIA YAZUIA HUJUMA**

Idara ya Ujasusi ya Russia (FSB) imesema imezuia idara ya ujasusi ya Ukraine kutekeleza kile ilichosema hujuma kwenye bomba la gesi la South Stream.

Kwa mujibu wa vyanzo vya habari vya Russia, bomba hilo ni mradi uliokusudiwa kusafirisha gesi kupitia Bahari Nyeusi hadi Bulgaria, ingawa baadaye mradi huo ulifutwa kwa niaba ya TurkStream.

Huku haya yakijiri Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Ryabkov ametangaza kwamba nchi yake haina mpango wa kuwasiliana na Marekani na wala haikujaribu kukutana nayo wakati wa mkutano wa nchi zilizoendelea na zinazoinukia kiuchumi za G20 nchini Indonesia.

Ryabkov amedokeza kwamba mawasiliano yoyote kati ya nchi hizo mbili yanafanyika tu kwa njia ya simu na kwa kufuata njia za kidiplomasia na sio ngazi ya urais. **DW**

## Wakubaliana kuwaondoa kwa nguvu waasi wa M23

**LUANDA,** Angola

MKUTANO kuhusu hali ya usalama mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo umemalizika nchini Angola na kuazimia kuondoshwa kwa nguvu waasi wa M23.

Mazungumzo hayo yaliyowakutanisha viongozi wa kikanda, yaliangazia kuzorota hali ya usalama na tishio linaloletwa na waasi wa M23 juu ya uthabiti wa eneo la maziwa makuu.

Mkutano huo uliunga mkono kuendelea kutumwa kwa wanajeshi chini ya jeshi la kikanda na kuharakisha juhudi za kupokonya silaha vikundi vya wanamgambo.

Viongozi kutoka DRC na Rwanda walikutana kwa mara ya kwanza kufuatia mzozo wa kidiplomasia uliosababishwa na mgogoro unaoendelea katika eneo hilo lenye utajiri wa madini.

Mkutano huo wa kilele uliongozwa na Rais wa Angola Joao Laurenco (pichani chini) uliunda ratiba ambayo inatanguliza hatua muhimu ikiwa ni pamoja na kukomesha uhasama, kuwaondoa waasi wa M23 kutoka katika maeneo yanayokaliwa kwa mabavu na kurejea katika nafasi zao za awali.

Waliidhinisha uingiliaji kati wa kijeshi dhidi ya kundi hilo iwapo watashindwa kutii.

Wakuu hao wa nchi walielezea wasiwasi wao juu ya ukosefu wa usalama ulioenea na mashambulizi ya kudumu ya kundi la M23 dhidi ya jeshi la DRC.

Walikubaliana kwamba makundi yote yenye silaha yanayoendesha shughuli katika eneo la DRC yanapaswa kuweka chini silaha zao. **BBC**





Wafanyakazi wa afya wakiwa wamevaa vifaa vya kujikinga (PPE) wakiendesha baiskeli kwa ajili ya kusambaza vipimo vya Covid-19 katika jiji la Beijing nchini China juzi. **PICHA: AFP**

## Panya watafuna kilo 200 za bangi, polisi walihifadhi kama ushahidi

**NEW DELH,** India

POLISI nchini India wamewalaumu panya kwa kuharibu karibu kilo 200 za dawa za kulevya aina ya bangi zilizohifadhiwa baada ya kunaswa kutoka kwa wauzaji.

"Panya ni wanyama wadogo na hawana hofu na polisi. Ni vigumu kulinda dawa dhidi yao," mahakama katika jimbo la Uttar Pradesh ilisema.

Mahakama iliwataka polisi kuwasilisha siri hiyo kama ushahidi katika kesi za ulanguzi wa dawa za kulevya.

Hakimu alizitaja kesi tatu ambazo bangi iliharibiwa na panya.

Jaji Sanjay Chaudhary, alisema baada ya mahakama kuwataka polisi kuwasilisha dawa hiyo iliyokamatwa kama ushahidi, iliambiwa kuwa kilo 195 za bangi ziliharibiwa na panya.

Katika kesi nyingine inayohusu kilo 386 za dawa hiyo, polisi waliwasilisha ripoti wakisema baadhi ya bangi hiyo iliiliwa na panya.

Jaji Chaudhary alisema baadhi ya kilo 700 za bangi zilizokamatwa na polisi zilikuwa zimelazwa katika vituo vya polisi wilayani Mathura na kwamba zote ziko katika hatari ya kuvamiwa na panya.

Alisema polisi hawana utaalamu wa kushughulikia suala hilo kwani panya hao ni wadogo mno.

Njia pekee ya kulinda bidhaa zilizokamatwa kutokana na panya hao wasio na woga ni kuzipiga mnada dawa hizo kwa maabara za utafiti na makampuni ya dawa, huku mapato yakienda kwa serikali.

Hata hivyo, mbunge Singh, ofisa mkuu wa polisi wa wilaya ya Mathura, aliwaambia waandishi wa habari kwamba baadhi ya mirungi iliyohifadhiwa katika vituo vya polisi vilivyo karibu na hapo imeharibiwa na mvua na sio panya.

Mwaka 2018, maofisa wanane wa polisi wa Argentina walifutwa kazi baada ya kuwalaumu panya kwa kutoweka kwa nusu tani ya bangi kutoka ghala la polisi.

Baadhi ya wataalamu walipinga madai hayo wakisema kwamba wanyama hao hawakuweza kuchanganya dawa hiyo kama chakula na kama kundi kubwa la panya wangekula, mizoga mingi ingepatikana kwenye ghala hilo.

Utafiti uliochapishwa mnamo 2019 uligundua kuwa panya wa maabara walipopewa unga uliotiwa bangi, walizoea kufanya kazi kidogo na joto la mwili wao pia lilipungua.

Mwaka wa 2017, katika jimbo la mashariki la Bihar polisi waliwatupia lawama panya kwa kunywa maelfu ya lita za pombe iliyochukuliwa, mwaka mmoja baada ya serikali kupiga marufuku uuzaji na unywaji wa pombe. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**CAROLINE KAHUMBYA BISHAIJA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0239-0016** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST. FRANCIS GIRLS' SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CHU/RB/453095/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARY JACKSON MALEKO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S0266/0027** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **REGINAMUNDI GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2002. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/454924/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **ADELTUS MWEMEZI AUDAX** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya pikipiki yenye chassis Na. **LTBPK8BG6K2K03514,** injini Na. **KL162FMJ19J03514** na namba za usajili **MC 701 CHB.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/MUL/RB/452130/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochte cha polisi au apige simu namba **0784681834**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ZAINABU TAKI HASSANALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya Honda yenye namba za usajili **T203AAF** Chasis namba **MD031013808** na Engine namba **MD03E1013860** Kwa yeyote atakayeiona au kuiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAN/BAB/RB/435581/2022**

**MWAMBA MILLENIUM COMPANY LIMITED**

## MNADA WA HADHARA
**Shauri la ndoa No.10/2022**

KWA AMRI YA MAHAKAMA YA MWANZO MAKOLE WILAYA YA DODOMA MJINI TUTAENDESHA MNADA WA HADHARA WA KUUZA NYUMBA PLOT NO. 1, ILIYOPO NUNDULU – IHUMWA MALI YA JOSEPH PAUL GYOLY, MARRY KAVINDI NDANI YA SIKU 21 MGAWANYO WA TALAKA. MNADA UTAFANYIKA TAREHE 14.12.2022 SAA TANO KAMILI ASUBUHI (05:00) HUU MNADA UTAFANYIKA KATIKA KIJIJI CHA NUNDULU – IHUMWA. NYUMBA SAFI YA KISASA.

**MASHARTI YA MNADA**
1. UKAGUZI UNARUHUSIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALIPA 25% NA ATAMALIZIA NDANI YA SIKU 14 MALIPO 75% YA BEI ITAYOWEKWA KWENYE MNADA.
3. ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPA SALIO KWA MUDA ULIOTOLEWA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE
4. KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA SIMU NAMBA **0712245977, 0784 155 866, 0654 686 106, 0767 245 977.**

**WOTE MNAKARIBISHWA**

Pastory H. Kaboya
Mkurugenzi Mtendaji

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA DODOMA LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI NA. 129 YA mwaka 2022**

**THE REGISTERED TRUSTEES OF TANZANIA ASSEMBLIES OF GOD (TAG)..........MDAI**

**VERSUS**

**ISAYA NGAHYA..........MDAIWA 1**
**RITA KOMBA..........MDAIWA 2**
**HUSSEIN SHABANI..........MDAIWA 3**
**ESTA MBATA..........MDAIWA 4**
**SEMENI HENRY MPABANDI..........MDAIWA 5**
**DEOGRATIUS NICHOLOUS LUHUMNYA..........MDAIWA 6**
**THE REGISTERED TRUSTEES OF MENNONITES CHURCH..........MDAIWA 7**

**KWA:**
**ISAYA NGAHYA, RITA KOMBA, HUSSEIN SHABANI, ESTA MBATA, SEMENI HENRY MPABANDI, DEOGRATIUS NICHOLOUS LUHUMNYA, THE REGISTERED TRUSTEES OF MENNONITES CHURCH.**

**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 08.12.2022 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 23 ya mwezi wa Novemba,2022.

MWENYEKITI
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya
DODOMA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**Wilaya ya Morogoro, Mkoa Wa Morogoro**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 52 YA 2021**

**KIBAGA G. MWAIPAJA..........MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**CHRISTOPHER SILVESTER..........MJIBU MAOMBI**
**DEODATUS KITUY..........MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA DEODATUS KITUY**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza za Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 12/12/2022 mbele ya mwenyekiti M .KHASIM wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilzwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 23 Mwezi November 2022.

M. KHASIM
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU ABDALLAH JUMA MUHENGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC419CJP** aina ya **BOXER BM150** Rangi Nyekundu yenye Chasis No. **MD2A21BY2KWE94205,** Engine No. **PFZWKE18129** yenye jina la **MOHAMMED ENTEPRISES (T) LTD.**Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **DOD/DOD/RB/454045/2022**

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Diamond awataja Kiba, Harmonize

DIAMOND Platnumz kupitia akaunti yake ya Instagram amekiri wasanii wenzake wakiwamo Ali Kiba, Harmonize na Rayvanny ni wasanii wakali.

Diamond alisema jambo linalowazuia wasanii wa Tanzania kuvuma hata kwa nchi za nje ni mazoea ya kushindana badala ya kuwa na umoja.

Alieleza wasanii wanafaa kuwa na malengo ya kusonga mbele wala si kubaki mahali pamoja wakizozana.

"Huku Tanzania tuna tabia ya kuonyeshana nani mkali kuliko mwenzake, mpaka leo hamjafahamu kuwa nyote ni wakali tu? Hivi leo, nani asiyejua kuwa Ali Kiba ni msanii mkali, nani asiyejua Rayvanny ni msanii mkali, nani asiyejua Harmonize ni msanii mkali? Hivyo tushavipitisha vyote," alisema Diamond.

Aliongeza hapendi kujihusisha na kitu ambacho watu wanazungumza kumhusu kwani anaweza kuwa mwenye mawazo na kujibu kwa madharau, jambo ambalo anafahamu litampotezea wakati.

Alilinganisha wasanii wa Tanzania na wa nje kama Marekani na kusema wasanii wa nchi yake wakizozana wale wa nchi za nje wanasonga na kuimarika kimuziki.





"Wasanii huongozwa na watu, marafiki, jamaa, lazima watuongoze kwenye njia ya kusonga mbele wala si chuki za wenyewe kwa wenyewe, kwa sababu zinaturudisha nyuma."



# MIMI MARS AMKATAA MARIOO



MSANII wa Bongofleva, Mimi Mars amesema Marioo sio mpenzi wake na haitaweza kutokea.

Akizungumza na wanahabari akiwa mkoani Morogoro kwenye Tamasha la Mziki Mnene, Mars alisema Marioo sio mpenzi wake.

Mbali na hilo amezungumzia tattoo zake ambazo amesema zipo nyingi na ni kitu anachopenda ila kwa imani ya dini yake hairuhusu.

Lakini anatamani kuacha kuchora tattoo ila ni kitu anachopenda.

# *Akothee amfichua aliyemtusi mitandaoni*

**NAIROBI,** Kenya

MWANAMUZIKI na gwiji wa mitandao ya kijamii, Akothee amemfichua mwanamke anayemtukana mtandaoni mara kwa mara.

Akizungumza na mwanamke fulani ambaye amekuwa akimtusi na kumwamuru aondoke kwenye ukurasa wake.

"Habari za mchana binti natumai u mzima, ningeweza kukuita binti yangu kwa vile unaonekana kama 18 hadi 22.

"Niruhusu nikuombe uondoke kwenye ukurasa huu na ufuatilie binti ambao ni wenzako, ukurasa huu ni wa wanawake waliokomaa kabisa na sio watoto wachanga kama wewe, hautaelewa kitu."

Alimwambia mwanamke huyo ajiepushe na mitandao yake ya kijamii kwa sababu hajui ni nini kimemfanya kuwa katika mahusiano mengi.



# POLISI TANZANIA YAANZA TAMBO IKIWAALIKA SIMBA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Polisi Tanzania umetambulisha kampeni yake mpya ya 'Lazima Utoe Ushirika' katika michezo yao ya Ligi Kuu Bara watakayochezea kwenye Uwanja wa Ushirika ulioko Moshi mkoani, Kilimanjaro na wataanza kuitekeleza pale watakapoikaribisha Simba kutoka Dar es Salaam, imefahamika.

Maafande hao wataikaribisha Simba katika mechi ya raundi ya 13 ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa keshokutwa kuanzia saa 10:00 jioni.

Polisi Tanzania wanashuka katika dimba la nyumbani kwao Ushirika kwa mara ya kwanza msimu huu baada ya uwanja huo uliokuwa unakarabatiwa kupata ruhusa kutoka kwenye mamlaka husika inayosimamia Ligi Kuu.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Polisi Tanzania, Hassan Juma, alisema ingawa timu yao msimu huu imekuwa na 'mwendo wa kinyonga', sasa wanarudi nyumbani na wataitumia vyema kampeni ya "Lazima Utoe Ushirika" kwa kuvuna pointi zote tatu.**

Juma alisema wanaanza rasmi ukurasa mpya ndani ya uwanja wao wa asili na wanaimani Wekundu wa Msimbazi hawataondoka na pointi hata moja.

"Japo tuna mwendo wa kinyonga, sasa tunarudi nyumbani, tunarudi nyumbani kwa mashabiki wetu, tumecheza viwanja sita tofauti, sasa tunarudi Ushirika uwanja ambao tunapata matokeo, tuna matumaini makubwa ya kuitekeleza kampeni yetu," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kampeni hiyo sio kwa ajili ya mechi moja bali wataiendeleza katika kila mechi watakayocheza kwenye dimba la Ushirika.

Baada ya kucheza na Simba, Polisi Tanzania itabakiwa kwenye uwanja huo na kusubiri kuwakaribisha Azam FC katika mechi nyingine ya ligi hiyo itakayofanyika Desemba 6, mwaka huu.




Mkurugenzi wa Global Peace Foundation, Martha Nghambi (aliyesimama), akizungumza wakati wa kufunga semina iliyoandaliwa na taasisi hiyo kwa waandishi wa habari za michezo ili kuhamasisha kuondoa mitazamo hasi kwa jamii kuhusiana na soka wanawake hapa nchini iliyofanyika jijini, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Manula, Ayoub Lyanga rekodi safi

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikitimiza raundi ya 13, winga wa Azam FC, Ayoub Lyanga ndiye anayeongoza kwa kutoa pasi nyingi za mabao akiwa na 'assist' sita huku kipa wa Simba, Aishi Manula ndiye mlinda mlango mwenye 'clean sheet' nyingi, imefahamika.

Manula ambaye juzi aliruhusu bao moja katika sare ya goli 101, ana jumla ya 'clean sheets' nane mpaka sasa.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, mchezaji anayeshika nafasi ya pili kwa kutoa pasi nyingi zilizozaa mabao ni Sixtus Sabilo kutoka Mbeya City ambaye pia anakamata nafasi ya pili kwenye ufungaji bora akiwa na mabao saba chini ya Fiston Mayele anayeongoza kwenye orodha ya wafungaji bora kwa mabao yake nane kibindoni.



Manula



Lyanga

Sabilo ana 'assist' tano mpaka sasa, na wanaoshika nafasi ya tatu ni Clatous Chama, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' wote wa Simba na Saido Ntibazonkiza wa Geita Gold ambao wote wao wametoa pasi za mwisho nne.

Kwa upande wa makipa, Manula amecheza mechi nane mpaka sasa bila kuruhusu wavu wake kuguswa, akifuatiwa na Ali Ahmada wa Azam FC akiwa na 'clean sheets' sita, huku Mcomoro mwenzake Mahamoud Mroivili wa Coastal Union akiwa na tano.

Makipa ambao wana 'clean sheets' nne mpaka sasa kwenye Ligi Kuu ni Djigui Diarra wa Yanga, Jonathan Nahimana wa Namungo, Metacha Mnata wa Singida Big Stars, na Said Kipao wa Kagera Sugar.

## Wachezaji watakiwa kutumia lishe, tiba sahihi

**Na Saada Akida**

MKURUGENZI wa Idara ya Maendeleo ya Michezo katika Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo nchini, Ally Mayai, amewataka walimu wa michezo kuwa mabalozi wa kutoa elimu kuhusiana na matumizi sahihi ya chakula na hasara ya utumiaji wa dawa za kusisimua miili kwa wachezaji.

Akifungua semina ya makocha wa michezo mbalimbali inayohusu mafunzo utaalamu wa tiba, lishe na mbinu haramu za dawa za kusisimua mwili michezoni, Mayai alisema mpira wa miguu ni sayansi na mchezaji anahitaji aandaliwe vyema kuanzia lishe, tiba pamoja na kupiga vita matumizi ya kutumia dawa hatarishi.

Mayai aliwataka walimu hao kutumia vyema mafunzo hayo kwa kuwaanda wachezaji wa baadaye na kuepukana na matumizi ya dawa hizo.

"Wachezaji wamekuwa hawafahamu juu ya lishe, tiba ambayo anatakiwa kupata lakini pia kupiga vita hili suala la dawa haramu za kusisimua mwili kwa sababu italeta athari kubwa hapo baadaye," alisema bosi huyo.

## Ceasiaa Queens yaanza mikwara

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Ceasiaa Queens ambayo itacheza Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania kwa mara ya kwanza msimu huu, imetamba inautaka ubingwa wa ligi hiyo ikiamini imefanya usajili mzuri utakaosaidia kutimiza malengo yao.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Ceasiaa Queens yenye maskani yake Iringa, Jumanne Mwanyiro, amesema timu yao imejiandaa vyema kuonyesha ushindani kutokana na kufanya mazoezi kwa muda wa miezi mitatu.

Mwanyiro pia ameliomba Shirikisho la Soka Nchini (TFF) kuongeza idadi ya timu kwenye ligi hiyo inayotarajiwa kutimua vumbi kuanzia Desemba 6, mwaka huu kwa mabingwa watetezi, Simba Queens kuvaana na JKT Queens kwenye Uwanja wa Mo Arena.

"Ligi itachezwa kwa kipindi kifupi sana, tunataka timu nyingi ichezwe msimu mzima, mchezaji anajengeka kwa kucheza mechi nyingi siyo chache, hivyo naamini watalifanyia kazi hili, tunataka timu ikichukua ubingwa iwe imetoka jasho," alisema Mwanyiro.

Ceasiaa Queens yenyewe itaanza kampeni ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Desemba 7, mwaka huu kwa kuwafuata Alliance Girls kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mwanza.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DEPAY KUREJESHWA UNITED

KLABU ya Manchester United itajaribu katika dirisha la usajili la Januari kumrejesha mshambuliaji wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay, 28, ambapo aliondoka mwaka wa 2017. ***(Sport)***

### YAMKATAA RONALDO

NEWCASTLE United haina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo, 37, baada ya kuondoka Manchester United. ***(Football Insider)***

### CHELSEA : RONALDO HAPANA

KLABU ya Chelsea haina uwezekano wa kumnunua nahodha na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo kwa sasa ambaye ni mchezaji huru, licha ya kuwa na nia ya kumsajili hapo awali. ***(Sun)***

### UNITED KUJAZA NAFASI

KLABU ya Manchester United inajadili iwapo itamleta mbadala wa Cristiano Ronaldo Januari au wasubiri hadi msimu wa joto na kufanya usajili wa mkopo wa muda mfupi, kama walivyofanya walipomsajili mshambuliaji wa Nigeria, Odion Ighalo, mwaka 2020. ***(Mail).***

### USAJILI KUVUTIA WANUNUZI

MANCHESTER United inaamini mashabiki wengi wa kimataifa kutawavutia wanunuzi wa Liverpool kwenda Old Trafford. ***(Watch)***

### LAIMER KUBAKIA BAYERN

KLABU za Chelsea na Liverpool zinatazamiwa kumkosa mchezaji anayesakwa katika uhamisho wa Januari, Konrad Laimer, 25, huku kiungo huyo wa kati wa RB Leipzig na Austria akitaka kujiunga na Bayern Munich mkataba wake utakapokamilika msimu wa joto. ***(Bild, via Express)***

### KATALAERE ATAJWA LEEDS

LEEDS United imewasiliana na AC Milan wakiomba kufahamishwa kuhusu hali ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Charles de Ketelaere, 21. ***(TeamTalk)***

### RICE KUONDOKA WEST

KLABU ya West Ham inatarajia kumpoteza kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Declan Rice, 23. ***(Football Insider)***

### ASENSIO: SIONDOKI MADRID

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Hispania, Marco Asensio, 26, amesema anataka kusalia Real Madrid, licha ya mkataba wake kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Redio Marca)***

### BARCA KUFANYA USAJILI

BARCELONA wamemwambia Kocha Mkuu wa timu hiyo, Xavi wanaweza kufanya usajili mpya katika dirisha dogo la Januari iwapo baadhi ya wachezaji wataondoka kwanza. ***(Marca)***

### THURAM KUTUA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid inataka kumsajili mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach, Marcus Thuram, 25. ***(AS, via Mundo Deportivo)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MULLER: UJERUMANI ILISTAHILI KUFUNGWA

**●●● Sasa yaelekeza nguvu kuikabili Hispania keshokutwa ili...**

**DOHA,** Qatar

THOMAS Muller alielezea kufungwa kwa Ujerumani katika Kombe la Dunia na Japan kama "ujinga", lakini akakiri timu yao ilistahili kupoteza mchezo huo.

**Ujerumani walionekana kuanza vyema kampeni zao za Kundi E wakati Ilkay Gundogan alipowaweka mbele siku ya Jumatano, lakini ujio wa ajabu kutoka kwa Japan uliwashangaza washindi hao mara nne wa Kombe la Dunia.**

Wachezaji wawili wanaocheza Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga, Ritsu Doan na Takuma Asano, walitokea benchi na kufunga mabao katika ushindi maarufu wa Samurai hao wa Bluu, na kuwaacha Ujerumani kwenye presha kubwa kabla ya mechi ya Jumapili watakapovaana na Hispania.

Hii ni mara ya pili kwa Ujerumani kupoteza mechi ya kwanza katika michuano ya Kombe la Dunia baada ya kufanya hivyo mwaka 2018.

Akizungumza na ARD Muller alisema: "Kwa upande wa hisia, tulicheza mchezo mzuri kwa muda mrefu.

"Kwa kweli, mchezo mzuri katika soka pia unajulikana na ukweli unabadilisha nafasi na ubora kuwa mabao.

"Ufanisi katika ncha zote mbili haukulingana. Ni ujinga tulifungwa.

"Lakini mwisho wa siku, unapoona kile tunachoacha nyuma yetu na jinsi tulivyoruhusu mabao mwishoni, unaweza kuona tulistahili kupoteza."

Nahodha wa Ujerumani, Manuel Neuer, kwa upande wake, alilalamikia kitendo cha timu hiyo kuanza taratibu hadi kipindi cha pili katika mahojiano yake baada ya mechi.

"Nimechanganyikiwa na kukasirika kwamba tuliacha mchezo," Neuer alisema. "Hiyo ilikuwa zaidi ya ulazima. Tulitengeneza nafasi nyingi za kufunga, kwa hivyo bahati mbaya na mbaya huenda pamoja.

"Lazima tuliyotaka kufunga bao la pili ilikosekana na tukairudisha Japan kwenye mchezo."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,053,2
MECHI KALI
ENGLAND
VERSUS
USA
1 | 1.62
X | 3.90
2 | 5.14
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DE BRUYNE ASHANGAA MCHEZAJI BORA



**DOHA,** Qatar

KEVIN De Bruyne alitangazwa Mchezaji Bora wa mechi katika ushindi wa bao 1-0 ambao Ubelgiji waliupata dhidi ya Canada katika mechi yao ya kwanza ya Kombe la Dunia iliyochezwa juzi, lakini hajui uhakika kwa nini yeye.

Ubelgiji walikuwa na kiwango bora kwa sehemu kubwa ya mchezo huo wa Kundi F kwenye Uwanja wa Ahmad Bin Ali, huku Thibaut Courtois akilazimika kuokoa penalti kutoka kwa Alphonso Davies kabla ya Michy Batshuayi kufunga bao la ushindi.

De Bruyne ambaye kiwango chake kilikuwa cha kawaida alishangaa kama mtu yeyote kwa nini alipewa tuzo ya mchezaji bora wa mechi.

"Sidhani kama nilicheza mchezo mzuri, sijui kwa nini nilipata tuzo - labda kwa sababu ya jina langu," alisema katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Hatukucheza vizuri kama timu, haswa katika kipindi cha kwanza.

"Tulianza vibaya sana, kasi ilikuwa na Canada na nadhani kulikuwa na nafasi zaidi kuliko tulivyofikiria. "Sidhani kama tulicheza mchezo mzuri, nikiwamo mimi, lakini tulishinda."

De Bruyne alikamilisha pasi 23 tu kati ya 33 (asilimia 70), ingawa bado alitengeneza nafasi nne, tatu zaidi ya mchezaji yeyote.

"Nilipoona jinsi tulivyocheza nilidhani tunacheza kwa muda mrefu sana, kulikuwa na nafasi zaidi," aliongeza.



## Enrique amtabiria neema Gavi

**DOHA,** Qatar

LUIS Enrique anaamini Gavi atakuwa mmoja wa "mastaa wa soka" baada ya kijana huyo kufunga bao lake la kwanza la Kombe la Dunia kwa Hispania ilipoizaba Costa Rica magoli 7-0 hapo juzi.

Gavi alifunga bao la tano katika pambano la upande mmoja, akimalizia pasi ya Alvaro Morata na kupiga shuti nje ya lango la kulia zikiwa zimesalia dakika 16.

Akiwa na umri wa miaka 18 na siku 110, ilimfanya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufunga katika Kombe la Dunia kwa taifa lolote tangu Pele (miaka 17 na siku 249) akiwa na Brazil katika fainali ya mwaka 1958 dhidi ya Sweden.

Katika mkutano na waandishi wa habari baada ya ushindi huo wa Kundi E, Enrique aliul zwa jinsi kiungo huyo w Barcelona anavyowez kuwa mzuri.

"Yeye ni wa kipeke tofauti sana kwa sabab ana miaka 18 sasa, lakin ana tabia ya mcheza mwenye uzoefu. Ni furah kumchezesha kijana, kw sababu ni mvulana. Anal itaji utulivu kidogo waka mwingine lakini tunafur hi sana kuwa naye katik timu."

232,366/-

# MANDONGA KUMSINDIKIZA KIDUKU ULINGONI MOROGORO

**Na Sabato Kasika**

BONDIA aliyejizolea umaarufu nchini, Karim Mandonga ambaye sasa anatamba na staili ya ngumi aliyoibatiza jina la 'ndoige', anatarajia kupanda ulingoni katika jukwaa moja pamoja na Twaha Kiduku atakayepigana na Damian Bonell kutoka nchini Argentina kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani, Morogoro.

Ofisa Uhusiano wa Kampuni ya Mo Geen International, ambayo imeandaa pambano hilo, Kessa Mwambeleko, aliliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana kuwa maandalizi yamekamilika na anatarajia wadau wa ngumi watapata burudani safi.

"Baadhi ya mapambano ya utangulizi yatakuwa ni kati ya Mandonga ambaye atavaana na Said Mbelwa, Dulla Mbabe atapigana na Mbiya Kanku kutoka Congo (DRC)," alisema Mwambeleko.

**Mratibu huyo aliongeza tayari mpinzani wa Kiduku, Bonell aliwasili nchini tangu juzi na alishatua Morogoro.**

"Tunawaalika wapenzi wa mchezo wa ngumi kuja kushuhudia burudani nzuri kutoka kwa mabondia mbalimbali watakaopanda ulingoni kesho (leo), lakini pia kutakuwa na burudani ya muziki wa dansi," Mwambeleko alisema.

Alitaja bendi mbili za muziki wa dansi zitakazotoa burudani ni Waluguru Original na Town Class, ambayo ilifanya onyesho lake la kwanza la kujitambulisha, jijini hapa mwezi uliopita.

Aliongeza uongozi wa kampuni hiyo pamoja na kujishughulisha na masuala ya kilimo, itaendelea kujikita kwenye burudani ili kuwapa nafasi vijana wa Kitanzania kuendeleza na kutambulisha vipaji vyao.

## Mgunda awaambia

INATOKA UKURASA 32

"Unapopata sare na timu kubwa kama Simba ni jambo la kushukuru, unapopata sare huwezi kuhuzunika, tulipanga kushinda mechi hii lakini kilichotokea ni kwamba wenzetu walianza kupata bao kwa hiyo tulipambana ili kurudisha.

Kwanza niwashukuru wachezaji wetu walifuata maelekezo. Tulianza kwa kukaa nyuma kwanza, unapocheza na Simba huwezi kuanza kufunguka, unatakiwa uwaangalie ni wapi wana nguvu, wapi na wapi wana udhaifu, tulipohakikisha tumewakamata kwenye udhaifu wao ndiyo tukafunguka na kuwashambulia," alisema kocha huyo.

Aliongeza wanatarajia kuendelea kujipanga kusaka pointi katika mechi zinazofuata kwa sababu wamepata sare nne mfululizo kwenye uwanja wa nyumbani.

Naye mfungaji wa bao la kusawazisha la Mbeya City, Tariq Seif, aliliambia gazeti hili hajafurahi kufunga bao dhidi ya Simba, bali huwa anafurahi akifunga goli na timu yake kuondoka na ushindi.

"Kwanza sijafurahi sana kwa sababu hatukushinda, tulihitaji tushinde kwani si vizuri kupata sare kwenye mechi za nyumbani mfululizo," alisema nyota huyo na kueleza aina ya ushangiliaji aliyoionyesha ameiga kutoka kwa mchezaji anayemhusudu, Mario Balotelli, nyota wa zamani wa Inter Milan, AC Milan, Liverpool, Manchester City na Timu ya Taifa ya Italia.

MSHINDI...




Mshindi wa Jackpot bonus, Bethuel Laurent (38) kutoka Morogoro akishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 6.7 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita. Supa Jackpot kwa wiki hii ni Sh. bilioni 1.05. **PICHA: MPIGAPICHA**

## *Yanga: Hakuna atakayepona*

INATOKA UKURASA 32

tunahitaji kumfurahisha kila shabiki wa timu yetu," aliongeza kocha huyo.

Tayari kikosi kimesharejea Dar es Salaam na kinaendelea na mazoezi yake kwenye Uwanja wa Gymkana huku kikitarajia kuingia kambini kesho kwa ajili ya kujiandaa kuwakaribisha Mbeya City kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa hapo kesho.

Yanga ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 29, sawa na Azam FC lakini ikicheza mechi mbili pungufu, watani zao, Simba wako katika nafasi ya tatu wakiwa na pointi 28 kibindoni.

Wakati huo huo, Geita Gold FC inatarajia kuwakaribisha Ihefu SC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Nyankumbu iliyoko mkoani Geita.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/11/22 | 18:00 | Walsall FC vs Carlisle United | 2.28 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/11/22 | 18:00 | AFC Wimbledon vs Chesterfield FC | 2.44 | 3.35 | 2.75 |
| 03. 26/11/22 | 18:00 | Shrewsbury Town vs Peterborough United | 3.10 | 3.25 | 2.27 |
| 04. 26/11/22 | 18:00 | Hartlepool United vs Harrogate Town | 2.75 | 3.30 | 2.47 |
| 05. 26/11/22 | 20:00 | Dagenham and Redbridge FC vs Gillingham FC | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 06. 26/11/22 | 20:00 | SC Pisa vs Ternana Calcio | 2.21 | 3.30 | 3.20 |
| 07. 26/11/22 | 20:30 | Albacete Balompie vs Racing Santander | 2.27 | 3.05 | 3.30 |
| 08. 27/11/22 | 13:30 | Ankara Keciorengucu vs Samsunspor | 2.48 | 3.35 | 2.75 |
| 09. 27/11/22 | 13:30 | Pendikspor vs Eyupspor | 2.40 | 3.35 | 2.80 |
| 10. 27/11/22 | 16:00 | Burgos CF vs Real Zaragoza | 2.48 | 2.90 | 3.10 |
| 11. 27/11/22 | 16:00 | Erzurumspor FK vs Bandirmaspor | 2.34 | 3.35 | 2.90 |
| 12. 27/11/22 | 17:00 | Como 1907 vs SSC Bari | 2.85 | 3.20 | 2.46 |
| 13. 27/11/22 | 17:00 | FC Sudtirol Bolzano vs Ascoli Calcio 1898 | 2.40 | 3.15 | 3.00 |
| 14. 27/11/22 | 18:00 | CD Leganes vs Granada CF | 2.55 | 3.00 | 2.90 |
| 15. 27/11/22 | 20:00 | Palermo FC vs Venezia FC | 2.35 | 3.25 | 2.95 |
| 16 27/11/22 | 20:00 | FC Cartagena vs SD Eibar | 2.38 | 3.10 | 3.05 |
| 17. 27/11/22 | 22:00 | Spain vs Germany | 2.50 | 3.25 | 2.75 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 25/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4462 | Wales vs Iran | 2.10 | 3.14 | 3.64 |
| 14:00 | 1799 | Chengdu Qianbao vs Guangzhou RF | 1.39 | 4.37 | 6.61 |
| 14:00 | 3927 | Buriram Utd vs Ratchaburi | 1.29 | 4.87 | 8.18 |
| 14:00 | 5547 | Rayong FC vs Suphanburi | 3.06 | 3.35 | 2.11 |
| 14:30 | 5594 | Shanghai Shenhua vs Beijing Guoan | 3.35 | 3.40 | 1.97 |
| 15:00 | 4170 | Chonburi vs Port FC | 2.23 | 3.31 | 2.87 |
| 15:15 | 5478 | Tripoli SC vs AL Akhaa AL Ahli | 2.39 | 3.10 | 3.00 |
| 15:30 | 5552 | Sur vs Rustaq Club | 5.26 | 3.26 | 1.66 |
| 15:45 | 1669 | Fursan Hispania FC vs AL-Rams | 3.12 | 3.51 | 2.03 |
| 15:45 | 2508 | City Football Club vs AL Arabi | 6.61 | 4.67 | 1.36 |
| 15:45 | 3800 | Jazira Abu Dhabi vs Dibba Al Fujairah | 1.14 | 6.80 | 13.61 |
| 15:45 | 4823 | AL Bataeh (UAE) vs Al Nasr Dubai | 2.97 | 3.41 | 2.13 |
| 15:45 | 4903 | Al Nahda (Oman) vs AL Bashair | 1.34 | 4.29 | 8.39 |
| 16:00 | 1020 | MC Oran vs Olympique Akbou | 1.21 | 5.64 | 10.70 |
| 16:00 | 1161 | ES Besbes vs Irb Sedrata | 1.84 | 3.20 | 4.70 |
| 16:00 | 1249 | Fasil Kenema vs Legetafo Legedadi | 1.26 | 4.89 | 9.77 |
| 16:00 | 3107 | Geita Gold FC vs Ihefu FC | 1.65 | 3.36 | 5.06 |
| 16:00 | 3478 | ES EL Ghozlane vs ASO Chlef | 4.70 | 3.65 | 1.71 |
| 16:00 | 3864 | ES Mostaganem vs WAB Tissemessilt | 1.19 | 5.83 | 11.67 |
| 16:00 | 4534 | Qatar vs Senegal | 5.58 | 3.64 | 1.62 |
| 16:00 | 4962 | Ib Khemis El Khechna vs USM Annaba | 7.02 | 4.00 | 1.41 |
| 16:00 | 5502 | MSP Batna vs El Bayadh | 6.62 | 3.79 | 1.46 |
| 16:00 | 5697 | Skaf Khemis Miliana vs US Biskra | 6.00 | 3.70 | 1.59 |
| 17:00 | 4095 | Northeast United FC vs Mumbai City FC | 6.22 | 4.76 | 1.37 |
| 17:00 | 5290 | Sheffield United U23 vs Crewe U23 | 1.36 | 5.07 | 6.05 |
| 18:00 | 4061 | Muharraq SC vs Al Shabbab | 2.25 | 2.92 | 3.21 |
| 18:00 | 5797 | Riffa Club vs Sitra Club | 1.27 | 4.78 | 9.76 |
| 18:30 | 5904 | Al Wasl Dubai vs AL Khaleej Khor Fakkan | 1.36 | 4.67 | 6.61 |
| 19:00 | 4252 | Netherlands vs Ecuador | 1.76 | 3.50 | 4.61 |
| 19:00 | 4567 | Arsenal Tula vs Baltika Kaliningrad | 2.53 | 3.22 | 2.53 |
| 19:00 | 5671 | Bahir Dar Kenema FC vs Adama City FC | 2.57 | 3.25 | 2.48 |
| 20:00 | 4706 | Denizlispor vs Bodrumspor | 4.56 | 3.84 | 1.61 |
| 20:00 | 5584 | Akritas Chlorakas vs EN Paralimni | 2.66 | 3.16 | 2.66 |
| 21:00 | 3436 | Gloria Buzau vs Concordia Chiajna | 1.81 | 3.45 | 3.89 |
| 21:30 | 1126 | FC Martigues vs Orleans | 1.98 | 3.26 | 3.65 |
| 21:30 | 1510 | Red Star vs Nancy | 2.04 | 3.27 | 3.47 |
| 21:30 | 1782 | Saint Brieuc vs Cholet | 2.17 | 3.25 | 3.16 |
| 21:30 | 1861 | Yverdon-Sport FC vs Neuchatel Xamax | 1.92 | 3.69 | 3.26 |
| 21:30 | 1908 | Avranches vs Dunkerque | 3.16 | 3.21 | 2.18 |
| 21:30 | 1954 | Paris 13 Atletico vs Concarneau | 3.65 | 3.21 | 2.00 |
| 21:30 | 5516 | Sedan vs Bastia Borgo | 1.78 | 3.41 | 4.35 |
| 21:30 | 5854 | Le Puy vs Bourg Peronnas | 3.40 | 3.25 | 2.07 |
| 22:00 | 3729 | Anadia FC vs Felgueiras | 2.77 | 3.16 | 2.36 |
| 22:00 | 5022 | Stade Nyonnais vs FC Biel-Bienne | 1.36 | 4.87 | 6.23 |
| 22:00 | 5603 | England vs USA | 1.62 | 3.90 | 5.14 |
| 22:15 | 2819 | FC Schaffhausen vs AC Bellinzona | 2.02 | 3.59 | 3.06 |
| 22:45 | 1336 | Larne vs Coleraine FC | 1.53 | 3.88 | 5.24 |
| 22:45 | 5765 | BSC Glasgow FC vs Alloa Athletic | 5.67 | 4.30 | 1.45 |
| 23:00 | 4268 | Huesca vs Sporting Gijon | 2.25 | 3.03 | 3.28 |
| 23:45 | 1678 | Porto vs Mafra | 1.08 | 9.62 | 24.04 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Novemba 25, 2022

Nipashe




'Ujerumani ilistahili kufungwa' UKURASA 29




Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uswisi, Breel Embolo (kushoto), akifunga bao katika mechi ya Kombe la Dunia dhidi ya Cameroon iliyochezwa jana nchini Qatar. Uswisi ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Mgunda awaambia Simba safari mbichi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema matokeo ya sare ya bao 1-1 waliyopata dhidi ya Mbeya City haijamfurahisha lakini akaongeza safari ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara bado ni ndefu.

Sare hiyo ya Simba iliwafanya watani zao, Yanga kuendelea kutawala kileleni huku wakiwa nyuma kwa michezo miwili jambo ambalo linaonekana kuwanyima raha mashabiki wa Msimbazi.

Mgunga aliliambia gazeti hili matokeo hayo yalisababishwa na safu yake ya ulinzi kufanya makosa na kupelekea kugawana pointi na wenyeji.

Kocha huyo alisema mabeki wake walionyesha udhaifu lakini hawezi kuwatupia lawama wachezaji wake kwa asilimia 100 kwa sababu mechi hiyo waliyocheza ilikuwa ngumu licha ya kupambana.

"Haya ndiyo matokeo ya mpira, nilishasema toka mwanzo tulitegemea tangu awali mechi itakuwa ngumu, tulipata bao mapema, lakini kipindi cha pili nikiri kwenye safu ya ulinzi ndiyo iliyosababisha makosa hadi wenzetu kupata bao, lakini siwezi kupeleka lawama kwa wachezaji wangu.

Kwanza kutoka sare siyo dhambi, halafu leo (juzi) tumecheza na Mbeya City, ni timu bora msimu huu na ndiyo maana unaona mechi ilikuwa ngumu, niwapongeze wapinzani wetu kucheza kwa nidhamu," alisema Mgunda.

Naye Kocha Msaidizi wa Mbeya City, Antony Mwamlima, alisema pamoja kutofurahia sare kwa sababu malengo yao yalikuwa ni kupata ushindi, wanalazimika kuyapokea matokeo hayo.

INAENDELEA UK. 31

# Yanga: Hakuna atakayepona

**Na Saada Akida**

## Nabi afunguka kikosi chake sasa imara na...

WAKATI Yanga ikiendelea kutesa na rekodi yao ya Unbeaten katika Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nesreddine Nabi, amesema kikosi chake kimeimarika zaidi na sasa kiko tayari kukutana na klabu yoyote ndani ya nchi na kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**Yanga ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, mabingwa wa Kombe la FA, mabingwa wa Ngao ya Jamii na imetinga hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.**

Nabi aliliambia gazeti hili baada ya Yanga kufanya vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara na sasa anahitaji kuona nguvu hizo zinahamia kwenye michezo ya hatua ya makundi ya CAF inayotarajiwa kufanyika kuanzia Februari mwakani.

Kocha huyo alisema anajivunia namna kikosi chake kinavyopambana katika michezo yote ya Ligi Kuu Tanzania Bara waliyocheza ambapo kwa sasa wanaongoza ligi hiyo licha ya kucheza michezo miwili pungufu.

"Nina kikosi imara, kinapambana katika kila mechi ya Ligi Kuu, hili sasa ninataka wakafanye katika michuano ya kimataifa, ninajua sasa kimejengeza zaidi," alisema Nabi.

Aliongeza licha ya kutopata muda wa kutosha wa maandalizi katika michezo hiyo ya ligi, anaitumia nafasi hiyo hiyo iliyopo kuboresha kikosi chake kwa ajili ya kuwa tayari kukutana na timu yeyote kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Licha ya ratiba kuwa na michezo mfululuzio lakini wachezaji wangu wanapambana kupata pointi tatu katika kila mchezo, mechi hizi ni muhimu kwa ajili ya kufanyia kazi mapungufu kama sehemu ya maandalizi ya michuano ya CAF," alisema kocha huyo.

Mtunisia huyo alisema pia anatambua hatua wanayokwenda kucheza ni ngumu na hivyo analazimika kuandaa kikosi chake ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

"Tunasubiri ratiba ya CAF, tutajipanga kukabiliana na mpinzani yeyote atakayekuja mbele yetu, ninaimani na kikosi changu kitapata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele, hatutadharau timu yoyote, tunajua hayo ni mashindano makubwa," Nabi alisema.

Aliongeza michuano hiyo imekuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila timu watakayokutana nayo inahitaji kusonga mbele kuelekea hatua inayofuata na si kusindikiza wengine.

"Ninakiamini kikosi changu, kina uwezo wa kupambana kuhakikisha tunapata matokeo mazuri, nguvu za kwenye Ligi Kuu sasa zitahamia katika michuano ya CAF,

INAENDELEA UK. 31


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >